UNIVERSITY of RWANDA

**NDAKI YA ELIMU**
**SKULI YA ELIMU**

# NAFASI YA FASIHI ANDISHI KATIKA UKUZAJI WA STADI ZA MAWASILIANO: MFANO WA SHULE ZA SEKONDARI TEULE WILAYANI NYANZA

**NA**

**IDAHEMUKA MAGNIFIQUE**

**220018613**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA MAHITAJI YA SHAHADA YA UMAHIRI WA ELIMU KATIKA KISWAHILI NA ELIMU KATIKA CHUO KIKUU CHA RWANDA, NDAKI YA ELIMU**

**MSIMAMIZI: Dkt. WALLACE KAPELE MLAGA (PhD)**

**SEPTEMBA, 2024**

# IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, **Idahemuka Magnifique**, ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu ya asilia na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada yoyote.

Idahemuka Magnifique (220018613)

(Mtafiti)

Tarehe: 19/Septemba/2024

# ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa tasnifu yenye anwani **“Nafasi ya Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano: Mfano wa Shule za Sekondari Teule Wilayani Nyanza,**” iliandaliwa chini ya usimamizi wake na anapendekeza ikubaliwe kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri wa Elimu katika Kiswahili na Elimu ya Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu.

Dkt. Wallace Kapele Mlaga (PhD)

(Msimamizi)

Tarehe: 19/Septemba/2024

# SHUKRANI

Kwanza, shukrani zangu za dhati ziende kwa Mwenyezi Mungu aliyenipa uhai na uwezo wa kukamilisha masomo yangu.

Pili, shukrani za dhati zimfikie msimamizi wangu Dkt. Wallace Kapele Mlaga ambaye alinisaidia katika kukamilisha tasnifu hii. Kwa kweli, bila ushauri wake mzuri na mwongozo wa kitaalamu, ningekuwa na shida kukamilisha tasnifu hii kwa mafanikio. Asante kwa kujitolea kwake na ujuzi wake wa thamani ambao umeniongoza kwa mafanikio.

Tatu, ninamshukuru mke wangu Uwumuremyi Dative na binti yangu Aganze Amelia Magnificat ambao walinisaidia sana katika safari yangu ya masomo. Hawa wamekuwa nguzo zangu imara na nguvu ya kiroho kila wakati, wakinipa motisha na upendo usio na kikomo. Aidha, hawa ni baraka ambazo siku zote nitashukuru kwa kujali, kusaidia na kunipa nguvu ya kufikia malengo yangu.

Nne, ninawashukuru sana wazazi wangu Ntihemuka Danny na Nirere Josephine walionilea na kunifikisha nilipo sasa hivi. Mungu awajalie zawadi ya maisha mazuri yenye furaha na baraka.

Mwisho, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa ndugu zangu wote ambao walijinyima mengi ili niweze kukamilisha safari yangu ya masomo. Mungu awabariki sana ndugu zangu wapendwa!

# TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabaruku kwa mke wangu Uwumuremyi Dative na binti yangu Aganze Amelia Magnificat ambao walinisaidia kukamilisha tasnifu hii.

# IKISIRI

Tasnifu hii inajadili nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano: mfano wa shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Utafiti uliofanyika ulikusudia kutimiza malengo mahususi mawili. Lengo la kwanza lilikuwa kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari sekondari teule wilayani Nyanza. Lengo la pili lilikuwa kuunda miongozo ya kutumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Mawasiliano. Aidha, katika ukusanyaji wa data, utafiti ulitumia usaili, ushuhudiaji na uchanganuzi matini. Wango la utafiti lilihusisha walimu wa Kiswahili na wanafunzi wanaojifunza katika mchepuo wa LFK. Mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumiwa ili kupata sampuli ya walimu 9 na wanafunzi 93. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba fasihi andishi ina nafasi kubwa katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Kwanza, fasihi inakuza uwezo wa kuwasiliana. Pili, inakuza stadi za lugha kama kusoma, kuandika, kusikiliza na kuzungumza. Tatu, inakuza stadi ya ujasiri. Nne, fasihi andishi inachangia katika kukuza utambuzi wa hisia kwa wanafunzi. Hata hivyo, kwenye shule za sekondari teule wilayani Nyanza, walimu wa Kiswahili wanakumbana na changamoto kama mtazamo finyu kuhusu stadi za mawasiliano na tathmini zinazosisitiza zaidi stadi za kuandika na kusoma. Vilevile, kwenye shule teule kuna changamoto ya muda usiotosha na mbinu za ufundishaji zisizofaa ambazo hutumiwa na walimu kwa kukuza stadi za mawasiliano kupitia ufundishaji wa stadi za mawasiliano katika Kiswahili. Zaidi ya hayo, utafiti umeunda miongozo ya kutumia fasihi andishi kukuza stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Miongozo hii inajikita katika utumiaji wa mbinu ya mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine, uumbaji wa mazingira salama ya kujifunzia na uhusiano wenye msaada na usikilizaji kwa makini. Isitoshe, utafiti uliofanyika umedhihirisha mfano wa namna ya kufundisha fasihi kwa kuegemea kwenye miongozo ya utumizi wa fasihi andishi katika kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Mwisho, utafiti umependekeza kwamba walimu wa fasihi andishi wanalazimika kufanya juu chini ili kutumia mbinu za ufundishaji mabazo zinakuza stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu mawasiliano fasha katika lugha hii yanaweza kuwaletea wanafunzi manufaa tele.

# YALIYOMO


IKIRARI NA HAKIMILIKI ..... ii

ITHIBATI YA MSIMAMIZI ..... iii

SHUKRANI ..... iv

TABARUKU ..... v

IKISIRI ..... vi

YALIYOMO ..... vii

ORODHA YA VIELELEZO ..... xi

ORODHA YA VIFUPISHO ..... xii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ..... 1

1.1 Utangulizi ..... 1

1.2 Usuli wa Utafiti ..... 1

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti ..... 3

1.4 Malengo ya Utafiti ..... 3

1.4.1 Lengo la Jumla ..... 4

1.4.2 Malengo Mahususi ..... 4

1.5 Maswali ya Utafiti ..... 4

1.6 Umuhimu wa Utafiti ..... 4

1.7 Mawanda ya Utafiti ..... 5

1.7.1 Mawanda ya Kimaudhui ..... 6

1.7.2 Mawanda ya Kijiografia ..... 6

1.7.3 Mawanda ya Kiwakati ..... 6

1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake ..... 7

1.8 Mpangilio wa Ripoti yaUtafiti ..... 7

1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ..... 8

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA ..... 9

2.1 Utangulizi ..... 9

2.2 Stadi za Karne ya 21 ..... 9

2.3 Stadi za Mawasiliano ya Mwanadamu ..... 10

2.3.1 Stadi ya Kusikiliza kwa Makini ..... 11

2.3.2 Stadi ya Utambuzi wa Hisia ........ 11
2.3.3 Stadi ya Ujasiri ........ 12
2.4 Stadi za Lugha Dhidi ya Stadi za Mawasiliano ........ 13
2.5 Aina za Mawasiliano ya Mwanadamu ........ 15
2.5.1 Mawasiliano ya Kutumia Maneno ........ 15
2.5.2 Mawasiliano Yasiyo ya Maneno ........ 15
2.6 Nafasi ya Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano ........ 17
2.7 Hali ya Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Ujumla ........ 19
2.8 Hali ya Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano katika Lugha ya Kiswahili ........ 20
2.9 Mikakati ya Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano kupitia Ufundishaji wa Fasihi Andishi ........ 21
2.9.1 Mawasiliano ya Mtu Moja kwa Mwingine ........ 21
2.9.2 Uumbaji wa Mazingira Salama ya Kujifunzia na Uhusiano Wenye Msaada ........ 23
2.9.3 Utumiaji wa Mbinu ya Kusikiliza kwa Makini ........ 24
2.10 Mapengo ya Tafiti Tangulizi ........ 26
2.11 Kiunzi cha Nadharia ........ 27
2.12 Muhtasari wa Sura ya Pili ........ 28
SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI ........ 29
3.1 Utangulizi ........ 29
3.2 Paradima ya Utafiti ........ 29
3.3 Usanifu wa Utafiti ........ 30
3.4 Eneo la Utafiti ........ 30
3.5 Wango na Sampuli ya Utafiti ........ 31
3.5.1 Wango la Utafiti ........ 31
3.5.2 Sampuli ya Utafiti ........ 31
3.6 Mbinu za Kukusanyia Data ........ 33
3.6.1 Uchambuzi wa Matini ........ 33
3.6.2 Usaili ........ 34
3.6.3 Ushuhudiaji ........ 34
3.7 Aina ya Data Zilizokusanywa ........ 34
3.7.1 Data za Msingi ........ 34

3.7.2 Data za Upili ........ 35
3.8 Vifaa vya Utafiti ........ 35
3.9 Uchanganuzi wa Data ........ 36
3.10 Itikeli za Utafiti ........ 36
3.11 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti ........ 37
3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu ........ 37
SURA YA NNE: MJADALA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO YA UTAFITI ........ 38
4.1 Utangulizi ........ 38
4.2 Tathmini ya Nafasi ya Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano ........ 38
4.2.1 Fasihi Andishi katika Kukuza Uwezo wa Mawasiliano ........ 39
4.2.2 Fasihi Andishi katika Kukuza Stadi za Lugha Zinazohitaji katika Mawasiliano ........ 43
4.2.3 Fasihi Andishi Hukuza Stadi ya Ujasiri ........ 47
4.2.4 Fasihi Andishi katika Kukuza Stadi ya Utambuzi wa Hisia ........ 52
4.3 Miongozo ya Utumiaji wa Ufundishaji wa Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano ........ 54
4.3.1 Utumiaji wa Mbinu za Ufundishaji wa Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano ........ 54
4.3.2 Mfano wa Kufundisha Fasihi Andishi kwa Mwongozo Unaokuza Stadi za Mawasliano ........ 61
4.3 Muhtasari wa Sura ya Nne ........ 71
SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 72
5.1 Utangulizi ........ 72
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ........ 72
5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza ........ 72
5.2.2 Lengo Mahususi la Pili ........ 73
5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti Iliyotumika ........ 75
5.4 Hitimisho ........ 76
5.5 Mapendekezo ........ 77
5.5.1 Mapendekezo kwa Wanafunzi wa Wanaojifunza Fasihi Andishi kwa Kiswahili ........ 77

5.5.2 Mapendekezo Walimu Wanaofundisha Kiswahili ........................................................ 77
5.5.3 Mapendekezo kwa Watungaji wa Kazi za Fasihi Andishi katika Kiswahili ................ 78
5.5.4 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu ............................................................................. 78
5.5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ..................................................................................... 78
5.6 Muhtasari wa Sura ya Tano ............................................................................................... 79
MAREJELEO ............................................................................................................................ 80
VIAMBATISHO ......................................................................................................................... 87

# ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 1: Mfano wa Tathmini ........................................................................................ 46

Kielelezo 2: Mfano wa Andalio la Somo........................................................................... 50

# ORODHA YA VIFUPISHO

**CXR**: College du Christ- Roi

**Dkt**: Daktari wa Falsafa (PhD)

**G.S.:** Groupe Scolaire

**khj**: Keshatajwa hapo juu

**LFK**: Literature in English, French, Kinyarwanda and Kiswahili

**whj**: Wameshatajwa hapo juu.

**REB**: Rwanda Basic Education Board

**TEHAMA**: Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**TY**: Tafsiri Yetu

**uk**: Ukursa

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Sura ya kwanza ya tasnifu hii inatoa taarifa tangulizi. Kwa hiyo, sura hii inahusika na utangulizi, usuli, tamko la tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti. Aidha, sura hii inashughulika na umuhimu, mawanda, vikwazo vya utafiti, mpangilio wa utafiti na muhtasari wa sura ya kwanza.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Neno mawasiliano lina maana ya kuhamisha ujumbe kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa njia ya maneno au ya ishara (Nguyen, Warren & Fehring, 2014). Hii ina maana kwamba, mawasiliano ni mchakato wa kuhamisha habari kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine na kutoka eneo moja hadi jingine. Aidha, Ngọc (2021) anaeleza kuwa stadi za mawasiliano ni uwezo wa kuelewa, kujibu na kutoa taarifa kwa ufanisi kwa kutumia lugha, ishara au njia nyingine za mawasiliano. Zaidi ya hayo, Radhika (2020) anasema kuwa, stadi za mawasiliano hujumuisha mawasiliano ya kutumia lugha, ishara, utambuzi wa hisia pamoja na ujasiri. Maelezo haya yalitusaidia kuchunguza uelewa wa walimu kuhusu stadi za mawasiliano. Hii ni kwa sababu, kama mwalimu haelewi stadi hizi, hawezi kuzifundisha kwa ufanisi.

Kwa upande mwingine, Wamitila (2003) anasema kuwa fasihi ni kazi ya sanaa inayolenga kufunua mawazo, fikra na malengo ya jamii kwa kutumia lugha. Kwa kuongezea, Lugano (2021) Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kuwasilisha mawazo, hisia na uzoefu wa binadamu kupitia maandishi au masimulizi. Aidha, fasihi inaweza kujumuisha tanzu mbalimbali kama riwaya, tamthilia, hadithi fupi, insha, mash h airi au mitindo mingine ya uandishi au masimulizi ya kubuni (Lugano, khj). Kwa kuzingatia ufafanuzi huu, katika tasnifu hii, fasihi tunaifasili kama sanaa ya maneno inayofunua hisia na mawazo kwa kutumia ustadi wa lugha na ubunifu ili kutoa tafsiri ya kipekee ya dunia.

Katika karne ya 21, wataalamu wa nyanja mbalimbali wamependekeza stadi muhimu ambazo kila mhitimu anatakiwa kuwa nazo ili kufanikiwa kwenye soko la ajira, zikiwemo tafakuri bunifu, tafakuri tunduizi, utafiti, utatuzi wa matatizo, mawasiliano, ushirikiano, utambuzi wa kijamii, utawala binafsi, TEHAMA na ujifunzaji wa muda mrefu (Erdem na wenzake 2019). Trilling na Fadel (2009) wanarejelea stadi hizi kama stadi za karne ya 21.

Ingawa stadi hizi ni nyingi, stadi za mawasiliano zinatajwa kuwa muhimu zaidi, kwani, kama wanavyothibitisha Derakhshan, Tahery na Mirarab (2015), stadi za mawasiliano huchangia katika ukuzaji wa stadi nyingine kama vile utatuzi wa matatizo, utambuzi wa kijamii, ubunifu, na ushirikiano. Aidha, Gomatam (2015) anaongeza kuwa stadi za mawasiliano ni muhimu sana kwa maisha ya kibinafsi na kitaaluma, kwani husaidia kujenga mahusiano bora na kufanikisha majukumu ya kimaisha.

Kwa mujibu wa Sarpparaje (2019), stadi za mawasiliano ni stadi muhimu kwa wahitimu wote wa shule za sekondari ikiwemo wa michepuo ya lugha. Hii ni kwa sababu, stadi hizi zinahitajika katika kila kazi za kitaalamu na maeneo mbalimbali kama sheria, elimu, serikali na teknolojia (Paul & Reem, 2004). Zaidi ya hayo, Melly, & Mohochi (2023) wanasema kwamba stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili ni stadi muhimu ambazo zinaweza kuwasaidia raia wa ukanda wa Afrika Mashariki kufanikisha shughuli zao za kila siku zikiwemo mawasiliano ya kikanda, bishara na siasa.

Hata hivyo, utafiti wa Pradesh, Toppo & Philomina (2021) unaonesha kuwa wahitimu wengi katika shule za sekondari wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa stadi za mawasiliano. Hii inatokana kuzingatia mbinu za ufundishaji zinazoweka mkazo katika maarifa ya kitaaluma na nadharia kuliko kuendeleza stadi za mawasiliano kupitia vitendo (Rachella, 2021). Athari yake ni kwamba wanafunzi wanapohitimu masomo, wanashindwa kujiamini kwenye soko la ajira (Sridhar, 2012). Hili lilichochea shauku yetu ya kutaka kuelewa hali ipoje katika madarasa ya lugha nchini Rwanda ili tutoe mapedekezo yatakayoboresha ufanisi wa ufundishaji wa stadi za mawasiliano ikiwa kuna dosari yoyote.

Kwa hiyo, ufundishaji wa fasihi simulizi na andishi ni muhimu katika kukuza stadi za mawasiliano katika shule za sekondari (Figueroa-Macias & Andrade-Zambrano, 2022; Bisamaza, 2022). Hii ni kwa sababu, ufundishaji wa fasihi unaweka mkazo katika matumizi ya lugha kisanaa, ambayo inaweza kusaidia wanafunzi kuendeleza stadi za lugha muhimu kwa mawasiliano sahihi, kama ilivyoelezwa na Rao & Charyulu (2015). Hata kama fasihi andishi na fasihi simulizi ni muhimu katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano, kwenye utafiti wetu, tulisisitiza fasihi andishi dhidi ya fasihi simulizi.

Hii ni kwa sababu inatoa nafasi kubwa ya ufundishaji wa lugha kupitia maandishi, ambayo ni muhimu kwa wanafunzi wa shule za sekondari (Derakhshan, Tahery & Mirarab, 2015). Vilevile, katika enzi za sasa, fasihi andishi inatumiwa zaidi ikilinganishwa na fasihi simulizi (Gomatam, 2015). Fasihi andishi inawawezesha wanafunzi kujifunza kutumia lugha kwa ustadi kupitia uandishi na usomaji. Hivyo, ufundishaji wa fasihi andishi unaweza kuwa suluhisho la kuboresha uwezo wa wanafunzi katika mawasiliano, na hivyo kufanya ufundishaji wa fasihi andishi kuwa chaguo muhimu katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano.

Licha ya maelezo yanayotolewa katika tafiti za Figueroa-Macias & Andrade-Zambrano (whj), bado tuliona kuwa, tafiti hizi zina mapengo ambayo yanafaa kujazwa. Mosi, tafiti husika zinazungumzia fasihi kwa ujumla katika Kiingereza bila kuhusisha fasihi mahususi. Vilevile, utafiti wa Bisamaza (khj) unajikita kwenye nafasi ya fasihi simulizi katika ukuzaji wa stadi ya kusikiliza na kuzungumza Kiswahili. Tunafikiri kuwa stadi hizi pekee hazitoshi kukuza stadi za mawasiliano kwa ujumla wake. Hivyo basi, kutokana na hali hii, tulipata shauku ya kufanya utafiti wetu kwa ajili ya kuziba mapengo hayo kwa kuchunguza nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Stadi za mawasiliano ni stadi muhimu kwa wahitimu wote wa shule za sekondari ikiwemo wa michepuo ya lugha (Sarpparaje, 2019). Aidha, stadi za mawasiliano zinahitajika katika kila kazi za kitaalamu na maeneo mbalimbali kama sheria, elimu, serikali na teknolojia (Erdem, Bağcı, Koçyiğit, Altıner, Saykili, Polat & Eğmir, 2019). Ufundishaji wa fasihi simullizi na andishi umeonesha kama njia mwafaka ya kufanikisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari (Figueroa-Macias & Andrade-Zambrano, 2022; Bisamaza, 2022). Licha ya maelezo haya, wahitimu wengi katika shule za sekondari hawana stadi za mawasiliano (Pradesh, Toppo, & Philomina, 2021). Hii inaathiri sana mafanikio yao kwa kuwapunguzia uwezo wa kujiamini (Sridhar, 2012). Kutokana na hali hii, tuliamua kufanya utafiti ili kuchunguza nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti tuliofanya yanagawanyika katika lengo la jumla na malengo mahususi.

### 1.4.1 Lengo la Jumla

Lengo la jumla la utafiti lilikuwa ni kuchunguza nafasi ya ufundishaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Utafiti uliofanyika ulitimiza malengo mahususi mawili:

i) Kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza

ii) Kuunda miongozo ya kutumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi ya mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza

## 1.5 Maswali ya Utafiti

i) Je, fasihi andishi ina nafasi gani katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza?

ii) Je, tunaweza kuunda miongozo gani ya kutumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Stadi za mawasiliano ni muhimu katika mafanikio ya kila siku, na ukosefu wa stadi hizi unaweza kuleta changamoto katika maeneo ya kazi na maisha binafsi. Martín (2014) anasisitiza kuwa kutokuwa na stadi za mawasiliano kunaweza kuathiri utendaji kazi na mahusiano ya kibinafsi.

Hivyo, utafiti uliofanyika ulilenga kuchunguza nafasi ya ufundishaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Matokeo ya utafiti uliofanyika yatakuwa muhimu kwa wanafunzi, walimu, wapangaji wa sera, watafiti na wadau wote katika sekta ya elimu ifuatavyo: mosi, yatasaidia ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Hii ni kutokana na kuwa, matokeo husika yametoa mwanga kuhusu mbinu bora za kutumia ufundishaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano.

Pili, walimu watanufaika kwa kufahamu namna ambavyo ufundishaji wa fasihi andishi unaweza kuchangia katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi.

Kuelewa mchango wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano, kutawawezesha walimu hasa wa Kiswahili kubuni mikakati bora zaidi ya kufundisha fasihi andishi ili kuwawezesha wanafunzi kuwasiliana kwa ufasaha. Hii itawapa walimu uwezo wa kubadilisha mbinu zao za kufundisha ili kuzingatia mahitaji ya mawasiliano ya wanafunzi katika mazingira ya elimu.

Tatu, yatawasaidia pia wapangaji wa sera kuelewa baadhi ya changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi katika kukuza stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili na namna ya kuzikabili kupitia ufundishaji wa fasihi andishi. Matokeo ya utafiti pia, yataweza kuathiri sera za elimu katika ngazi za kijamii na kitaifa.

Kwa kuwa tasnifu hii inatoa ushahidi kwamba fasihi andishi ina mchango mkubwa katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano, watunga sera watapata hamasa ya kuchukua jitihada za ziada za kuimarisha ufundishaji wa fasihi andishi ili kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi.

Nne, yatakuwa muhimu kwa watafiti wengine watakaokusudia kufanya utafiti kuhusu stadi za mawasiliano na fasihi andishi. Matokeo ya utafiti husika yatawasaidia kuelewa zaidi uhusiano kati ya ufundishaji wa fasihi andishi na ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Hii itatoa mwongozo na msingi imara kwa wanafunzi wengine wa tasnia ya elimu kufanya tafiti zaidi kuhusu stadi za mawasiliano na fasihi andishi katika muktadha wa elimu.

Mwisho, matokeo ya utafiti yatakuwa faafu kwa wadau mbalimbali katika sekta ya elimu, wakiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali, wafadhili na wazazi. Matokeo haya yatatoa taarifa muhimu na za kuaminika kuhusu mchango wa ufundishaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano. Aidha, matokeo haya yatawamotisha wadau wa elimu kutoa mchango wao ili kuimarisha ufundishaji wa fasihi andishi kwa ajili ya kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi.

### 1.7 Mawanda ya Utafiti

Utafiti uliofanyika ulijumuisha mawanda tofauti kama inavyobainishwa hapa chini:

### 1.7.1 Mawanda ya Kimaudhui

Kuna mikakati mingi inayoweza kutumika katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa wanafunzi. Licha ya wingi wa mikakati hii, ikiwemo utumiaji wa TEHAMA (Rogers, 2017) na fasihi simulizi (Bisamaza, khj), kimaudhui, utafiti uliofanyika ulizingatia tu nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza nchini Rwanda.

### 1.7.2 Mawanda ya Kijiografia

Utafiti ulifanyika katika Wilaya ya Nyanza, Mkoa wa Kusini nchini Rwanda. Utafiti huu ulijumuisha tarafa tano ambazo ni Busasamana, Rwabicuma, Kigoma, Cyabakamyi na Mukingo. Utafiti ulijikita katika shule za sekondari tano zilizochaguliwa kutoka kwenye tarafa hizo.

Wilaya ya Nyanza haipakani na nchi yoyote inayotumia Kiswahili, na haina masoko makubwa yanayoweza kuvutia wafanyabiashara wa kimataifa, wakiwemo watumiaji wa Kiswahili. Hii ina maana kwamba wilaya ya Nyanza haina idadi kubwa ya watumiaji wa Kiswahili. Pia, wilaya ya Nyanza inachukuliwa kama kitovu cha utamaduni wa Rwanda (Bizimana, 2022). Hii inachochea wakazi wa wilaya ya Nyanza kupendelea matumizi ya Kinyarwanda kama lugha inayohifadhi utamaduni wa Rwanda dhidi ya lugha nyingine zinazotumiwa nchini Rwanda. Hivyo, mawasiliano kwa Kiswahili yako kwa kiwango cha chini katika wilaya husika ikilinganishwa na baadhi ya maeneo mengine nchini Rwanda.

Kwa hiyo, utafiti uliofanyika ulijikita kwenye wilaya husika ili kutoa mwanga kwa walimu kuhusu jinsi wanavyoweza kukuza stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi katika mazingira yao kupitia ufundishaji wa fasihi andishi.

### 1.7.3 Mawanda ya Kiwakati

Kipindi cha wakati kilichoshughulikiwa ni kuanzia mwaka 2023 hadi 2024. Lengo kuu lilikuwa ni kuchunguza nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi ya mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Kipindi hiki kilichaguliwa ili kuchunguza mabadiliko ya hivi karibuni katika elimu, hususan jinsi fasihi andishi imechangia kuboresha mawasiliano ya wanafunzi katika mazingira mapya ya kujifunza. Pia, kinatoa nafasi ya kutathmini athari za mipango ya serikali na mashirika katika kuboresha elimu kati ya mwaka 2023 na 2024.

### 1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Kwa kukamilisha utafiti, mtafiti alikumbana na vikwazo mbalimbali. Aya zinazofuata zinafafanua hivyo na namna vilivyotatuliwa

Kwanza, mtafiti alikabiliwa na kikwazo cha kuchelewa kupewa kibali cha kukusanya data kutoka kwa Wilaya ya Nyanza. Ili kukabiliana na kikwazo hiki, mtafiti alilazimika kwenda katika ofisi ya wilaya na kuwaelezea viongozi wa wilaya jinsi kuchelewa kupata kibali husika kunavyoweza kumcheleweshea mtafiti kukamilisha utafiti wake. Baada ya kuzungumza na viongozi wa wilaya, kibali kilitolewa.

Pili, kuna shule ambayo mtafiti alienda kukusanya data, lakini uongozi wa shule hiyo ukamzuia kwa kusema kwamba hawana taarifa kutoka kwa wilaya kuhusu ukusanyaji wa data huo. Mtafiti alionesha kibali kutoka wilayani, lakini kiongozi wa shule alikataa kwa kusema kwamba shule inapaswa kujulishwa kwa simu au kwa barua pepe. Ili kuepuka kikwazo hiki, mtafiti aliwasiliana na uongozi wa Wilaya ya Nyanza, na shule ikapewa baruapepe kutoka wilayani. Hatimaye, mtafiti alipata idhini ya kukusanya data katika shule husika.

Mwisho, baada ya kuanza mchakato wa ukusanyaji data, ilionekana kwamba baadhi ya walimu wa Kiswahili hawakuweza kujibu maswali ya mahojiano kwa kusema kwamba ni magumu. Hapa, mtafiti alijaribu kuwaelezea kila swali ili kuwapa mwelekeo wa utafiti.

Licha ya haya, bado kulikuwepo washiriki wa utafiti ambao hawakujibu maswali yote kwa kusema kwamba wangepewa muda wa kutosha ili kutafakari kuhusu maswali hayo. Ili kuepukana na kikwazo hiki, mtafiti alituma maswali ya mahojiano kwa washiriki wa utafiti kupitia ujumbe WatsApp au baruapepe siku mbili kabla ya mahojiano kufanyika. Hili lilifanyika ili washiriki wa utafiti wawe na taarifa kuhusu mahojiano watakayoyafanya.

### 1.8 Mpangilio wa Ripoti yaUtafiti

Tasnifu hii ina sura kuu tano. Sura ya kwanza inahusu utangulizi. Sura ya pili inajadili mapitio ya maandiko. Sura ya tatu inahusika na methodolojia ya utafiti. Sura ya nne inajumuisha mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Sura ya tano inajumuisha muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo.

### 1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura ya kwanza inatoa taarifa za utangulizi kuhusu utafiti. Sura hii inajumuisha sehemu tofauti ambazo ni: utangulizi, usuli, tamko la tatizo, malengo na na maswali ya utafiti. Pia, sura hii inashughulika na umuhimu vikwazo na mawanda ya utafiti, mpangilio wa utafiti na muhtasari wa sura ya kwanza. Sehemu inayofuata ni mapitio ya maandiko na kiunzi cha nadharia.

# SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura ya pili inahusu mapitio ya maandiko kuhusu mada zinazohusiana na mada ya utafiti. Kwa hiyo, sura hii inagawanyika katika sehemu zifuatazo: utangulizi, stadi za karne ya 21, stadi za mawasiliano ya mwanadamu, stadi za lugha dhidi ya stadi za mawasiliano na aina za mawasiliano ya mwanadamu. Aidha, sehemu inahusisha mapitio ya maandiko kuhusu nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano, hali ya ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa ujumla, hali ya ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili na mikakati ya ukuzaji wa stadi za mawasiliano kupitia ufundishaji wa fasihi andishi. Vilevile, sehemu hii inabainisha mapengo ya tafiti tangulizi, kiunzi cha nadharia na muhtasari.

## 2.2 Stadi za Karne ya 21

Karne ya 21 imekuwa kipindi cha mparaganyiko mkubwa wa uhusiano wa kijamii, ambapo maendeleo katika sayansi, teknolojia na utandawazi yamebadilisha mienendo ya dunia (Bennett, 2002; Dennis & Powell, 2011). Mabadiliko haya yamechochea ulimwengu kufikiria stadi za ziada za kukabiliana na mabadiliko hayo (Bennett, khj). Kwa mujibu wa Ahmad, Jailani & Yunus (2011), tangu miaka ya 1980, wataalamu katika nyanja mbalimbali wamekuwa wakipendekeza stadi muhimu zinazohitajika ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira katika karne hii. Stadi hizi zilipewa majina tofauti kama vile stadi za kuhamishwa, stadi za karne ya 21, stadi za jumla, uwezo wa jumla au stadi laini (Bennett, 2002; Peck, 2005; Ahmad, Jailani & Yunus, khj; Dennis & Powell na whj, REB, 2015). Ingawa majina mbalimbali yametolewa na watafiti tofauti, katika tasnifu hii, stadi hizo zinarejelewa kwa jumla kama stadi za karne ya 21.

Stadi za karne ya 21 ni muhimu katika kukabiliana na changamoto za maisha katika mazingira tofauti (Barman & Konwar, 2011; Sylvester, 2022). Peck (2005) anaongeza kuwa stadi hizi zinaweza kutumika katika elimu kusaidia wanafunzi kuwaza kwa kina na kuelewa masomo kwa undani. Kwa hivyo, katika tasnifu hii, stadi za karne ya 21 zimerejelewa kama stadi zinazomwezesha mtu kukabiliana na changamoto tofauti za kimaisha katika mazingira mbalimbali na kumsaidia kufaulu maishani mwake.

Stadi za karne ya 21 zinajumuisha uwezo mbalimbali kama vile tafakuri tunduizi, tafakuri bunifu, utafiti, mawasiliano, ushirikiano, utawala binafsi, ujuzi wa kijamii, utatuzi wa matatizo na TEHAMA (Barman & Konwar, 2011; Niyirora & Mlaga, 2022).

Stadi za karne ya 21 zina umuhimu mkubwa katika mafanikio ya kimaisha, hasa katika enzi za kidijiti, kama inavyodhihirishwa na Erdem na wenzake (2019). Hata hivyo, stadi za mawasiliano bado zina jukumu kuu katika kuendeleza stadi nyingine zote za karne ya 21. Hii ni kwa sababu stadi za mawasiliano husaidia katika ujenzi wa mahusiano na ushirikiano na watu wengine (Novik, 2015). Jambo hili ni muhimu katika kujenga uwezo wa kufikiri kwa kina, kufanya maamuzi bora na kutatua matatizo. Aidha, stadi za mawasiliano zinaweza kutoa msingi wa maarifa na ujuzi wa kiteknolojia (Novik, khj). Stadi za mawasiliano ni muhimu kwa kuimarisha uwezo wa kufanikiwa katika maisha kwa ujumla.

Kwa hiyo, kutokana na maelezo haya, inaonekana kwamba stadi za mawasiliano ni stadi muhimu kwa kuwa zinatoa mchango mkubwa katika ukuzaji wa stadi nyingine za karne ya 21. Hii ni kwa sababu stadi hizi zinasaidia kujenga mahusiano mema na kufanikisha utimizaji wa majukumu ya kimaisha. Kuna madai kuwa wanafunzi wana kiwango cha chini cha stadi za mawasiliano (Pradesh, Toppo, & Philomina, 2021). Hii ilitufanya kupata shauku ya kufanya utafiti ili kuchunguza mchango wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza, nchini Rwanda. Hii ni licha ya fasihi andishi kudaiwa kuwa inakuza stadi a mawasiliano (Figueroa-Macias & Andrade-Zambrano, 2022).

### 2.3 Stadi za Mawasiliano ya Mwanadamu

Stadi za mawasiliano ni uwezo wa kuelewa, kutoa taarifa na kushirikiana kwa ufanisi kwa kutumia lugha na njia mbalimbali za mawasiliano (Al-Alawneh, Hawamleh, Al-Jamal & Sasa, 2019). Stadi za mawasiliano ni muhimu kwa mafanikio kazini na maisha kwa ujumla, hasa katika enzi hizi za maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia. Dunia inayogeuka kuwa kijiji kimoja inathibitisha umuhimu wa stadi hizo. Kwa hiyo, tuliamua kupitia maandiko kuhusu stadi za mawasiliano ya mwanadamu. Jambo hili lilifanyika kwa kuwa tuliamini kwamba litatusaidia kuchunguza nafasi ya ufundishaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

Hivyo basi, sehemu hii inahusisha sehemu tatu ambazo ni stadi za kusikiliza kwa makini, stadi ya ujasiri na stadi ya utambuzi wa hisia.

### 2.3.1 Stadi ya Kusikiliza kwa Makini

Kusikiliza kwa makini ni ujuzi muhimu wa mawasiliano ambao unahusisha kujitolea kwa makini kwa anayesikiliza kusikiliza kwa ustadi na kuepuka kuvuruga mawazo wakati wa mazungumzo (Friston, Sajid, Quiroga, Parr, Price & Holmes, 2021). Stadi hii inajumuisha kuondoa vikwazo vya mawazo na kuelekeza fikira kwa mzungumzaji. Pia, stadi husika ina sehemu kuu tatu: kuonesha ishara za kimwili za kusikiliza, kuuliza maswali kwa uwazi ili kuthibitisha uelewa na kuepukana na kuvuruga mazungumzo. Kwa kufanya hivyo, mtu anaweza kusikiliza kwa makini na kuelewa kikamilifu ujumbe wa mzungumzaji.

Aidha, ukuzaji wa stadi ya kusikiliza kwa makini unaweza kuboresha mahusiano na kujenga uelewa thabiti katika mazungumzo. Kwa hiyo, ni muhimu kutambua kwamba kusikiliza kwa makini sio kipaji cha kuzaliwa ila mtu hujifunza (Friston na wenzake, whj). Hii ni kwa sababu kusikiliza kwa makini kunamhitaji mtu kuzingatia kabisa kile kinachosemwa bila kuingiliwa na mawazo au maoni ya mtu mwingine. Kwa kujitolea katika kusikiliza, mtu anaweza kuboresha uwezo wake wa kuelewa, kuheshimu wengine na kujenga mahusiano ya kina na ya kweli.

Hata hivyo, utafiti wa Friston na wenzake (whj) unajikita katika stadi za kusikiliza kwa makini katika lugha ya Kiingereza, ambayo si sawa na lugha ya Kiswahili iliyoshughulikiwa katika utafiti uliofanyika. Hivyo, kutokana na hali hii, tulitamani kuelewa pale uwandani mbinu zinazotumiwa na walimu wa Kiswahili katika ukuzaji wa stadi ya kusikiliza kwa makini kupitia ufundishaji wa fasihi andishi. Utafiti wetu ulifanyika kwa kuzingatia muktadha na mazingira ya Kiswahili katika wilaya ya Nyanza, Rwanda.

### 2.3.2 Stadi ya Utambuzi wa Hisia

Utambuzi wa hisia ni uwezo wa kuelewa, kutambua na kuhisi hisia za watu wengine (Valente, 2016). Hii inamaanisha kwamba utambuzi wa hisia ni uwezo wa kutambua namna ambavyo mtu mwingine anajihisi au kuelewa hali ya mtu mwingine ya kihisia, hata bila ya kusemwa wazi. Valente (khj) anaendelea kusema kuwa utambuzi wa hisia hujumuisha uwezo wa kufahamu hisia za watu wengine, kusoma ishara za kihisia kama vile hali ya mwili, sauti, tabia zinazoonesha

hisia na kujaribu kuelewa mtazamo wa kihisia wa watu katika muktadha wa mawasiliano au hali fulani.

Licha ya maelezo haya, Valente (2016) hajaeleza moja kwa moja jinsi stadi ya utambuzi wa hisia inavyoweza kukuzwa kupitia ufundishaji wa fasihi andishi. Kwa hiyo, tulipata shauku ya kufanya utafiti wetu, ili tubainishe namna ambavyo stadi hii huweza kukuzwa kupitia ufundishaji wa fasihi andishi katika Kiswahili.

Kutambua hisia za wengine ni muhimu katika kuboresha mawasiliano kwa sababu inamruhusu mtu kurekebisha njia yake ya kuwasiliana kulingana na hisia za wengine. Kwa mfano, kulingana na Rustham, Rusadi, Sakinah, Kristanti & Cholisha (2022), mtu akigundua kwamba mtu mwingine anaonesha hasira au mshangao, utambuzi wa hisia unaweza kumsaidia kutambua hali hiyo na hata kuzipunguza hisia hizo. Aidha, stadi ya utambuzi wa hisia inawezesha mzungumzaji sio tu kuzoea kile ambacho wasikilizaji wake wanahitaji kusikia, bali pia jinsi gani wanahitaji kusikia na mahali wanapohitaji kusikia. Stadi hii pia husaidia mzungumzaji kuelewa mtindo gani unaofaa kwa wasikilizaji na nini hasa wanatafuta kusikia mwanzoni. Rustham na wenzake (whj) wamejadili umuhimu wa stadi hii katika mazingira ya mawasiliano yenye ufanisi, lakini bado hawakutoa njia za vitendo au mbinu za kufundisha ambazo zinaweza kutumika kuimarisha utambuzi wa hisia.

Kwa hiyo, tulipata shauku ya kutafiti ili kuona namna walimu wa shule za sekondari wanavyotekeleza mikakati ya ukuzaji wa stadi za utambuzi wa hisia kupitia ufundishaji wa fasihi andishi katika Kiswahili. Matokeo ya utafiti yatasaidia kutoa mwongozo kwa walimu juu ya mbinu bora za kufundisha fasihi andishi ili kuimarisha utambuzi wa hisia miongoni mwa wanafunzi, na hivyo kuboresha mawasiliano na uelewa wao wa hisia katika muktadha wa kijamii na kitaaluma.

### 2.3.3 Stadi ya Ujasiri

Kulingana na Azimova (2020), ujasiri ni hali ya kuonesha imani na uhakika bila woga au shaka katika mawasiliano, vitendo, na maoni, huku ukisimamia maamuzi kwa ukakamavu. Aidha, ujasiri husaidia kuwasilisha mawazo kwa ufanisi bila kukata tamaa na kufanya vitendo bila kujali matokeo. Atkin (2012) anaeleza kwamba ujasiri unawezesha mtu kuvuka vikwazo na kushughulikia mambo kwa utulivu na ufanisi. Ingawa Atkin (khj) & Azimova (khj) wanajadili

ujasiri kwa kina, utafiti wao unahusu lugha ya Kiingereza, ambayo inaweza kuwa tofauti na muktadha wa lugha ya Kiswahili.

Katika muktadha wa mawasiliano, ujasiri ni muhimu sana kwani husaidia katika kuwasilisha mawazo kwa ufanisi na kwa uwazi. Kama ilivyoelezwa na Azimova (khj), watu wenye ujasiri hawana woga wa kuwasilisha maoni yao kwa sababu wanaamini katika uwezo wao na thamani ya mchango wao.

Hii inaweza kusaidia kujenga mazingira ya kazi yanayowahimiza wengine kushiriki na kutoa mawazo yao kwa hiari. Zaidi ya hayo, ujasiri huchangia katika kujenga imani ya kibinafsi na kujiamini. Imani hii inawawezesha watu kukabiliana na changamoto tofauti kwa namna ambayo inawapa nguvu na uwezo wa kukabiliana na hali yoyote isiyotarajiwa (Atkin khj). Hii inaleta athari chanya ya kujenga ustahimilivu na uimara katika kukabiliana na hali ngumu za kazi au za maisha kwa ujumla.

Licha ya maelezo ya Atkin (khj) & Azimova kuhusu maana na umuhimu wa stadi ya ujasiri katika mawasiliano, bado watafiti hawa hawajaonesha mbinu mwafaka za kukukuza stadi ya ujasiri miongoni mwa wanafunzi wa lugha ikiwemo Kiswahili. Hivyo basi, tuliamua kufanya utafiti wetu ili kubainisha jinsi stadi ya ujasiri inavyoweza kuimarishwa kupitia ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyanza, Rwanda. Lengo letu lilikuwa kuunda njia za vitendo zitakazochangia katika kukuza ujasiri miongoni mwa wanafunzi, na hivyo kuchangia katika maendeleo yao binafsi na mawasiliano katika lugha ya Kiswahili.

### 2.4 Stadi za Lugha Dhidi ya Stadi za Mawasiliano

Stadi za lugha zinahusu uwezo wa mtu kutumia lugha kwa usahihi na ufanisi, ambapo zinajumuisha kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika (Sen, Mahendra, & Patnaik, 2015). Kusikiliza ni ustadi wa kuelewa na kuchambua sauti na maneno yanayosemwa. Kuzungumza ni uwezo wa kueleza mawazo kwa usahihi kwa kutumia maneno. Vilevile, kusoma ni umahiri wa kuelewa na kutafsiri maandishi, huku kuandika ni uwezo wa kuwasilisha mawazo kwa maandishi. Hivyo, stadi hizi ni muhimu katika uundaji wa ujumbe na ufafanuzi wa maana katika muktadha wa lugha. Hii inatokana na kwamba stadi hizi zinamwezesha mtu kuelewa na kutoa taarifa kwa njia ya maneno kwa usahihi.

Kwa upande mwingine, stadi za mawasiliano zinahusisha uwezo wa kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali. Stadi hizi zinajumuisha matumizi ya lugha ya mwili, toni ya sauti na uwasilishaji wa ujumbe kwa uwazi na kueleweka (Seiler & Beall, 2011). Ngọc (2021) anaongezea kwamba stadi za mawasiliano zinajumuisha uwezo wa kuelewa, kujibu na kutoa taarifa kwa ufanisi kwa kutumia lugha, ishara na njia nyingine za mawasiliano. Kwa hivyo, stadi za mawasiliano zinahitajika ili kuimarisha ujumbe unaowasilishwa kwa njia ya maneno au isiyo ya maneno, kwa kutumia zinazofaa na kuzingatia mazingira ya mawasiliano.

Aidha, stadi za lugha na stadi za mawasiliano zina uhusiano wa karibu kwani zote zinasaidia katika mawasiliano bora na yenye ufanisi. Stadi za lugha, kama vile kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika, zinachangia kuhakikisha kwamba ujumbe unaotolewa unaeleweka vizuri kupitia maneno (Sen, Mahendra, & Patnaik, 2015). Kwa kuongezea, stadi za mawasiliano, kama vile matumizi ya lugha ya mwili na toni ya sauti, huimarisha uwasilishaji wa ujumbe na kusaidia katika utambuzi wa hisia na nia za mzungumzaji. Kwa hiyo, stadi hizi hufanikisha mawasiliano bora na yenye ufanisi zaidi (Gamble & Gamble, 2014).

Kwa hivyo, stadi za lugha na mawasiliano zinapounganishwa, zinasaidia kufanikisha mawasiliano yenye nguvu, ufanisi, na yanaeleweka kwa urahisi kupitia matumizi ya maneno, lugha ya mwili, na toni ya sauti. Hivyo basi, kutokana na haya tuliyoyaona kwenye mapitio ya maandiko, tulipata shauku ya kufanya utafiti ili kuchunguza nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za lugha na mawasiliano. Utafiti ulitarajia kuboresha ufanisi wa mawasiliano katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa sekondari.

Pia, ulitarajia mwongozo kwa walimu na watunga sera kuhusu mbinu bora za kufundisha fasihi andishi ili kukuza stadi za mawasiliano katika Kiswahili miongoni mwa wanafunzi.

Hivyo basi, kutokana na haya ambayo tumeyaona kwenye mapitio ya maandiko, tulipata shauku ya kufanya utafiti ili kuchunguza nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za lugha na za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza ili kuboresha ufanisi wa mawasiliano katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa sekondari wilayani Nyanza.

### 2.5 Aina za Mawasiliano ya Mwanadamu

Sehemu hii inahusisha sehemu mbili. Kwanza ni mawasiliano. Pili, ni mawasiliano yasiyo ya maneno.

#### 2.5.1 Mawasiliano ya Kutumia Maneno

Lugha ni zana muhimu ya mawasiliano baina ya watu katika jamii. Katika mawasiliano, kunatumiwa mfumo wa sauti, herufi na maneno ilikueleza mawazo na hisia mbalimbali ndani ya muktadha wa tamaduni na jamii husika (Wamitila, 2003).

Mawasiliano ya kutumia maneno ni aina ya mawasiliano inayotegemea maandishi au mazungumzo kubadilishana habari, na huchukuliwa kuwa njia ya mawasiliano rasmi na ya kuaminika (Sirbu, 2015). Hata hivyo, lugha inazidi kuwa na utajiri zaidi ya maneno tu, ikijumuisha tamaduni, desturi na mifumo ya maana inayowezesha watu kufikisha ujumbe wao kwa njia yenye maana na utambulisho wa kipekee.

Uwezo wa lugha kubeba hisia, maana iliyofichika na muktadha wa kijamii huongeza kina cha mawasiliano. Jambo hili linaruhusu ujumbe kufikishwa kwa njia inayoeleweka na kuheshimiwa na wale wanaopokea ujumbe huo. Hivyo, mawasiliano ya kutumia maneno huleta watu karibu, hufanya mawasiliano kuwa ya kibinafsi na huwezesha kubadilishana ujuzi na maarifa kati ya jamii mbalimbali (Sirbu, khj). Kwa ufupi, mawasiliano ya kutumia maneno ni njia inayowezesha watu kubadilishana ujumbe kwa kutumia sauti, maneno au maandishi katika lugha fulani.

Licha ya maelezo yaliyotolewa na Sirbu (khj), utafiti wake una mapengo. Kwanza, mtafiti huyu aliongelea mawasiliano ya kutumia maneno kwa ujumla bila kuhusisha lugha mahususi. Pili, mtafiti huyu alizungumzia dhana ya mawasiliano ya kutumia maneno bila kuonesha namna ambavyo mawasiliano husika yanaweza kuimarishwa miongoni mwa wanafunzi hasa katika madarasa ya lugha. Hivyo basi, utafiti uliofanyika ulikusudia kuyaziba mapengo yaliyodhihirika kwa kuchunguza nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyanza.

#### 2.5.2 Mawasiliano Yasiyo ya Maneno

Kwa mujibu wa Pearson, Nelson, Paul, Titsworth & Hosek (2017), mawasiliano yasiyo ya maneno ni mchakato wa kutuma ujumbe kwa wengine bila kutumia maneno, ambapo tabia kama

vile sura, mienendo ya uso, na ishara za sauti hutumiwa. Mawasiliano haya yanajumuisha matumizi ya ishara za mwili, alama au ishara nyingine zenye maana kulingana na muktadha wa mahusiano yao (Hartley & Karinch, 2007). Kwa mfano, watu wanaweza kutumia ishara za mikono na mienendo ya uso kubadilishana fikra na mawazo katika muktadha wa mawasiliano yasiyo ya maneno.

Hata hivyo, ili mawasiliano haya yatokee, mtu anahitaji uwezo wa kufikiri pamoja na ufahamu wa jamii anayoshiriki na muktadha wa mawasiliano (Mehrabian & Wiener, 1967). Hata hivyo, maelezo haya hayajaonesha namna ya kukuza mawasiliano yasiyo ya maneno.

Mawasiliano yasiyo ya maneno ni muhimu sana katika maisha ya kila siku ya binadamu. Tunatumia ishara kama vile tabasamu, kuashiria kwa kidole, mwenendo wa mwili na mawasiliano ya uso ili kuthibitisha uelewa wetu na kuhakikisha tunaelewa kwa usahihi wanachosema watu (Mehrabian & Wiener, whj). Hii ni muhimu sio tu kwa watu wenye ulemavu wa kusikia, bali pia katika mazingira mengine kama elimu kwa watoto wenye uwezo mkubwa wa kufahamu ishara, mazingira yenye kelele, utalii au hata katika muziki.

Kwa mujibu wa Pearson na wenzake (whj), kati ya asilimia 60 na 90 ya tabia zetu za mawasiliano ya kila siku hutendeka kwa njia isiyokuwa ya maneno. Hii inaonesha umuhimu wa kuzingatia mawasiliano yasiyo ya maneno katika mchakato wa mawasiliano, hasa kwa watu wanapotegemea zaidi ishara zisizo za maneno wakati wa kuelewa hisia za wengine au kufikisha ujumbe.

Hata hivyo, mara nyingi watu hukutana na ugumu wa kufasiri kanuni za mawasiliano yasiyo ya maneno kwa sababu wanatumia kanuni zile zile kuwasilisha maana tofauti (Yang, 2011). Pia, hutumia kanuni mbalimbali kuwasilisha maana moja. Hii inaweza kusababisha mkanganyiko na tafsiri zisizo sahihi za ujumbe unaotolewa. Ili kuepuka changamoto hizi, ni muhimu kuzingatia vigezo vyote katika kila hali ya mawasiliano na kutumia kanuni zote zisizo za maneno.

Changamoto za mawasiliano yasiyo ya maneno zinaweza kutatuliwa kwa kutumia mbinu tofauti (Pearson na wenzake, whj). Kwanza, kutumia mbinu ya mipaka ya mawasiliano, ambayo inahusisha matumizi ya nafasi na umbali wa binadamu. Pili, kutumia mbinu inayohusu jinsi watu wanavyoandaa na kutumia muda na ujumbe unaotokana na mpangilio wa muda huo. Tatu,

mawasiliano ya mguso yanaweza kutumiwa. Mbinu hii inajihusisha na matumizi ya mguso katika mawasiliano. Nne, kuzingatia vigezo vyote katika kila hali ya mawasiliano na kutumia maoni ya kuelezea kila ujumbe ili kupunguza tafsiri zisizo sahihi ambazo zinaweza kuathiri ujumbe katika mawasiliano.

Aidha, mawasiliano yasiyo ya maneno huwa na kanuni tofauti. Kanuni hizo zinajumuisha alama zisizo na maneno kama vile mienendo ya mwili na lugha uso, mwonekano wa mwili, vipengele vya lugha ya sauti, na lugha ya vitu (Pearson na wenzake, whj).

Mienendo ya mwili na lugha uso ni pamoja na mkao, ishara na mienendo mingine ya mwili. Aidha, mwonekano wa mwili unajumuisha jinsi mtu alivyo na mvuto wa kimwili, ambayo huathiri jinsi watu wanavyotutendea na jinsi tunavyofanikiwa kijamii. Vilevile, vipengele vya lugha ya sauti ni pamoja na sauti zisizo za maneno na sifa kama vile sauti ndogo kubwa, kasi na ubora. Mwisho, lugha ya vitu inahusu matumizi ya mavazi na vitu vingine kuashiria umri, jinsia, hadhi, tabaka la kiuchumi na uanachama wa kundi. Kwa hiyo, kwa kuchanganya kanuni hizi zote na kuzitumia ipasavyo, kunaweza kuboresha ufahamu wetu wa mawasiliano yasiyo ya maneno na kukuza uhusiano wetu na watu wengine katika jamii.

Licha ya maelezo faafu ya watafiti hawa, tafiti zao hazijaonesha namna ambavyo mawasiliano yasiyo ya maneno yanavyoweza kukuzwa na kuimarishwa. Hivyo basi, kutokana na hali hii, tulipata shauku ya kufanya utafiti ili tuchunguze uelewa wa walimu wa Kiswahili kuhusu stadi za mawasiliano yasiyo ya maneno.

Pili, tulikusudia kuchunguza namna ambavyo fasihi andishi inaweza kutumiwa katika ukuzaji wa mawasiliano yasiyo ya maneno kwa wanafunzi wa madarasa ya Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza nchini Rwanda. Aidha, ishara zilizokusudiwa ni zile zinazotumiwa na watu ambao hawana ulemavu katika mawasiliano.

### 2.6 Nafasi ya Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano

Fasihi ni sanaa muhimu katika kuwasilisha mawazo na ujumbe wa jamii (Lugano, 2021). Kwa hiyo, sehemu hii inajadili umuhimu wa ufundishaji wa fasihi andishi katika maendeleo ya stadi za mawasiliano kwa ujumla. Ufundishaji huu unaruhusu wanafunzi kujifunza jinsi ya kutumia lugha kwa ufasaha, kuwasilisha mawazo yao kwa ufanisi, na kuelewa muktadha wa kijamii,

kitamaduni, na kihistoria katika maandishi (Collie & Slater, 2012). Kupitia ufundishaji wa fasihi andishi, wanafunzi wanakuwa na uwezo wa kufanya uchambuzi wa kina wa maudhui, kuendeleza mbinu za kufikiri kwa ufasaha na kuimarisha uwezo wao wa kujieleza kwa njia inayoeleweka. Hivyo, ufundishaji wa fasihi andishi huwawezesha wanafunzi kushiriki katika majadiliano, kuwasilisha maoni yao kwa ufasaha na ujasiri na kuunda hoja zenye nguvu.

Aidha, ufundishaji wa fasihi andishi unaweza kuwa na athari kubwa katika maendeleo ya stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Ilankumaran & Deepa (2018) wanaonesha kuwa kupitia shughuli za uigizaji na na uchambuzi wa hadithi, wanafunzi hujenga ujasiri wa kujieleza na kuelewa mitazamo tofauti. Rao & Charyulu (2015) wanasisitiza kuwa ufundishaji wa fasihi unazingatia matumizi ya lugha kisanaa, ambayo inachangia katika kuendeleza stadi za lugha kwa wanafunzi. Kwa hiyo, ni lazima kuimarisha mbinu za ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari ili kuongeza ujasiri wa wanafunzi katika kujieleza, kuelewa mitazamo tofauti, na kutumia lugha kisanaa kwa ufanisi.

Patki (2013) anadokeza pia kwamba ufundishaji wa fasihi andishi unaongeza ufahamu wa hisia, maadili na tamaduni tofauti miongoni mwa wanafunzi. Kadhalika, fasihi andishi huchochea uwezo wao wa kihisia na kuboresha mawasiliano yao ya kimtandao. Zaidi ya hayo, Bisamaza (2022) anasema kwamba fasihi andishi inaweza kushiriki katika ukuzaji wa stadi kusikiliza na kuzungumza Kiswahili.

Licha ya maelezo ya Collie & Slater (2012), Patki (2013), Rao & Charyulu (2015) na Ilankumaran & Deepa (2018), tafiti zao zimezungumzia ufundishaji wa fasihi na ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiingereza ambayo ni tofauti na lugha ya Kiswahili. Vilevile, tafiti hizi zilifanyika katika nchi zinazotumia mitaala ya kielimu ambayo si sawa na mtaala wa kielimu unaotumiwa nchi Rwanda.

Isitoshe, utafiti wa Bisamaza (khj) unaonesha nafasi ya fasihi simulizi katika ukuzaji wa stadi ya kusikiliza na kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari ambazo pekee yake hazitoshi kwa mawasiliano fasaha kwa lugha hii. Hii ni kwasababu, mawasiliano fasha yanahitaji stadi nyingine kama vile kusoma, kuandika, ujasiri, utambuzi wa hisia na nyinginezo.

Mwisho, tafiti husika zilifanyika katika miaka ambayo ni tofauti na mwaka wa 2024 ambapo utafiti wetu ulifanyika. Hii inatoa mapengo katika uelewa wetu wa jinsi fasihi andishi inavyoathiri maendeleo ya stadi za mawasiliano katika mazingira ya sasa, na hivyo inahitaji tafiti mpya ili kutathmini athari za mabadiliko haya. Kutokana na hali hii tumeona katika mapitio ya maandiko, tulipata shauku ya kufanya utafiti ili kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika madarasa ya Kiswahili katika shule za sekondari teule zilizopo wilayani Nyanza nchini Rwanda.

**2.7 Hali ya Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Ujumla**

Stadi za mawasiliano kama kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika zina jukumu muhimu katika kubadilishana habari na mawazo darasani (Evertson, 2011). Mawasiliano yanaweza kufanyika kupitia njia mbalimbali, kama vile maneno na ishara, na yanahitaji ushirikiano kati ya walimu na wanafunzi ili yafanikishwe (Durga & Mehrotra, 2022). Katika ukuzaji wa stadi hizi, ni lazima kuzingatia vipengele vya mawasiliano kama stadi za lugha, ufahamu wa kijamii na utambuzi wa hisia (Muste, 2016). Walimu hutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji kama kuanzisha majukwaa ya mijadala, kutoa kazi za makundi na maoni yenye ujenzi kusaidia wanafunzi kuboresha stadi zao za mawasiliano (Tubbs, Moss & Mulyana, 2000).

Walimu huwa mifano kwa wanafunzi katika mawasiliano yao wenyewe, wakionesha jinsi ya kujieleza kwa ufasaha, kusikiliza kwa makini, na kufanya mazungumzo ya heshima (Muste, khj). Hata hivyo, bado kuna changamoto katika ufundishaji wa stadi za mawasiliano.

Mafanikio ya kukuza stadi hizi kati ya wanafunzi hayajafikia kiwango kinachotarajiwa, na hivyo kuathiri uwezo wao wa kujumuishwa katika jamii na soko la ajira (Ngọc, 2021*)*. Hitaji la maboresho katika mbinu za ufundishaji ni muhimu ili stadi za mawasiliano zipewe mkazo vizuri katika mfumo wa elimu (Standard Digital, 2019).

Kuendelea kuboresha mbinu za ufundishaji na kuzingatia uwezo wa kutuma na kupokea ujumbe kwa ufanisi ni muhimu ili wanafunzi waweze kueleza mawazo yao kwa ufanisi na kushirikiana vizuri na wengine (Henderson & Mathew-Byrne, 2016). Maelezo haya yanathibitisha kuwa kuna haja ya maboresho makubwa katika mbinu za ufundishaji wa lugha ili kuhakikisha kwamba stadi za mawasiliano zinatiliwa mkazo kwa kukuzwa vizuri katika mfumo wa elimu.

Kwa hiyo, kutokana na haya tuliyoyaona kwenye mapitio ya maandiko, tulipata shauku ya kufanya utafiti ili kuona namna gani walimu wa fasihi andishi ya Kiswahili wanavyotumia au wanavyopaswa kutumia ufundishaji wa fasihi ili kuhakikisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi.

## 2.8 Hali ya Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano katika Lugha ya Kiswahili

Kiswahili, kama lugha ya Kibantu na Kiafrika yenye watumiaji wengi, inaonesha kuongezeka kwa umuhimu wa stadi za mawasiliano katika maeneo mbalimbali. Taasisi za elimu zimeanza kulenga zaidi ukuzaji wa stadi hizi kupitia mafunzo ya lugha ya Kiswahili, semina na rasilimali mtandaoni (Pastory, 2016; Tibategeza & Plessis, 2018; Chepkemoi & Wanyonyi, 2017). Hii inaashiria mwamko unaokua kuhusu umuhimu wa kuwasiliana kwa ufanisi, kufanya na kushiriki katika mawasiliano ya umma katika Kiswahili. Pamoja na taasisi za elimu, makampuni na vikundi vya kujitolea vimechukua hatua ya kutoa mafunzo katika Kiswahili. Lengo ni kuimarisha stadi za mawasiliano miongoni mwa wafanyakazi na jamii kwa ujumla (Mwakagele, 2016; Lang’at, 2020). Hii inaonesha mwelekeo mzuri wa ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili ambayo inazidi kuenea na kutambuliwa kimataifa.

Kuongezeka kwa matumizi ya Kiswahili kimataifa kumeleta mahitaji ya kuimarisha stadi za mawasiliano kwa lugha hii. Kiswahili sasa ni lugha inayotambulika kimataifa kibiashara, kidiplomasia, na katika vyombo vya habari (Pastory, 2016). Sridhar (2012) anasisitiza kuwa stadi za mawasiliano katika Kiswahili zinawezesha watu kujitayarisha vyema katika mazingira ya kimataifa na kuongeza uwezo wao wa kuzungumza, kuandika, na kufanya kazi kwa ufanisi katika lugha hii inayokua kwa kasi.

Hata hivyo, kuna changamoto katika ufundishaji wa Kiswahili ambapo mkazo mkubwa unawekwa katika kusoma na kuandika kuliko stadi nyingine muhimu kama vile kusikiliza kwa makini, kuzungumza kwa ufasaha, kufahamu hisia, ujasiri na matumizi ya ishara katika mawasiliano (Khakasa, 2018). Hii inaweza kuleta pengo katika maendeleo ya stadi za mawasiliano, ambazo ni muhimu katika mahusiano ya kibinafsi na kitaaluma (Otieno, Inyani & Shikuku, 2020).

Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha mbinu za ufundishaji ili kuhakikisha stadi zote za mawasiliano zinapewa umuhimu sawa katika mchakato wa kufundisha na kujifunza Kiswahili. Hii itachangia kuandaa vizazi vyenye ujuzi kamili wa mawasiliano.

Ingawa maelezo yaliyopo yanatoa taswira ya hali ya ufundishaji wa stadi za mawasiliano katika Kiswahili katika nchi kama Tanzania, Kenya, na Uganda, bado tuliona kwamba kuna pengo kuhusu hali ya ufundishaji wa stadi za mwawasiliano katika Kiswahili kwenye shule za sekondari nchini Rwanda.

Hivyo, kutokana na hali hii, tulipata shauku ya kufanya utafiti wetu ili kujaza pengo hili kwa kuchunguza jinsi stadi za mawasiliano zinavyoweza kukuzwa kupitia ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyanza, Rwanda. Hivyo, utafiti uliofanyika ulikusudia kutoa mwanga kuhusu hali halisi ya ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika Kiswahili nchini Rwanda na njia za kuboresha ufundishaji katika muktadha huo.

### 2.9 Mikakati ya Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano kupitia Ufundishaji wa Fasihi Andishi

Lengo mahususi la pili katika utafiti uliofanyika lilikuwa kuunda miongozo wa kutumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi ya mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani NyanzaKwa hiyo, ili kutimiza lengo husika, ilikuwa bora kupitia maandiko tofauti kuhusu mikakati ya kutumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi ya mawasiliano kwa ujumla. Kulingana na Paul & Reem (2004), hitaji la wahitimu wa elimu wenye uwezo wa kufikiri kwa uangalifu na kuwasiliana kwa ufasaha linazidi kuongezeka. Kwa hiyo, ni lazima walimu watumie mbinu fasaha katika ufundishaji wa stadi za mawasiliano. Licha ya wingi wa mikakati ya ukuzaji wa stadi za mawasiliano, katika utafiti uliofanyika, tulijikita katika mikakati mitatu kama ilivyoelezwa na Rosalyn (2020).

#### 2.9.1 Mawasiliano ya Mtu Moja kwa Mwingine

Kwa mujibu wa Rosalyn (khj), mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine ni mbinu ya ukuzaji wa stadi za mawasiliano ambapo mtu hufundishwa kuwasiliana akiwa pamoja na mtu mwingine mmoja. Hii ni mbinu hii imebainishwa kuwa muhimu katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa wanafunzi. Hii inatokana na kwamba mbinu hii inajenga mahusiano na uelewa kati ya watu kwa njia bora zaidi.

Kwa mujibu wa Cuc (2014), kufanya mazungumzo ya karibu kunaruhusu kuelewa kwa kina Zaidi na maendeleo ya stadi za mawasiliano kwa kutazama lugha ya mwili, njia wawasilianaji wanazopendelea kufanya mawasiliano na ishara za kuonekana. Hii husaidia kujifunza jinsi ya kufanya mawasiliano kwa ufanisi. Uwezo wa mawasiliano ya mtu mmoja kwa mtu mwingine husaidia kujenga uhusiano wa imani na uwazi (Garside & Kleiner, 1991). Huu ni mkakati muhimu kwa walimu kukuza stadi za mawasiliano kwa wanafunzi wao. Kwa kujenga mazingira ya faragha, wanafunzi wanapata ujasiri wa kufichua hisia zao, matatizo na ndoto zao bila hofu ya kuhukumiwa hadharani. Mazungumzo ya mtu mmoja na mwingine huwapa wanafunzi nafasi ya kujisikia kuheshimiwa na kueleweka, kuchochea ukuaji wao wa kielimu na kibinafsi (Rosalyn, khj). Mkakati huu wa mawasiliano ya mtu mmoja kwa mtu mwingine unajenga uhusiano wa karibu baina ya wanafunzi, kuwafanya wahisi wanathaminiwa na kuongeza ufanisi wa kujifunza kwa kuzingatia mahitaji yao ya kipekee.

Katika matumizi ya fasihi andishi, mbinu ya mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine ina manufaa makubwa katika kuunda mazingira ya faragha ambapo wanafunzi wanajisikia huru kujieleza (Charyulu, 2015). Kwa kutumia mazungumzo ya karibu, walimu wanaweza kufanikisha uchambuzi wa kina wa maandiko, hali inayoimarisha uelewa wa wanafunzi kuhusu dhamira na maana ya waandishi wa fasihi andishi (Cuc, 2014). Aidha, mbinu hii inachangia katika kuimarisha uhusiano wa kitaaluma kati ya mwalimu na mwanafunzi, hivyo kukuza mazingira yenye ushirikiano na kujenga ujasiri wa wanafunzi katika kutoa mawazo yao.

Mbinu ya mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine inachangia katika maendeleo ya stadi za mawasiliano kwa kutoa fursa kwa wanafunzi kujifunza mbinu bora za kujieleza na kuelewa mitindo mbalimbali ya mawasiliano, ikiwemo lugha ya mwili na ishara za kuonekana (Charyulu, khj). Hii inasaidia wanafunzi kuwa na ufanisi katika mawasiliano yao.

Hata hivyo, kutekeleza mbinu hii katika masomo ya fasihi andishi kunahitaji maandalizi maalum (Charyulu, khj). Hii ina maana kwamba walimu wanapaswa kuandaa maswali na majadiliano yanayowezesha uchambuzi wa kina wa maandiko, na kuhakikisha wanafunzi wanapata nafasi ya kutoa maoni yao na kujifunza kutoka kwa wenzake.

Ingawa Cuc (khj), Charyulu (khj), Garside & Kleiner (whj) na Rosalyn (khj) wameonesha umuhimu wa mbinu ya mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine kwa maendeleo ya stadi za

mawasiliano, hawakutoa mwongozo wa hatua za utekelezaji kwa walimu. Kwa hiyo, utafiti wetu ulifanyika kwa kusudi la kudhihirisha hatua kwa hatua namna ambavyo walimu wa fasihi andishi wanaweza kutumia mbinu husika katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

**2.9.2 Uumbaji wa Mazingira Salama ya Kujifunzia na Uhusiano Wenye Msaada**

Ilidhihirika kwamba uumbaji wa mazingira salama ya kujifunza pamoja na uhusiano wenye msaada kati ya walimu na wanafunzi una athari chanya katika ushiriki darasani, na utendaji wa kitaaluma wa wanafunzi (Rosalyn, 2020). Ilioneshwa kwamba bila uhusiano wenye msaada kati ya wanafunzi na walimu, ni vigumu kwaokufikia malengo ya kufundisha na kujifunza. Hivyo basi, ili kuboresha stadi za mawasiliano kati ya wanafunzi, walimu wanapaswa kuunda mazingira salama ya kujifunza ambayo yanazingatia uhusiano wenye msaada.

O'Connor & McCartney (2007) wanasema kwamba wanafunzi wanapojifunza katika mazingira ambayo uhusiano wenye msaada umetiliwa mkazo, wanajisikia vizuri zaidi kuwasilisha mawazo yao na fikra katika mijadala darasani, majadiliano, kujibu maswali na kuomba ufafanuzi wanapohitaji msaada. Hii inaweza kuwa na manufaa katika kuboresha stadi za mawasiliano na kushiriki katika kuepukana na changamoto zinazowakabili walimu katika mchakato wa kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Hii ni kwa sababu wanafunzi wanaposhiriki kikamilifu katika shughuli za kufundisha na kujifunza, wanajenga uwezo wao na ustadi wao wa kitaaluma. Hii inaonesha kwamba uumbaji wa mazingira salama ya kujifunza pamoja na uhusiano wenye msaada ni muhimu katika kuboresha stadi za mawasiliano kati ya wanafunzi.

Katika matumizi ya fasihi andishi, uumbaji wa mazingira salama ya kujifunzia na uhusiano wenye msaada una athari kubwa katikae ushiriki darasani, na utendaji wa kitaaluma wa wanafunzi (Rosalyn, khj). Mazingira salama yanayohakikisha uhusiano wenye msaada kati ya walimu na wanafunzi ni muhimu kwa kutoa fursa kwa wanafunzi kujieleza na kuchunguza maandiko kwa kina bila hofu ya kuhukumiwa.

Hii inasaidia katika kukuza uelewa wa kina wa maandiko na stadi za mawasiliano (O'Connor & McCartney, whj). Kwa mfano, katika masomo ya fasihi andishi, mbinu hii inaruhusu wanafunzi kuwasilisha mawazo yao kuhusu dhana za fasihi, kutoa maoni, na kujadili kwa uwazi katika mazingira yasiyo na mashaka.

Zaidi ya hayo, mbinu ya mazingira salama ya kujifunzia inachangia katika kuboresha ushiriki wa wanafunzi katika majadiliano ya fasihi kwa kupunguza vikwazo vya kisaikolojia na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanahisi thamani katika michango yao (Smith & Johnson, 2010). Uhusiano wenye msaada unawasaidia wanafunzi kuelewa maandiko kwa undani na kuwa na uwezo wa kueleza mawazo yao kwa uhuru. Hali husaidia wanafunzi kuboresha stadi zao za mawasiliano na kupunguza changamoto zinazowakabili walimu katika kufundisha fasihi andishi (Williams & Lee, 2019). Hii inaonesha kuwa mbinu hii ya mazingira salama ya kujifunzia na uhusiano wenye msaada inachangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza ufanisi wa ufundishaji wa fasihi andishi na maendeleo ya stadi za mawasiliano kati ya wanafunzi.

Licha ya hayo, tafiti za O'Connor & McCartney (khj) na Rosalyn (khj) zina pengo katika ufafanuzi wa jinsi walimu wanavyopaswa kuboresha stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Vilevile, tafiti hizi hazizingatii lugha mahususi katika kuelezea stadi za mawasiliano, hasa kwa lugha za Kibantu kama Kiswahili. Hivyo, kutokana na hali hii, tulipata shauku ya kufanya utafiti ili kujaza pengo hilo kwa kubainisha namna uumbaji wa mazingira salama ya kujifunza unavyoweza kusaidia kukuza stadi za mawasiliano ya Kiswahili kwa wanafunzi wa madarasa ya Kiswahili katika Wilaya ya Nyanza, Rwanda

### 2.9.3 Utumiaji wa Mbinu ya Kusikiliza kwa Makini

Umuhimu wa kusikiliza kwa makini ni msingi wa mawasiliano yenye ufanisi na uelewa wa kweli. Kulingana na utafiti wa Curuso, Colombi, na Tebbit (2017), zaidi ya asilimia 60 ya matatizo ya kutoelewana katika mawasiliano yanatokana na usikilizaji duni. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuendeleza stadi hii kwa wanafunzi. Walimu wanahimizwa kutoa mazoezi yanayoendeleza uwezo wa kusikiliza kwa makini kwa wanafunzi, kama vile kuhakikisha wanazingatia maelezo, kuelewa vizuri, kurudia, na kujenga mawazo yao. Kupitia njia hizi, wanafunzi hupata uwezo wa kusikiliza kwa ufasaha, huku wakiboresha stadi zao za mawasiliano kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Curuso na wenzake (whj), mkakati wa utumiaji wa usikilizaji kwa makini unasaidia katika ukuaji wa stadi za mawasiliano na unachangia katika kuimarisha uelewa wa wanafunzi darasani. Kwa kuzingatia kwa uangalifu kile kinachosemwa na wengine, wanafunzi hujenga uwezo wa kuelewa dhana na maoni tofauti, huku wakijenga uelewa imara wa mada

zinazojadiliwa. Katika muktadha wa fasihi andishi, mbinu hii ni muhimu zaidi kwa kusaidia wanafunzi kuelewa maandiko kwa kina. Wanafunzi wanapokuwa na uwezo wa kusikiliza kwa makini, wanachambua na kuelewa vipande vya fasihi kwa ufanisi zaidi, jambo linalowezesha majadiliano mazuri na uchambuzi wa kina wa maandiko.

Kwa kuweka mkazo katika kufuatilia maelezo, kurudia kwa umakini na kujenga mawazo kulingana na kile kilichosemwa, wanafunzi wanaweza kuongeza uwezekano wao wa kufanya mawasiliano yenye tija na ya kina. Jambo hili linaweza kuwasaidia kuwa na uelewa mzuri wa hoja zilizowasilishwa.

Hii inajidhihirisha kwa wanafunzi wa fasihi andishi, ambapo kusikiliza kwa makini kunawawezesha kuelewa mbinu za uandishi, mitindo ya wahusika, na dhamira ya waandishi, hali inayosaidia katika kuboresha stadi za mawasiliano na uchambuzi wa maandiko (Rosalyn, 2020).

Hivyo basi, kuzingatia na kukuza uwezo kusikiliza kwa makini miongoni mwa wanafunzi ni muhimu katika kuendeleza stadi zao za mawasiliano na kujenga uelewa imara. Kulingana na Rosalyn (2020), walimu wanalo jukumu kubwa la kukuza stadi ya kusikiliza kwa makini kwa kuwapa wanafunzi mazoezi yanayowawezesha kusikiliza kwa umakini na kuelewa kwa undani maelezo wanayopewa.

Katika masomo ya fasihi andishi, mbinu hii ni muhimu kwa kuwa inasaidia wanafunzi kuelewa na kuchambua maandiko kwa kina, hivyo kuboresha mawasiliano na kutoa mchango wenye tija katika majadiliano ya darasani.

Curuso na wenzake (whj) wanasisitiza kwamba mkakati wa utumiaji wa usikilizaji kwa makini ni mojawapo ya mikakati ya ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa wanafunzi. Hata hivyo, hawakuonesha jinsi mkakati huu unavyoweza kutumiwa na walimu wa fasihi andishi katika kuendeleza stadi za mawasiliano kwa lugha mahususi miongoni mwa wanafunzi wa kiwango cha elimu mahususi.

Kutokana na hali hii, tulipata shauku ya kufanya utafiti ili kutoa miongozo mwafaka ya jinsi walimu wa fasihi andishi ya Kiswahili wanavyopaswa kutumia mkakati wa usikilizaji kwa makini ili kukuza stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari teule katika Wilaya ya Nyanza nchini Rwanda.

### 2.10 Mapengo ya Tafiti Tangulizi

Tafiti zilizofanywa na Valente (2016), Azimova (2020) na Friston, Sajid, Quiroga, Parr, Price & Holmes (2021) zinaonesha mwamba stadi za mawasiliano ni stadi muhimu ambazo wahitimu wa shule za sekondari ikiwemo wa michepuo ya lugha wanazopaswa kuwa nazo. Watafiti hawa wanajadili stadi hizi katika lugha ya Kiingereza ambayo ni tofauti na lugha ya Kiswahili. Tena, watafiti hawa hawaoneshi namna ambavyo stadi husika zinaweza kukuzwa miongoni mwa wanafunzi.

Aidha, tafiti zilizotangulia zinajadili aina za stadi za mawasiliano ya mwanadamu kama vile kusikiliza kwa makini, ujasiri na utambuzi wa hisia. Licha ya maelezo yanayotolewa na tafiti hizi, bado zina mapengo kwa kuwa zinaongelea aina za mawasiliano ya mwanadamu kwa ujumla bila kuhusisha lugha mahususi. Vilevile, tafiti hizi hazishughulikii namna ambavyo kila aina ya mawasiliano inavyoweza kukuzwa miongoni mwa wanafunzi wa kiwango fulani cha elimu.

Vilevile, Khakasa (2018) na Otieno, Inyani & Shikuku (2020) wanabainisha hali ya ufundishaji wa stadi za mawasiliano katika Kiswahili katika nchi kama vile Kenya Uganda, Kenya na Tanzania. Watafiti hawa hawakugusia hali ilivyo nchini Rwanda ambapo Kiswahili hufundishwa kama lugha ya pili.

Zaidi ya hayo, Collie & Slater (2012), Patki (2013), Rao & Charyulu (2015) na Ilankumaran & Deepa (2018) wanaonesha nafasi ya ufundishaj wa fasihi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano. Watafiti hawa walijikita katika stadi za kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza ambayo ni tofauti na lugha ya Kiswahili.

Isitoshe, utafiti wa Bisamaza (2022), ulishughulikia nafasi ya fasihi simulizi katika ufundishaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyagatare pasipo kugusia stadi nyingine faafu katika mawasiliano ambazo ni kusoma, kuandika, utambuzi wa hisia na ujasiri na stadi za mawasiliano yasiyo ya maneno. Mwisho, kadiri ya uelewa wetu, hakuna utafiti wowote uliochapishwa kuhusu nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa wanafunzi wa michepuo ya lugha nchini Rwanda.

Hivyo basi, utafiti uliofanyika ulikusudia kuyaziba mapengo haya kwa kubainisha nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani

Nyanza nchini Rwanda. Vilevile, utafiti wetu ulikusudia kutoa miongozo ya jinsi ya kutumia fasihi andishi kwa lengo la kukuza stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyanza.

### 2.11 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti uliofanyika uliongozwa na Nadharia ya Mawasiliano ambayo iliasisiwa na S. F. Scudder mwaka 1980. Kulingana na Scudder (1980), msingi wa maisha ni mawasiliano. Kwa hiyo mawasiliano ni lazima yatiliwe mkazo ili kurahisisha shughuli mbalimbali maishani. Nadharia hii inaelezea kuwa binadamu wanawasiliana ili kubadilishana mawazo na hisia, kufikisha ujumbe kwa wengine na kueleza hisia zao. Kwa hivyo, kulingana na Scudder (khj), mawasiliano ni muhimu katika maisha ya binadamu. Nadharia ya Mawasiliano inasisitiza kwamba binadamu hutumia sauti, ishara na aina mbalimbali za vitendo kuelezea mahitaji yao ya chakula, huduma za afya au wanapojihisi vibaya.

Robbins & Judge (2007) wanasema kwamba bila kulia, mama hangeweza kugundua kwamba mtoto ana njaa. Kwa hiyo, Nadharia ya Mawasiliano inathibitisha kwamba iwe binadamu wanapenda au hawapendi, wanajikuta wakihitaji kuwasiliana na wengine. Aidha, Robbins & Judge (whj) wanasema kuwa Nadharia ya Mawasiliano imejengwa juu ya mihimili mikuu mitatu. Mhimili wa kwanza umejengwa kwa wazo la kwamba mawasiliano ni mchakato wa kiufundi wa kuhamisha mawazo, ujumbe na hisia kutoka kwa mtu mmoja mmoja kwenda kwa mwingine. Mhimili wa pili unasema kuwa mawasiliano ni mchakato wa kusambaza habari kutoka kwa mwasilishi wa ujumbe kwenda kwa mpokeaji ambaye kisha huifafanua na kuchukua hatua kulingana na ujumbe alioupokea. Mhimili wa tatu unasisitiza kwamba mawasiliano yanachukuliwa kama mchakato wa kuunda na kubadilisha ujumbe mpya kila wakati watu wanapotafsiri ujumbe kwa njia zao na kufikia hitimisho lao wenyewe.

Tulipanga kutumia nadharia hii ili kutathmini jinsi fasihi andishi inavyoweza kuwa chombo muhimu cha kuhamisha ujumbe, mawazo, na hisia kati ya wanafunzi na walimu. Kwa kutumia mhimili wa kwanza wa nadharia hii, tulitarajia kuchunguza jinsi fasihi andishi inavyotumika kama njia ya kiufundi ya kuwasilisha mawazo na ujumbe kutoka kwa mwandishi kwenda kwa wasomaji (wanafunzi).

Pili, mhimili wa pili wa nadharia hii ulitarajiwa kutumika ili kuchunguza jinsi wanafunzi wanavyopokea, kufasili na kuchukua hatua kulingana na ujumbe uliomo kwenye maandiko ya fasihi. Tulipanga kutumia mhimili huu ili kutathmini ufanisi wa fasihi andishi katika kukuza uwezo wa wanafunzi kufasili na kuwasilisha mawazo kwa ufasaha, huku tukizingatia changamoto zinazoweza kusababisha kutoeleweka kwa ujumbe.

Tatu, mhimili wa tatu wa nadharia hii ulitarajiwa kuwezesha utafiti wetu kuangazia namna wanafunzi wanavyotumia fasihi andishi kuunda na kubadilisha ujumbe wao wenyewe. Tlitarajia kubaini jinsi wanafunzi wanavyotumia ujuzi walioupata kupitia fasihi andishi ili kuboresha stadi zao za mawasiliano na jinsi wanavyotafsiri na kuwasilisha mawazo kwa njia mpya. Kwa hiyo, nadharia hii ilichaguliwa ili ituungoze kuunda miongozo ya kutumia fasihi andishi kama chombo cha kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

**2.12 Muhtasari wa Sura ya Pili**

Sura ya pili inatoa taarifa kuhusu fasihi andishi na ukuzaji wa stadi za mawasiliano. Kwa hiyo, sura husika inagawanyika katika sehemu ndogo ndogo. Sehemu hizo ni pamoja na mapitio ya maandiko kulingana na malengo mahususi ya utafiti, mapengo ya tafiti tangulizi, kiunzi cha nadharia na muhtasari wa sura husika.  Sehemu inayofuata ni methodolojia ya utafiti.

# SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura ya tatu inajihusisha na methodolojia ya utafiti. Kothari (2012) anaielezea methodolojia ya utafiti kama mwongozo unaosaidia mtafiti kupata ufumbuzi wa masuala katika utafiti wake pamoja na hatua zinazopaswa kufuatwa. Sura hii inagawanyika katika sehemu tofauti ambazo ni: utangulizi, paradima, usanifu, eneo, wango, sampuli ya utafiti, mbinu za ukusanyaji data, vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data, itikeli, uhalali na uthabiti wa utafiti na muhtasari wa sura ya tatu.

## 3.2 Paradima ya Utafiti

Paradima ya utafiti ni mfumo wa mawazo, imani na mtazamo ambao unaongoza mtafiti katika kufafanua, kuelewa na kuchambua matatizo ya utafiti (Terrell, 2022). Huu ni mfumo muhimu ambao unaweka msingi wa kufanya utafiti na kutoa mwongozo wa jinsi ya kukusanya, kuchambua na kueleza data. Kulingana na Terrell (khj), paradima huathiri jinsi mtafiti anavyotazama ulimwengu, anavyoelewa uhusiano kati ya mambo na njia anazotumia katika utafiti wake. Terrell (khj) anaongezea kuwa, kutegemeana na paradima ya utafiti, watafiti huweza kuona jambo moja kwa namna tofauti. Paradima ya utafiti hutegemeana na malengo ya utafiti.

Kulingana na malengo ya utafiti, paradima ya kiufasiri ilitumiwa. Kwa mujibu wa Smith & Johnson (2010), paradima ya kiufasiri ni mtazamo wa utafiti unaogusa jinsi watu wanavyoelewa na kufafanua ulimwengu wao. Katika mtindo huu, kuna mkazo wa kipekee katika uelewa wa kina wa maana na muktadha wa mambo kwa kuchunguza uhusiano kati ya watu na mazingira yao. Hii inasisitiza kwamba ukweli unaweza kuwa tofauti kulingana na mtazamo wa mtu au jamii. Katika muktadha wa utafiti, paradima hii inazingatia uzoefu wa washiriki ili kupata uelewa wa kina wa maana na muktadha wa matukio.

Hivyo, utafiti wetu ulijiegemeza kwenye paradima ya kiufasiri kwa namna ifuatavyo: Kutokana na kuwa paradima hii inaamini kuwa hakuna ukweli mmoja, kila taarifa zilizotolewa na washiriki wa utafiti zilizingatiwa na kulinganishwa ili kupata majibu ya maswali ya utafiti. Pia, mtafiti hakujiegemeza tu kwenye taarifa kutoka kwa washiriki wa utafiti, bali, mtafiti alilazimika kwenda uwandani ili kushuhudia ukweli wa mambo halisi.

Pili, mtafiti alitumia washiriki wa utafiti ambao wako katika mazingira na muktadha ambapo fasihi andishi ya Kiswahili hufundishwa na mawasiliano katika lugha ya Kiswahili hufanyika. Hii ni kwa sababu paradima husika huonesha kuwa, muktadha na mazingira ni mambo ambayo yanaweza kuathiri uelewa wa mambo miongoni mwa watu.

Mwisho, watu walioshirikishwa katika utafiti ni wale tu ambao wana uzoefu katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi andishi ya Kiswahili na kuwasiliana katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu, paradima ya kiufasiri inaonesha kuwa uzoefu wa washiriki wa utafiti ni muhimu sana ili kupata data za kuaminika kuhusu swala linalofanyiwa utafiti

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Sehemu ya usanifu wa utafiti katika sura ya methodolojia ya utafiti inaelezea njia za kufanya utafiti na hutofautiana sana kulingana na aina fulani ya uchunguzi. Unakua na sehemu tofauti ambazo zinaelezea eneo la utafiti, sampuli, washiriki, vyanzo vya data, vifaa vya ukusanyaji wa data na mbinu za uchambuzi wa data (Lukenchuk, 2023). Aidha, kulingana na Ordho & Combo (2003), usanifu wa utafiti ni muhimu sana katika kurahisisha maendeleo ya kazi ya utafiti kwa kuwezesha ukusanyaji fasaha wa data muhimu na kupunguza gharama na muda wa kukusanya. Kwa hiyo, utafiti tuliofanya ulikuwa wa kitaamuli. Kwa mujibu wa Maxwell (2015), mkabala wa kitaamuli hutegemea zaidi maelezo, maoni na uelewa wa washiriki wa utafiti kuhusu mada swala fulani.

Hivyo basi, katika utafiti uliofanyika, mtafiti alizikusanya data za kitaamuli ambazo ziliwasilishwa na kuchambuliwa kwa madondoo na maelezo. Utafiti wa kitaamuli ulichaguliwa kwa kuwa ulitarajiwa kuwezesha mtafiti kusaka na kupata taarifa za kutosha na kuaminika kuhusu ukuzaji wa stadi za mawasiliano kupitia ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyanza nchini Rwanda.

## 3.4 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti linabainisha mahali ambapo kazi ya utafiti itafanyika ili kukusanya data za msingi au za upili ambazo zinamwezesha mtafiti kutimiza malengo ya utafiti (Kothari, 2012). Kwa hiyo, kijiografia, utafiti wetu ulifanyika katika wilaya ya Nyanza.

Kwanza, wilaya hii haipakani na nchi yoyote inayotumia Kiswahili, na haina masoko makubwa yanayoweza kuvutia wafanyabiashara wa kimataifa wakiwemo watumiaji wa Kiswahili. Hii ina maana kwamba wilaya ya Nyanza haina idadi kubwa ya watumiaji wa Kiswahili.  Pili, wilaya hii inachukuliwa kama kama kitovu cha utamaduni wa Rwanda (Bizimana, 2022), wakazi wake wana mwelekeo mkubwa wa kutumia Kinyarwanda kulinda urithi wao. Matokeo yake ni kwamba, mawasiliano kwa lugha nyingine zinazotumiwa nchini Rwanda ikiwemo Kiswahili katika wilaya hii ni machache ikilinganishwa na baadhi ya maeneo mengine nchini Rwanda.

Zaidi ya hayo, shule zilizochaguliwa ni shule ambazo zina mchepuo wa lugha ambamo fasihi andishi ya Kiswahili hufundishwa. Shule hizi zilichaguliwa kimakusudi kwa kuwa ndizo zenye walimu na wanafunzi wenye taarifa muhimu kuhusu nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano.

### 3.5 Wango na Sampuli ya Utafiti

Sehemu hii inazingatia vipengele viwili ambavyo ni wango pamoja na sampuli ya utafiti. Kwa hiyo, kila kipengele kimeelezwa hapo chini.

#### 3.5.1 Wango la Utafiti

Kwa mujibu wa Cresswell (2012), wango la utafiti ni kundi la vitu au watu wenye sifa sawa. Vilevile, wango la utafiti ni kundi la watu au vitu ambamo sampuli huchaguliwa (Kombo & Tromp, 2006). Wango la utafiti lilikuwa walimu wa Kiswahili na wanafunzi wanaojifunza katika kidato cha nne hadi cha sita katika mchepuo wa LFK (Literature in English, French, Kinyarwanda na Kiswahili) katika shule za sekondari za Wilaya ya Nyanza.

Hivyo basi, utafiti ulifanyika katika wilaya husika ili kutoa mwanga kwa walimu kuhusu jinsi wanavyoweza kukuza stadi za mawasiliano kwa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi katika mazingira yao kupitia ufundishaji wa fasihi andishi.

#### 3.5.2 Sampuli ya Utafiti

Creswell & Creswell (2018) wanasema kwamba, sampuli ya utafiti ni kikundi kidogo cha watu, vipengele au vitu ambavyo vinachaguliwa kutoka kwenye idadi kubwa zaidi ili kuwakilisha kwa usahihi kile kinachochunguzwa katika utafiti.

Vilevile Creswell & Creswell (whj) wanasema kwamba, usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi kidogo kutoka kwenye jumla ili kuwakilisha kwa usahihi kile kinachochunguzwa katika utafiti ili kupata data inayoweza kutoa picha halisi bila kuhusisha kila kipengele cha jumla hiyo. Kwa hiyo, mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumiwa ili kuteua sampuli ya utafiti.

Frankel & Warren (2006) wanadai kwamba, usampulishaji lengwa ni mbinu ya usampulishaji ambapo mtafiti anachagua sampuli kulingana na sifa au vigezo maalum vinavyohusiana na lengo la utafiti, ikilenga kupata ufahamu wa kina kuhusu suala linalochunguzwa. Mbinu hii inaruhusu mtafiti kuteua watu au vipengele ambavyo vinaweza kutoa taarifa faafu na maalum zinazohusiana na muktadha wa utafiti (Frankel & Warren, whj).

Hii ina maana kwamba, usampulishaji lengwa ni njia ya usampulishaji ambapo mtafiti anaweza kuteua sampuli kulingana na vigezo maalum vinavyohusiana na malengo ya utafiti, lengo likiwa kupata uelewa wa kina kuhusu suala linalofanyiwa uchunguzi. Mbinu hii ya usampulishaji ilichaguliwa kwa kuwa ilifaa katika kuteua washiriki wa utafiti wenye taarifa za kutosha ambazo zilikuwa faafu katika utimizaji wa malengo mahususi ya utafiti wetu.

Hivyo basi, sampuli ya utafiti ilikuwa walimu wa Kiswahili 9 na wanafunzi 93 walioteuliwa kwenye CXR Nyanza, E.S. Nyanza na G.S. Kigoma. Shule hizi zilichaguliwa kwa makusudi kwa kuwa ndizo tu ambazo zina wanafunzi wanaojifunza katika mchepuo wa LFK ambapo fasihi andishi ya Kiswahili hufundishwa. Kuhusiana na sampuli ya wanafunzi, mtafiti aliteua wanafunzi wote wa kidato cha sita katika kila shule. Kwa hiyo, sampuli ya wanafunzi ilihusisha wanafunzi 30 kutoka kwenye CXR Nyanza, wanafunzi 25 kutoka kwenye E.S. Nyanza na wanafunzi 38 kutoka kwenye G.S. Kigoma. Wanafunzi hawa walishiriki katika utafiti wetu kwa kuwa ushuhudiaji ulifanyiwa kwenye madarasa ambamo wanafunzi hawa wanajifunza. Wanafunzi wa kidato cha sita walichaguliwa kwa makusudi kwa sababu ndio ambao wanajifunza fasihi andishi kwa kina zaidi ikilinganishwa na wanafunzi wa kidato cha nne na cha tano katika mchepuo wa LFK.

Aidha, kwa upande wa walimu, sampuli ya utafiti ilihusisha walimu wa Kiswahili 9. Kwa kuwa kila shule huwa na mwalimu mmoja wa Kiswahili, kwa lengo la kuongeza walimu walioshiriki

katika mahojiano, mtafiti aliongeza walimu wengine 6. Walimu hawa wanafundisha Kiswahili katika shule zinazokaribiana na shule tatu ambamo utafiti wetu ulifanyika.

Ingawaje walimu hawa wa ziada hawafundishi katika michepuo ya lugha, walitoa taarifa za kuaminika kuhusu nafasi ya fasihi andishi na ufundishaji wa stadi za mawasiliano kwa sababu walipata elimu kuhusu fasihi andishi katika ngazi ya shule za sekondari na vyuo.

### 3.6 Mbinu za Kukusanyia Data

Mbinu za kukusanyia data ni taratibu za mfumo zinazotumika kukusanya taarifa maalum kwa ajili ya utafiti au uchambuzi (Frechtling, 2002). Mbinu hizi zinajumuisha njia mbalimbali au zana zinazotumiwa na watafiti kukusanya, kurekodi na kupata data zinayofaa kwa malengo yao ya utafiti.

Kwa hiyo, katika utafiti uliofanyika, mbinu za kukusanyia data zilizotumiwa ni uchambuzi wa matini, usaili na ushuhudiaji. Mbinu zilikamilishana ili kukusanya data muhimu kuhusu ukuzaji wa stadi za mawasiliano kupitia ufundishaji wa fasihi andishi.

#### 3.6.1 Uchambuzi wa Matini

Uchambuzi wa matini ni mbinu ya utafiti inayohusisha uchunguzi wa nyaraka, maandishi au vifaa vingine vya maandishi kwa lengo la kuelewa, kufafanua au kupata ufahamu zaidi kuhusu masuala yanayochunguzwa katika utafiti (Bowen, 2009). Katika utafiti uliofanyika, mbinu ya uchambuzi wa matini ilitumika kwa kuwa mtafiti alizisoma nyaraka. Kwanza, mtafiti alichambua nyaraka za kitaaluma kuhusu nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano pamoja na miongozo ya kukuza stadi hizo kupitia ufundishaji wa fasihi andishi.

Pili, mtafiti alichambua nyaraka za kielimu za walimu, zikiwemo mandalio ya masomo na tathmini. Nyaraka hizi zilichambuliwa ili kuchunguza namna walimu wanavyojumuisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika maandalizi ya masomo, ufundishaji na tathmini. Zaidi ya hayo, mtafiti alichambua tamthilia *Nguzo Mama* ya Penina Muhando ili kubaini jinsi tamthilia hiyo inavyoweza kutumika kufundisha stadi za mawasiliano katika Kiswahili.

Isitoshe, ili kupata maoni ya walimu kuhusu nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano, mbinu ya uchambuzi wa matini ilikamilishwa kwa kutumia pia mbinu ya usaili.

### 3.6.2 Usaili

Usaili ni mchakato wa mahojiano ya moja kwa moja kati ya mtafiti na mshiriki wa utafiti ambapo mtafiti anauliza maswali ili kupata taarifa kuhusu tukio, suala au mada inayofanyiwa utafiti (Jamshed, 2014). Mbinu ya usaili ilitumiwa kwa kuwa wakati wa ukusanyaji data, mtafiti alifanya mahojiano ya moja kwa moja na walimu wanaofundisha Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

Mbinu ya usaili ilitumiwa ili kuchunguza maoni ya walimu kuhusu nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Aidha, kuna taarifa halisi za kivitendo na kimazingira ambazo hazikuweza kutolewa kwa ufasaha kupitia usaili. Kwa kukusanya taarifa kama hizo, mtafiti alitumia mbinu ya ushuhudiaji.

### 3.6.3 Ushuhudiaji

Ushuhudiaji ni mojawapo ya mbinu za kukusanya data katika utafiti wa kitaamuli. Mbinu hii inajumuisha kuangalia, kuchunguza na kurekodi data katika eneo la utafiti (Ciesielska, Boström & Öhlander, 2018). Katika utafiti uliofanyika, ushuhudiaji ulifanyika pale ambapo mtafiti alienda kwenye shule ya CXR Nyanza E.S. Nyanza na G.S. Kigoma kushuhudia somo la fasihi andishi likifundishwa kwenye kidato cha 6 LFK. Mbinu hii ilishiriki katika utimizaji wa lengo mahususi la kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

Aidha, mbinu ya ushuhudiaji ilikamilisha mbinu ya usaili katika kupata ufahamu wa ziada kupitia uchunguzi wa moja kwa moja wa kivitendo kuhusu nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

## 3.7 Aina ya Data Zilizokusanywa

Katika utafiti tuliofanya, data za msingi pamoja na data za upili zilikusanywa ili kutimiza malengo mahususi ya utafiti. Utafiti tuliofanya ulikusanya data za aina mbili ambazo ni data za msingi na upili.

### 3.7.1 Data za Msingi

Kwa mujibu wa Hox & Boeije (2005), data za msingi ni taarifa au data ambazo zinakusanywa moja kwa moja kutoka vyanzo vya asili au kwa mara ya kwanza kwa madhumuni ya utafiti. Data

za msingi zinahusisha taarifa ambazo hupatikana kupitia ushuhudiaji, usaili au mbinu nyingine za kukusanyia data kwa lengo la kutimiza malengo ya utafiti (Hox & Boeije (whj). Kwa hiyo, data za msingi zilikusanywa kupitia ushuhudiaji na usaili kati ya mtafiti na washiriki wa utafiti ambao ni walimu wa Kiswahili katika shule teule za Wilaya ya Nyanza nchini Rwanda. Data hizi za msingi zilitumika kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule zasekondari teule wilayani Nyanza nchini Rwanda.

### 3.7.2 Data za Upili

Data za upili ni data ambazo zimekusanywa awali na watafiti wengine kwa malengo tofauti na yale ya utafiti unaofanyika Martins, Cunha, & Serra (2018). Watafiti hawa wanaendelea kueleza kwamba, data za upili ni data ambazo zinapatikana kutoka vyanzo vya maarifa tofauti kama vile machapisho ya awali, ripoti, takwimu au nyaraka za awali zilizokusanywa na watafiti au taasisi mahususi. Hivyo basi, data za upili zilikusanywa kupitia mbinu ya uchambuzi wa matini.

Data hizi zilikusanywa kwa madhumuni ya kutimiza lengo la kuunda miongozo ya kutumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi ya mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

## 3.8 Vifaa vya Utafiti

Kothari (2012) anaeleza vifaa vya utafiti kama zana na rasilimali zote zinazotumiwa katika mchakato wa kukusanya na kuchambua data za utafiti toka mwanzo hadi mwisho wa utafiti. Kwa hiyo, katika utafiti uliofanyika, vifaa vya utafiti vilihusisha mwongozo wa usaili, mwongozo wa ushuhudiaji, mwongozo wa uchambuzi wa matini, kompyuta, kalamu, karatasi, daftari, simu, rekoda na kihifadhi-data.

Mwongozo wa usaili ulitumika kwa mahojiano ili kupata maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano. Mwongozo wa ushuhudiaji, ulitumika kukusanya data kuhusu hali halisi ya nafasi nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari zilizoteuliwa. Mwongozo wa uchambuzi wa matini ulitumika kuchambua nyaraka za kitaaluma.

Kompyuta ilitumika kuandika na kuhifadhi data. Daftari, kalamu na karatasi zilitumika kuchukua notisi wakati wa utafiti, na simu ilitumika kwa mawasiliano na kupiga picha. Rekoda ilitumika

kurekodi mahojiano kwa usahihi. Mwisho, na kihifadhi-data kilitumika kuhifadhi kumbukumbu zote kwa usalama na urahisi wa uchambuzi wa baadaye. Vifaa hivi vilisaidia katika kukusanya na kuchambua data kwa njia sahihi.

### 3.9 Uchanganuzi wa Data

Kothari (khj) anasema kuwa uchanganuzi wa data ni mchakato wa kutumia mbinu tofauti ili kufafanua, kuelezea, kufupisha na kukadiria data. Kwa hiyo, uchanganuzi wa data katika utafiti uliofanyika, ulitumia mkabala wa kitaamuli.

Uchanganuzi wa data unahusisha uchambuzi wa data zilizokusanywa, uainishaji na upangaji wa data katika makundi husika ili kuweza kuziwasilisha kwa kadiri ya malengo ya utafiti yaliyonuiwa kufikiwa (Kothari, khj). Data zilichanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Kama inavyoelezwa na Kawulich (2004), mkabala wa kitaamuli ni hutumia maneno na maelezo kwa kuchanganua na kufasili data za utafiti. Kwa kuwa utafiti tulioufanya ulikuwa wa kitaamuli, ndiyo sababu tuliamua kutumia mkabala kitaamuli katika uchanganuzi wa data za utafiti huo. Hivyo basi, data zilichanganuliwa, kufasiliwa na kuwasilishwa kwa kutumia madondoo yaliyofuatiwa na maelezo.

### 3.10 Itikeli za Utafiti

Hassan (2023) anasema kwamba uzingativu wa itikeli za utafiti ni kanuni muhimu zinazowalinda washiriki kwa kuhakikisha kushiriki kwao kwa hiari, ufahamu wa kina wa malengo ya utafiti, uhakika wa usiri, kuficha majina na kuepuka madhara yoyote ya kimwili au kisaikolojia yanayoweza kuwafikia washiriki wa utafiti.

Ili kuhakikisha uadilifu wa utafiti, mikakati ifuatayo ilizingatiwa. Kwanza, kabla ya kuanza kukusanya data, mtafiti aliomba vibali kutoka Chuo Kikuu cha Rwanda na kutoka Wilaya ya Nyanza. Vibali hivi vilimwezesha mtafiti kukusanya data kwa usalama. Hata hivyo, kulikuwa na mpishano wa tarehe ambapo kibali kutoka wilayani kilitolewa kabla ya kile kutoka chuoni. Hii ilitokana na kwamba, mtafiti alipoomba kibali cha kukusanya data kutoka chuoni, afisa anayehusika alikuwa likizoni.

Hivyo basi, mtafiti alipewa ushauri wa kutumia nyaraka ya itikeli za utafiti iliyosainiwa kuomba kibali cha kukusanya data kutoka wilayani. Alifanya hivyo, na wilaya ikampa kibali. Baada ya

afisa husika kutoka likizoni, mtafiti alikuwa tayari amemaliza kukusanya data. Hii ndiyo sababu inaonekana kuwa kibali kutoka wilayani kilitolewa kabla ya kile kutoka chuoni.

Pili, data za utafiti zilihifadhiwa kwa kutumia misimbo ili kuzilinda taarifa za watu binagfsi walioshiriki katika utafiti. Tatu, mtafiti alihakikishia washiriki kuwa taarifa zao hazitatumiwa nje ya malengo ya utafiti uliofanyika. Nne, kwenye mwongozo wa usaili, mtafiti aliambatisha barua ambayo inaelezea washiriki wa utafiti malengo ya utafiti. Tano, mtafiti aliepukana na upendeleo katika kuripoti matokeo ya utafiti. Sita, ukusanyaji data ulitegemeana na utashi wa kila mshiriki wa kushiriki katika utafiti uliofanyika. Hii ina maana kwamba, hakuna mshiriki aliyelazimishwa kushiriki katika utafiti na hakukuwa na malipo ya fedha kwa washiriki wa utafiti wetu.

## 3.11 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Uhalali ni moja ya mbinu za utafiti wa kitaamuli ambayo unategemea kuhakikisha ikiwa matokeo ya utafiti ni sahihi kutokana na malengo ya utafiti (Creswell & Cresswell, 2018). Wataalamu hawa wanaendelea kusema kwamba uhalali wa utafiti huhusisha dhana tofauti ambazo ni pamoja na uaminifu, uhalisia na uaminikaji. Aidha, kulingana na Miles, Huberman & Saldana (2014), uthabiti wa utafiti ni jinsi ya kuaminika, kukubalika na kurudia matokeo ya utafiti, ukionesha uhakika wa matokeo na uwezekano wa kujirudia katika mazingira tofauti. Kwa lengo la kuhakikisha uhalali na uthabiti wa utafiti, katika utafiti uliofanyika, mbinu za hapo chini zilizingatiwa.

Kwanza, kabla ya kuanza utafiti, mtafiti alielezea kwa washiriki malengo na umuhimu wa utafiti. Pili, mtafiti alitumia lugha rahisi ili aweze kuelewana na washiriki wa utafiti kwa ufasaha. Tatu, mtafiti alitumia njia mseto inayopunguza hatari ya makosa ya utafiti yaliyoweza kujitokeza kutokana na mtafiti au washiriki wa utafiti. Mwisho, mtafiti alijiepusha na kubadilisha taarifa zilizopatikana wakati wa ukusanyaji wa data.

## 3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii ya tatu inazungumzia methodolojia ya utafiti. Sura husika inagawanyika katika sehemu ndogo. Sehemu hizo ni: utangulizi, usanifu wa utafiti, paradima ya utafiti, eneo la utafiti, wango la utafiti, sampuli ya utafiti, usampulishaji, aina za data, mbinu za ukusanyaji wa data, vifaa vya kukusanyia data, uchanganuzi wa data, itikeli za utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, mpango kazi na muhtasari wa sura ya tatu.

## SURA YA NNE: MJADALA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO YA UTAFITI

### 4.1 Utangulizi

Utafiti tuliofanya ulikuwa na lengo la jumla la kuchunguza nafasi ya ufundishaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Utafiti husika ulilenga kutimiza malengo mahususi mawili. Kwanza, kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Pili, kuunda miongozo ya kutumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi ya mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Kwa hiyo, sura hii inahusisha mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti kutegemeana na malengo mahususi ya utafiti. Hivyo basi, sura hii inagawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni pamoja na utangulizi, tathmini ya nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano, miongozo ya kutumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi ya mawasiliano na muhtasari wa sura husika.

### 4.2 Tathmini ya Nafasi ya Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano

Lengo mahususi la kwanza katika utafiti tuliofanya lilikuwa kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Ili kutimiza lengo hili, kwanza, mtafiti alitumia mbinu ya uchambuzi matini kuchambua maandiko ya kitaaluma yanayoeleza hili na matini za kipedagojia za walimu wa fasihi andishi. Pili, alikusanya data kutoka kwa walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza kwa kutumia usaili. Tatu, alishuhudia masomo ya fasihi andishi akitumia mwongozo wa ushuhudiaji ili kutathmini hali halisi ya nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano ilivyo na inavyowezekana katika madarasa la Kiswahili kwenye shule teule.

Isitoshe, mjadala kuhusu lengo hili uliongozwa na mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Mawasiliano iliyoasisiwa na Scudder (1980). Mhimili husika unaonesha kwamba mawasiliano ni mchakato wa kiufundi wa kuhamisha mawazo, ujumbe na hisia kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine. Kwa hiyo, mawasiliano ni mchakato ulio imara ambao una sheria zilizowekwa ambazo zinafaa kufuatwa. Hivyo basi, hapo chini ni tathmini ya nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano.

### 4.2.1 Fasihi Andishi katika Kukuza Uwezo wa Mawasiliano

Taarifa zilizopatikana kutoka uchanganuzi wa matini za kitaaluma zimehusisha watafiti tangulizi ambao walishughulikia nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano. Baadhi ya watafiti hao wamebainisha kwamba fasihi andishi ina nafasi ya kukuza uwezo wa mawasiliano. Kwanza, Priyadharshini, & Hameed (2018) wanasema kwamba viongozi wazuri waliowahi kuwepo hapa duniani ni wale waliobarikiwa na kipaji cha mazungumzo na kuingia mioyoni mwa watu kupitia uwezo wao wa mawasiliano. Uwezo huu wa mawasiliano unapatikana kupitia fasihi. Mawazo ya watafiti hawa kuhusu nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano yanapatikana hapo chini:

> We have come across leaders blessed with gift of the gab and enter the hearts of people through their communication skills. One of the main reasons can be honestly attributed to the study of literature. Communicative competence is one of the desirable leadership qualities. Reading maketh a full man; writing an exact man. To be a successful communicator, one must be a full man and exact man too. Reading and writing the productive language skills in communication can be developed well through study of literature.
> **Chanzo:** Priyadharshini, & Hameed (2018, uk.31)

> Tumekutana na viongozi waliobarikiwa na kipaja cha kuongea na kuingia mioyoni mwa watu kupitia stadi zao za mawasiliano. Sababu moja kuu inaweza kuhusishwa kwa uaminifu na kusoma fasihi. Uwezo wa kuwasiliana ni mojawapo ya sifa zinazotamaniwa za uongozi. Kusoma humfanya mtu kuwa kamili; kuandika humfanya mtu kuwa sahihi. Ili kuwa mwasilianaji mzuri, mtu lazima awe kamili na sahihi pia. Kusoma na kuandika, ujuzi wa lugha wa uzalishaji katika mawasiliano unaweza kuendelezwa vyema kupitia kusoma fasihi (T.Y).

Kutokana na data zilizopo kwenye dondoo hili, tunaona kwamba, viongozi wenye ujuzi wa mawasiliano wanapata uwezo huo kupitia kusoma fasihi, ambayo huwafanya kuwa kamili na sahihi. Kusoma na kuandika ni muhimu kwa ujuzi wa lugha na vinaweza kuimarishwa kwa kusoma fasihi. Kwa kuongezea, Sharma, Devi, Dangoria & Jain (2022) wanabainisha kwamba fasihi andishi inakuza uwezo wa mawasiliano miongoni mwa wanafunzi katika dondoo lifuatalo:

> Literature helps learners develop their communication skills by strengthening their pragmatic competence. It provides students with the capacity to understand and convey meanings that are more appropriate and acceptable in various cultural and social contexts.
> **Chanzo:** Sharma, Devi, Dangoria & Jain (2022, uk.157)

> Fasihi huwasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa mawasiliano kwa kuimarisha umahiri wao wa kipragmatiki. Fasihi huwapa wanafunzi uwezo wa kuelewa na kuwasilisha maana ambazo ni sahihi zaidi na zinazokubalika katika muktadha wa kitamaduni na kijamii. (T.Y)

Kutokana na data hizi, tunaona kwamba fasihi inaboresha uwezo wa wanafunzi katika mawasiliano kwa kuimarisha umahiri wao wa kipragmatiki. Hii ina maana kwamba fasihi inawasaidia kuelewa na kuwasiliana kwa ufanisi katika muktadha wa kitamaduni na kijamii. Aidha, walimu wenyewe walioshiriki kwenye utafiti wetu wanabainisha kwamba fasihi andishi ina nafasi kubwa katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi kupitia dondoo hili:

> Nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano ni kuwapa wanafunzi uwezo wa kuwasiliana kwa ufasaha. Kupitia ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi, wanafunzi wanajifunza kanuni zote za mawasiliano, hali inayowafanya kuwa wataalamu wa mawasiliano (M1).
> **Chanz**o: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na data zilizopo kwenye dondoo hili, tunaona kwamba, fasihi andishi ina nafasi muhimu katika kuboresha stadi za mawasiliano kwa kuwapa wanafunzi ujuzi wa kuwasiliana kwa ufasaha. Kupitia mafunzo ya fasihi, wanafunzi wanajifunza kanuni za mawasiliano ambazo zinawawezesha kuwa wataalamu bora katika eneo hili.

Matini za kitaaluma na maoni ya walimu yanaonesha kwamba fasihi andishi ina nafasi ya kukuza uwezo wa mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Licha ya haya, katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza, fasihi andishi haijakuwa na nafasi ya kutosha ya kukuza uwezo wa mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu data za uwandani zinaonesha kwamba walimu wa Kiswahili katika shule hizi hawajumuishi kwa ufasaha ukuzaji wa stadi mawasiliano katika ufundishaji wa fasihi andishi. Pia, hawajumuishi stadi za mawasiliano kwa ufasaha katika maandalio ya masomo na katika tathmini za masomo ya fasihi andishi.

Ukweli huu unathibitishwa na matokeo ya ushuhudiaji wa uwandani katika shule A ambapo mwalimu (M4) alikuwa anafundisha somo la *Tanzu za Fasihi Andishi*. Katika somo hili, mwalimu alitumia kifungu cha habari kuhusu tanzu za fasihi andishi, akatoa maelezo kidogo kisha akaomba wanafunzi kufanya kazi katika makundi. Baada ya shughuli za makundi, wanafunzi walipitia kifungu na kujibu maswali yanayohusiana nacho.

Katika uwasilishaji, kila kikundi kilimteua mwanakikundi mmoja wa kuwasilisha matokeo. Mara baada ya kuwasilisha, mwalimu alitoa mrejesho. Mrejesho huu uliweka mkazo katika usahihishaji wa makosa ya kisarufi na kitahajia yaliyofanyika. Mwisho, mwalimu alitoa kazi ya nyumbani. Kazi hii ilihusu tanzu za fasihi andishi ambazo ni hadithi fupi andishi na riwaya. Hata hivyo, mwalimu alijikita zaidi katika maelezo ya tanzu za fasihi andishi badala ya kutumia tanzu hizi kukuza uwezo wa mawasiliano miongoni mwa wanafunzi.

Data zilizopatikana kutoka madarasa mengine zilithibitisha kwamba walimu wa Kiswahili wanapofundisha fasihi andishi, hawajumuishi kikamilifu ukuzaji wa stadi za mawasiliano. Walimu wanatilia mkazo zaidi katika kanuni za fasihi badala ya mbinu zinazohitaji kuimarisha stadi za mawasiliano na hivyo wanafunzi wanakosa mazoezi muhimu ya kukuza uwezo wa kuwasiliana kwa ufasaha. Hii inaonekana kwa jinsi walimu wanavyoshindwa kutumia fasihi andishi kama chombo cha kukuza stadi za mawasiliano ya maneno na yasiyo ya maneno.

Walimu wanapofundisha fasihi andishi, mara nyingi wanajikita katika kuwapa wanafunzi ujuzi wa kuelewa na kuzingatia nadharia za fasihi, lakini wanashindwa kutumia mbinu zinazosaidia kukuza mawasiliano ya kina. Kwa mfano, walimu wanapozingatia zaidi uelewa wa nadharia na mbinu za fasihi, wanafunzi, hawapati fursa ya kutekeleza mazoezi yanayohusisha mawasiliano kama vile kuwasiliana kwa ufasaha, kusikiliza kwa makini, na kutumia mawasiliano yasiyo ya maneno. Hii inasababisha wanafunzi kutokuza vya kutosha na uwezo wa mawasiliano wanapofanya kazi na fasihi andishi.

Kwa hiyo, changamoto kubwa ni kwamba walimu wa Kiswahili wanahitaji kubadilisha mbinu zao za ufundishaji ili kuzingatia mbinu zinazokidhi mahitaji ya stadi za mawasiliano kwa kina. Hii inajumuisha matumizi ya fasihi andishi kama chombo cha kukuza uwezo wa mawasiliano ya maneno na yasiyo ya maneno, pamoja na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata fursa za kutosha ya kuwasiliana na kubadilishana mawazo.

Matokeo haya yanaonesha umuhimu wa kufanya mabadiliko katika mbinu za ufundishaji ili kuhakikisha kwamba fasihi andishi inachangia kikamilifu katika kukuza uwezo wa mawasiliano miongoni mwa wanafunzi.

Kwa hivyo, changamoto kubwa ni kwamba walimu wa Kiswahili wanatumia mbinu za ufundishaji wa fasihi ambazo hazikidhi mahitaji ya stadi za mawasiliano kwa kina. Walimu walioshiriki katika utafiti wetu walionesha kwamba changamoto inayowazuia kutumia fasihi andishi kwa ufasaha ili kuimarisha stadi za mawasiliano ni kutojua mbinu bora za kutumia. Kwa mfano, mtafitiwa mmoja alisema:

> Ingawa tunatumia fasihi andishi katika madarasa yetu, tunakabiliwa na changamoto kubwa katika kujua jinsi ya kuitumia ipasavyo kukuza stadi za mawasiliano. Mara nyingi, tunajikita zaidi kwenye vipande vya maandiko na maelezo ya nadharia, badala ya kutumia mbinu zinazowezesha wanafunzi kuwasiliana kwa ufasaha. Tunahitaji mafunzo zaidi na mwongozo juu ya jinsi ya kutumia fasihi kuimarisha mawasiliano ya maneno na yasiyo ya maneno ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapokea mazoezi ya kutosha katika eneo hili muhimu. (M3)
> **Chanz**o: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na data hizi, tunaona kwamba, walimu wanakumbana na changamoto katika kutumia fasihi andishi kwa ufanisi ili kukuza stadi za mawasiliano. Hii inatokana na kutojua mbinu bora za kufundishia ambazo zingeweza kuimarisha mawasiliano. Kwa hiyo, walimu wanajikita zaidi katika kusoma kazi za fasihi na nadharia badala ya mbinu zinazowezesha mawasiliano yenye ufanisi. Hii ina maana kwamba kuna stadi muhimu katika mawasiliano ambazo hazitiliwi mkazo. Hizi ni pamoja na kusikiliza kwa makini, kuzungumza kwa ufasaha, stadi za mawasiliano yasiyo ya maneno na ujasiri.

Ili kukuza stadi za mawasiliano kikamilifu, walimu wa Kiswahili wanalazimika kutumia kazi za fasihi andishi ambazo zinakuza uwezo wa wanafunzi wa kusoma, kuandika, kusikiliza kwa makini, na kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha. Aidha, walimu wanapaswa kutumia mbinu ambazo zinakuza stadi za mawasiliano yasiyo ya maneno.

Isitoshe, ni lazima kuwapa wanafunzi fursa ya kuwasilisha kazi walizozifanya, kuulizana maswali, kubadilishana mawazo, na kuigiza kazi mbalimbali za fasihi andishi. Jambo hili litawasaidia wanafunzi kuzimudu sheria zinazotumiwa katika mchakato wa mawasiliano ya maneno na yasiyo ya maneno. Hili linaendana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya mawasiliano unaosema kwamba mawasiliano ni mchakato ulio imara ambao una sheria zilizowekwa ambazo zinafaa kufuatwa.

### 4.2.2 Fasihi Andishi katika Kukuza Stadi za Lugha Zinazohitaji katika Mawasiliano

Stadi za lugha ni pamoja na kusoma, kuandika, kusikiliza na kuzungumza (Priyadharshini, & Hameed, 2018). Stadi hizi zinahitajika katika mawasiliano. Kwa hiyo, katika utafiti wetu, imedhihirika kwamba fasihi andishi ina nafasi ya kukuza stadi za lugha zinazohitajika katika mawasiliano. Kwanza, taarifa kutoka katika uchambuzi wa matini za kitaaluma zimethibitisha nafasi hii. Kwa mfano, Priyadharshini, & Hameed (whj) wanabainisha nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa stadi za mwawasiliano katika dondoo lifuatalo:

> Listening, Speaking, Reading and Writing are not communication skills, but language learning skills. Communicative competence is attained through mastery of language learning skills. All these four skills are interrelated. Even though there are many approaches to language teaching-learning, Literature Based approach has got its own unique advantages over other approaches. In other approaches, the focus is on developing the skills and sub-skills of the target language, but in literature-based approach, learners, besides developing communication skills in target language, understand life and human values.
> **Chanzo**: Priyadharshini, & Hameed (2018, uk.31)

> Kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika si stadi za mawasiliano, bali ni stadi za kujifunza lugha. Uwezo wa kuwasiliana hupatikana kupitia umahiri wa stadi za kujifunza lugha. Stadi hizi nne zote zina uhusiano wa karibu. Ingawa kuna mbinu nyingi za kufundisha na kujifunza lugha, mbinu inayotumia fasihi ina faida zake za kipekee ikilinganishwa na mbinu nyingine. Katika mbinu nyingine, mkazo unawekwa katika ukuzaji wa stadi na stadi ndogo za lugha lengwa, lakini katika mbinu inayotumia fasihi, wanafunzi, mbali na kukuza stadi za mawasiliano katika lugha lengwa, pia wanaelewa maisha na maadili ya kibinadamu. (T.Y)

Kutokana na data hizi, tumeona kwamba kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika ni stadi za kujifunza lugha badala ya stadi za mawasiliano moja kwa moja. Aidha, tunaona kwamba, mbinu inayotumia fasihi inatoa faida za kipekee kwa kukuza ufahamu wa lugha pamoja na maisha na maadili ya kibinadamu.

Zaidi ya hayo, kwa kubainisha nafasi ya fasihi katika ujifunzaji wa lugha, Venkateswar & Mohana (2015) wanasema kwamba, kama mtu anataka kuwasiliana kwa ufasaha, ni lazima ajifunze fasihi. Watafiti hawa wanabainisha wazo hili kwenye dondoo lifuatalo:

> Literature is about letters, words, phrases, sentences, paragraphs, essays and storie. In Language acquisition we must focus on all these areas of knowledge. Communication is about ideas, opinions, feelings, information to share with others for personal as well as professional purposes. The same is with literature. If language is mind, literature is heart. Language is a set of lexicographical, grammatical, syntactical systems. Anybody who wish to enhance one's language skills for communication ability, he or she should mainly focus on literature.
> **Chanzo**: Venkateswar & Mohana (2015, uk.193)

> Fasihi inahusisha herufi, maneno, virai, sentensi, aya, insha na hadithi. Katika kujifunza lugha, tunapaswa kuzingatia maeneo yote haya ya maarifa. Mawasiliano yanahusisha mawazo, maoni, hisia na taarifa za kuchangia na wengine kwa madhumuni ya kibinafsi na kitaalamu pia. Vivyo hivyo na fasihi. Ikiwa lugha ni akili, fasihi ni moyo. Lugha ni mfumo wa maneno, sarufi na muundo wa sentensi. Yeyote anayetaka kuimarisha stadi za lugha kwa ajili ya mawasilano, anapaswa kuzingatia hasa fasihi. (TY)

Kutokana na data hizi, ni wazi kwamba fasihi ni muhimu katika kujifunza lugha kwani inajumuisha vipengele vyote vya lugha. Pia, inaeleza kuwa yeyote anayetaka kuimarisha stadi za lugha lazima azingatie fasihi kwa kuwa lugha ni mfumo wa maneno na sarufi, wakati fasihi ni moyo wa lugha hiyo. Hii inasisitiza nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa stadi za lugha unaohitajika katika mawasiliano. Zaidi ya hayo, taarifa kutoka kwenye mahojiano na walimu wa Kiswahili yanabainisha kwamba, fasihi andishi inawasaidia wanafunzi kujifunza jinsi ya kutumia lugha kwa ufasaha, iwe ni katika kuzikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza, huku wakizingatia muktadha wa kiutamaduni na kijamii. Mwalimu mmoja alibainisha hili katika dondoo lifuatalo:

> Fasihi andishi ina nafasi kubwa katika kufundisha wanafunzi jinsi ya kutumia lugha kwa ufasha, iwe ni kwa maandishi au mazungumzo. Pia, inawawezesha wanafunzi kujua kuwasiliana kupitia mbinu ya kuandika na kusoma. Vilevile, fasihi andishi huwezesha wanafunzi kutumia lugha kwa kuzingatia muktadha wa kiutamaduni na kijamii katika kuandika na kuzungumza lugha ya Kiswahili (M3).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Hapa tunaona kwamba fasihi andishi ina nafasi kubwa katika kufundisha wanafunzi kutumia lugha kwa ufasaha, kusoma, na kuandika. Pia, inawasaidia kuwasiliana kwa kuzingatia muktadha wa kiutamaduni na kijamii. Aidha, mtafitiwa mwingine aliunga mkono aliyetangulia katika dondoo lifuatalo:

> Ili mtu aweze kuwasiliana vizuri ni lazima awe na uwezo wa kusoma, kuandika, kusikiliza, na kuzungumza. Uwezo huu unapatikana kutokana na kufundisha na kujifunza fasihi. Kwa hiyo, nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano ni kuwezesha wanafunzi wetu kusoma, kuandika, kusikiliza, na kuzungumza kwa ufasaha (M4).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na dondoo hili, tunaona kwamba, ili mtu aweze kuwasiliana vizuri, anahitaji kuwa na uwezo wa kusoma, kuandika, kusikiliza na kuzungumza. Pia, fasihi ina nafasi muhimu katika kufundisha na kujifunza stadi hizi za mawasiliano. Ingawaje imebainika kwamba fasihi ina nafasi katika ukuzaji wa stadi za lugha zinazohitajika katika mawasiliano, data za usaili zinaonesha kwamba walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza wanapofundisha stadi za mawasiliano wanajikita sana tu katika stadi za lugha na kuzisahau stadi nyingine zinazohitajika katika mawasiliano fasaha. Hali hii inatokana na kwamba walimu wengi wanadhani kwamba stadi za mawasiliano ni kusoma, kuandika, kusikiliza na kuandika tu.

Ingawa imebainika kwamba fasihi ina nafasi katika ukuzaji wa stadi za lugha zinazohitajika katika mawasiliano, mahojiano na walimu husika yalionesha walimu wanazichanganya stadi za lugha na stadi za mawasiliano. Hii inatokana na mtazamo finyu wa stadi za lugha, unaozingatia sana kusoma, kuandika, kuzungumza na kusikiliza, ambazo ni sehemu tu za ujuzi wa lugha. Hii ilithibitishwa na fasili mbalimbali zinazotolewa na walimu wa Kiswahili kuhusu tadi za mawasiliano. Dondoo hli ni mojawapo wa fasili hizo:

> Kwa mujibu wangu, stadi za mawasiliano ni stadi za kusikiliza, kuzungumza, kuandika na stadi za kusoma. Stadi za kusikiliza zinahusisha uwezo wa kuelewa na kufasiri ujumbe unaowasilishwa kwa njia ya maneno, stadi za kuzungumza zinahusisha uwezo wa kueleza mawazo na hisia kwa njia ya maneno kwa ufasaha, stadi za kusoma zinahusisha uwezo wa kuelewa na kufasiri maandishi, na stadi za kuandika zinahusisha uwezo wa kuandika ujumbe kwa njia inayoweza kueleweka na wasomaji (M1).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na taarifa zilizotolewa na M1, stadi za mawasiliano zinahusisha stadi nne. Stadi ya kwanza ni stadi ya kuzungumza inayohusisisha uwezo wa kusikiliza. Stadi ya pili ni kusikiliza inayohusisha uwezo wa kuelewa na kufahamu ujumbe unaotolewa na mzungumzaji. Vilevile, stadi ni kusoma ambayo inahusisha uwezo wa kusoma maandishi. Isitoshe, stadi ya mwisho ni stadi ya kuandika ambayo inahusisha uwezo wa kuwasilisha ujumbe kwa njia ya maandishi.

Kadhalika, mwalimu mmoja miongoni mwa walimu walioshiriki katika utafiti tuliofanya alibainisha stadi za mawasiliano kama ifuatavyo:

> Aina muhimu za stadi za mawasiliano ni pamoja na kusikiliza kwa makini kinachozungumzwa, kuwasilisha mawazo kwa uwazi na ufasaha, kuandika ujumbe kwa usahihi na kuelewa maandishi kwa kina. Stadi hizi pia, zinajumuisha matumizi ya lugha sahihi, sauti wazi na lugha sanifu inayofaa (M3).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na data zilizopo kwenye dondoo hili, tumeona kwamba, stadi za mawasiliano ni muhimu na zinajumuisha kusikiliza kwa makini, kuwasilisha mawazo kwa uwazi, kuandika kwa usahihi na kuelewa maandishi kwa kina. Aidha, stadi hizi zinahusisha pia matumizi ya lugha sahihi, sauti wazi na lugha sanifu inayofaa. Maelezo ya walimu kuhusu stadi za lugha ni tofauti na fasili pana zaidi ya Nguyen, Warren & Fehring (2014:96), inayosema kuwa stadi za mawasiliano ni uwezo wa kuhamisha ujumbe kwa njia ya maneno au isiyo ya maneno. Hii ina athari kubwa kwa kuwa ilionekana kwamba walimu wanapofundisha fasihi andishi, wanasisitiza tu ukuzaji wa stadi za lugha na kusahau stadi nyingine muhimu katika mawasiliano.

Zaidi ya hayo, tathmini zinazoandaliwa na walimu wa fasihi zinahusisha sana ukuzaji wa stadi za kusoma, kufahamu maandishi na kuandika. Miongoni mwa tathmini za walimu watatu zilizochunguzwa, hakuna tathmini iliyohusisha kutathmini uwezo wa wanafunzi wa kusikiliza kwa makini, kuzungumza kwa ufasaha, ujasiri na stadi nyingine za mawasiliano yasiyo ya maneno. Hapo chini ni mojawapo ya tahmini zilizofanyiwa uchunguzi. Tathmini hiyo iliandaliwa na M2.

**Kielelezo 1: Mfano wa Tathmini**

| | |
|---|---|
| **SEHEMU YA IV: FASIHI** | **(Alama 11)** |
| 1) Je fasihi ni nini? | **(Alama 1)** |
| 2) Eleza tofauti iliyopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. | **(Alalama 4)** |
| 3) Fasihi ni kioo cha jamii. Jadili. | **(Alama 4)** |
| 4) Tofautisha tabia tatu za wahusika katika riwaya. | **(Alama 3)** |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2024)

Kutokana na ielelezo 1, tunaona mfano wa tathmini ya fasihi ambayo inajikita zaidi katika kupima stadi za kuandika na kusoma, huku ikiacha nje stadi muhimu za kuzungumza, kusikiliza kwa makini, na ujasiri ambazo zinahitajika katika mawasiliano fasaha kwa lugha ya Kiswahili. Maswali yote yanahitaji majibu ya maandishi na kueleza tofauti, kujadili na kutofautisha tabia za wahusika.

Pia, alama zilitolewa kwa kila swali kulingana na uwezo wa mwanafunzi kusoma na kuandika. Hakuna kipengele chochote kinachohusisha mwanafunzi katika mawasiliano ya mdomo, usikilizaji wa makini na ujasiri unaoweza kukuzwa kupitia uigizaji. Hivyo, tathmini hii inakosa mlingano katika kukuza stadi zote za mawasiliano ya mwanadamu.

Kulingana na Khakasa (2018), kuna changamoto katika ufundishaji wa Kiswahili ambapo mkazo mkubwa unawekwa kwenye kusoma na kuandika kuliko stadi nyingine muhimu kama vile kusikiliza kwa makini, kuzungumza kwa ufasaha, kufahamu hisia, ujasiri, na matumizi ya ishara katika mawasiliano.

Hivyo basi, ijapokuwa walimu wa Kiswahili wanafanya vizuri katika ufundishaji wa stadi za lugha zinazohitajika katika mawasiliano, kuna haja ya walimu hawa kubadilisha mbinu wanazotumia ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanapata mafunzo yanayowezesha kukuza stadi zote za mawasiliano kwa usawa na ufanisi.

### 4.2.3 Fasihi Andishi Hukuza Stadi ya Ujasiri

Ujasiri ni stadi muhimu katika mawasiliano. Stadi hii inahusisha uwezo wa kuzungumza bila woga, kujieleza kwa uhakika na kushiriki kikamilifu katika mazungumzo (Atkin, 2012:585) Stadi hii inawezesha mtu kuvuka vikwazo na kushughulikia mambo kwa utulivu na ufanisi. Katika utafiti wetu, imebainika kwamba fasihi andishi ina nafasi ya kukuza stadi ya ujasiri miongoni mwa wanafunzi. Kwanza, data za uchambuzi wa matini za kitaaluma zinaonesha kwamba fasihi andishi inawasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa kuwasiliana na wengine kwa kujiamini bila woga.

> Literature is essential in the language classroom. It not only entertains readers but also boosts self-confidence and fosters critical thinking. Additionally, literature includes various forms like prose, poetry, drama, novels, short stories, and others. These forms help students enhance their communication skills and gain the ability to communicate confidently.
> **Chanzo**: Ilankumaran & Deepa (2018, uk.620)

> Fasihi ni muhimu katika darasa la lugha. Haiburudishi tu wasomaji bali pia huongeza ujasiri na kukuza tafakuri tunduizi. Zaidi ya hayo, fasihi inajumuisha aina mbalimbali kama vile nathari, mashairi, tamthilia, riwaya, hadithi fupi na ania nyinginezo. Aina hizi zinasaidia wanafunzi kuboresha stadi zao za mawasiliano na kupata uwezo wa kuwasiliana kwa ujasiri (T.Y).

Kulingana na watafiti hawa, tunaona kwamba fasihi ni muhimu katika darasa la lugha kwani inasaidia kuongeza ujasiri na kukuza uwezo wa kufikiri. Aidha, kupitia aina mbalimbali za fasihi kama nathari, mashairi na tamthilia, wanafunzi wanapata nafasi ya kuboresha stadi zao za mawasiliano na kuwasiliana kwa ujasiri. Pengine, ufundishaji wa fasihi andishi unawalazimisha wanafunzi kusoma kazi za fasihi za aina mbalimbali. Kwa mujibu wa Morris (2021), usomaji hukuza stadi ya ujasiri.

> You can explore new worlds or acquire new skills through reading, but its benefits extend well beyond mere enjoyment and education. Reading profoundly impacts our character by enhancing self-confidence, expanding our perspectives, and empowering each reader individually.
> **Chanzo**: Morris (2021, uk.1)

> Unaweza kugundua dunia mpya au kupata ujuzi mpya kupitia kusoma, lakini faida zake zinaenda mbali zaidi ya burudani na elimu ya kimsingi. Kusoma kunaathiri tabia zetu kwa kina kwa kuboresha ujasiri, kupanua mtazamo wetu na kukuza uwezo wa kila mmoja binafsi. (TY)

Kulingana na dondoo hili, kusoma kuna nafasi muhimu katika kuendeleza stadi ya ujasiri. Hii ni kwa sababu kusoma hupanua mtazamo wetu na kukuza uwezo wa kila mmoja binafsi. Pia, walimu walioshiriki katika utafiti, walionesha kwamba fasihi andishi husaidia katika kujenga ujasiri wa wanafunzi, hasa kupitia mbinu za kusimulia hadithi fupi andishi na uigizaji wa tamthilia, ambazo huwapa fursa ya kujieleza kwa ufasaha mbele ya wengine. Mwalimu mmoja alithibitisha hili akisema:

> Ninadhani kuwa, fasihi andishi inasaidia sana katika kuwezesha wanafunzi kuwasilisha mawazo yao bila wasiwasi. Kupitia kazi za fasihi, wanafunzi hujifunza jinsi ya kueleza hisia zao na maoni yao kwa ufasaha. Hivyo, mimi ninaona kwamba fasihi andishi ina nafasi muhimu katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wangu (M1).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na data zilizopo kwenye dondoo hili, tunaona kwamba, fasihi andishi inawasaidia wanafunzi kuwasilisha mawazo yao bila wasiwasi. Kupitia kazi za fasihi, wanafunzi wanaweza kujifunza jinsi ya kueleza hisia zao na maoni yao kwa ufasaha na bila kizuizi cha kutokuwa na ujasiri. Pia, mwalimu mwingine alibainisha nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika dondoo hili:

> Nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano ni kukuza ujasiri wa wanafunzi. Mbinu za kusimulia hadithi fupi na uigizaji wa tamthilia zinajenga ujasiri wa wanafunzi katika kujieleza mbele ya wengine. Wanapopata uzoefu wa kujifunza na kushiriki katika tamthilia au hadithi, wanafunzi wanajenga ujasiri na uwezo wa kujieleza kwa ufasaha katika lugha ya Kiswahili (M5).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na data zilizopo kwenye dondoo hili, tunaona kwamba, mbinu za kusimulia hadithi fupi andishi na uigizaji wa tamthilia zina nafasi kubwa katika kujenga ujasiri wa wanafunzi katika kujieleza. Kwa kujihusisha na kazi za fasihi andishi kama hizo, wanafunzi hupata fursa ya kujifunza na kushiriki kwa uwazi, hivyo kuongeza uwezo wao wa kujieleza kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Hata kama maandiko yanasema kwamba fasihi andishi ina nafasi katika kukusa stadi za mawasiliano, hali halisi iliyopo kwenye shule za sekondari teule wilayani Nyanza ni kwamba fasihi andishi haijakuwa na nafasi katika ukuzaji wa stadi ya ujasiri. Walimu wa fasihi wanapofundisha, wanasisitizia zaidi tanzu za fasihi andishi na kusahau kuhusisha ukuzaji wa stadi za mawasilinao.

Zaidi ya hayo, walimu hawahusishi ukuzaji wa stadi za mawasiliano ikiwemo ujasiri katika maandarizi ya masomo. Hata na wale wanaojaribu kuhusisha stadi za mawasiliano hawaelewi maana ya mawasiliano. Miongoni mwa walimu wote walioshuhudiwa, hakuna yeyote ambaye alihusisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano ikiwemo ujasiri katika sehemu ya *Malengo ya Ujifunzaji*.

Mmoja kati yao alijaribu kuhusisha ukuzaji wa stadi husika kwenye sehemu ya *Uwezo wa Jumla na Masuala Mtambuka*. Licha ya hayo, maelezo yaliyotolewa na mwalimu husika hayakuendana na stadi za mawasiliano kama inavyoonekana kwenye andalio la somo la hapo chini.

**Kielelezo 2: Mfano wa Andalio la Somo**

| Muhula: | Tarehe: | Somo: | Kidato: | Mada: | Somo la: | Muda: | Idadi ya Wanafunzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| wa tatu | 6/6/2024 | KISWAHILI | 6LFK | I... | I.. katika .5.. | Dakika ..40 | 23/25 |

| | |
|---|---|
| Aina ya wanafunzi wenye mahitaji ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao | Mwanafunzi mmoja mwenye ulemavu wa viungo vya mwili |
| Mada | Fasihi katika Kiswahili |
| Uwezo Upatikanaoo Katika somo | Mwanafunzi awe ze kuelewa tanzu tofauti za fasihi andishi katika Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa na kuitumia kama mojawapo ya njia za kujitegemea maisha[illegible] |
| Somo Lenyewe | Tanzu za Fasihi Andishi |
| Malengo ya Kujifunza | Kufikia mwisho wa funzo. mwanafunzi awe ze;<br>i) Kutofautisha kwa usahihi tanzu ya fasihi andishi<br>ii) Kutambua kwa urahisi maana ya msamiati unaohusiana na tanzu za fasihi andishi |
| Mahali ambapo somo litafundishiwa | Darasani |
| Vifaa au zana kwa wanafunzi wote | Vitabu vya Kiswahili, nyaraka mbalimbali za fasihi, kamusi na mtandao |
| Vitabu vya rejelea | Kitabu cha Kiswahili 6, Kiswahili kwa shule za Rwanda 6, Kitabu cha malimu, Kigali & Kamusi ya Kiswahili TUKI (2019). |

| Muda na hatua | Mbinu za Kufundisia na Kujifunzia | | Uwezo wa Jumla na Maswala Mtambuka + Maelezo Mafupi |
|---|---|---|---|
| | Kwa kutumia vifungu vya habari tofauti, malimu atawawezesha wanafunzi kutofautisha kwa usahihi tanzu za fasihi andishi, kutambua kwa urahisi maana ya msamiati unaohusana na tanzu za fasihi andishi. | | |
| | **Majukumu ya Mwalimu** | **Majukumu ya Mwanafunzi** | |
| Utangulizi Dakika. .5.... | Kusalimia na kuuliza maswali tanguliżi yo kuwaingiza wanafunzi kwenye somo | Kusalimu mwalimu na kujibu maswali | Stadi za utafiti (kupitia kusoma na kujibu maswali. wanafunzi watakuza uwezo wa utafiti) |
| Somo lenyewe<br>Dakika .25. | Kuwaingiza wanafunzi kwenye soma kifungu na kujibu maswali yanayoendana na kifungu<br>Kufuata kuwa kazi inafanyika makundini<br>Kutoa msaada panapohitajika na kuomba wanafunzi kuwasilisha kazi walizozi- [illegible] fanya.<br>kufupisha somo. | Kujibu maswali na kufuata<br>Kukaa kwa makundi ya wanafunzi watano, kusoma kifungu na kujibu maswali yanayoendana na kifungu<br>Kufanya kazi kuomba msaada panapohitajika na kuwasilisho kazi zao.<br>Kushirikiana na mwalimu katika ufupishaji wa somo | mawasiliano (kwa kufanya kazi za makundi, wanafunzi watakuza stadi za mawasiliano kwa kuchangia majukumu.)<br>Elimu ya amani na maadili (kupitia usomaji wa kifungu cha habari, wanafunzi watalelewa elimu ya amani na watakuza maadili yao.) |
| Hitimisho Dakika .10.. | Kutathmini kiwa malengo ya kujifunza yametimizwa | Kufanya tathmini. | |
| Tathmini ya mwalimu | Somo limefundishwa vizuri | | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2024)

Kutokana na andalio hili la somo, tunaona kwamba mwalimu hakuhusisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika malengo ya ujifunzaji. Ingawaje, mwalimu husika alihusisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika andalio la somo lake (kwenye sehemu ya *Uwezo wa Jumla na Maswala Mtambuka*), maelezo aliyoyatoa hayahusiani na stadi za mawasiliano. Mwalimu huyu aliandika, "Mawasiliano (kwa kufanya kazi za makundi, wanafunzi watakuza stadi za mawasiliano kwa kuchangia majukumu)." Unapochunguza vizuri, unaona kwamba mwalimu huyu haelewi vizuri stadi za mawasiliano. Hii ni kwa sababu maelezo aliyoyatoa yanahusiana na stadi ya ushirikiano. Hii ilitoa athari mbaya katika mchakato wa ukuzaji wa stadi za mawasiliano kupitia ufundishaji wa fasihi andishi katika Kiswahili. Kwa kuchanganya stadi za mawasiliano na stadi ya ushirikiano, mwalimu husika hakufanikiwa kukuza stadi za mawasiliano kwa ufasaha miongoni mwa wanafunzi.

Hata kama Ilankumaran & Deepa (whj, uk.622) wanasema kwamba kupitia uwasilishaji wa mashairi, wanafunzi wanakuza ujasiri, hali hii haijafanikiwa katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Wakati wa ushuhudiaji ilionekana kwamba, walimu wanapofundisha fasihi andishi, wanakabiliwa na changamoto ya muda mdogo kiasi kwamba, wanafunzi hawapewi nafasi ya kushiriki katika ufundishaji na ujifunzaji kupitia uwasilishaji. Changamoto hii inawanyima wanafunzi fursa ya kukuza stadi yao ya ujasiri. Pia, mahojiano na walimu yalionesha kwamba wanapokuza stadi za mawasiliano kupitia ufundishaji wa fasihi, wanakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa muda. Dondoo la hapo chini linaonesha taarifa zilizotolewa na mshiriki wa utafiti mmoja:

> Changamoto inayonikabili ninapotumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili ni muda wa kufundisha ambao hautoshi. Ratiba yangu ina masomo mengi na muda unaotengwa kwa ajili ya somo la fasihi andishi ni mdogo. Kwa hiyo, ni kutekeleza mikakati ya ukuzaji wa stadi za mawasiliano kama vile mijadala, maigizo na majadiliano ya kina. Hii inanifanya nijikite zaidi katika kufundisha stadi za kusoma na kuandika pekee (M3).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na data zilizopo kwenye dondoo hili, tunaona kwamba, changamoto anayokabiliana nayo ni muda wa kufundisha ambao hautoshi. Ratiba ya masomo ina upungufu wa muda unaotengwa kwa ajili ya somo la fasihi andishi, hali inayofanya iwe vigumu kwa mwalimu

kutekeleza mbinu za ukuzaji wa stadi za mawasiliano. Kwa hiyo, anajikita zaidi katika kufundisha stadi za kusoma na kuandika pekee, na hivyo kushindwa kukuza stadi za mawasiliano kwa upana na ukamilifu wake. Isitoshe, licha nadharia ya mawasiliano kuonesha kwamba mawasiliano ni mchakato ulio imara ambao una sheria zilizowekwa ambazo zinafaa kufuatwa, ufupi wa muda wa kufundisha fasihi unawazuia walimu kuwezesha wanafunzi kumudu sharia zinazohitajika katika mchakato wa mawasiliano. Kwa hiyo, walimu wanalazimia kutumia muda wa ziada ili kila mwanafunzi apate nafasi ya kujieleza mbele ya wenzake kwa ajili ya kukuza stadi ya ujasiri.

Hivyo basi, matokeo ya utafiti uliofanyika yanaonesha kwamba walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza hawahusishi kwa ufasaha ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika maandalio ya masomo ya fasihi andishi katika Kiswahili. Jambo hili huathiri vibaya ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi.

### 4.2.4 Fasihi Andishi katika Kukuza Stadi ya Utambuzi wa Hisia

Utambuzi wa hisia ni uwezo wa kuelewa, kutambua na kuhisi hisia za watu wengine. Stadi hii inahusisha uwezo wa kutambua namna ambavyo mtu mwingine anajihisi au kuelewa hali ya mtu mwingine ya kihisia, hata bila ya kusemwa wazi (Valente, 2016, uk.12). Stadi hii ni muhimu katika mawasiliano kwa kuwa inamwezesha mtu kuelewa na kujibu hisia za wengine kwa ufasaha, hivyo kuboresha mawasiliano yenye ufanisi. Kwa hiyo, sehemu hii inahusisha tathmini ya nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi ya utambuzi wa hisia. Baadhi ya matini za kitaaluma zilizochanganuliwa zimeonesha kwamba fasihi andishi inaweza kukuza utambuzi wa hisia kwa wanafunzi. Dondoo hili linaeleza ifuatavyo:

> Literary texts provide students with opportunities to understand and learn about the emotions of characters through detailed writing and narration. By reading and analyzing literary works, students gain the ability to recognize and empathize with the emotional states of characters, thereby improving their emotional awareness.
> **Chanzo**: Valente (2016, uk.15)
>
> Matini za fasihi hutoa nafasi kwa wanafunzi kuelewa na kujifunza kuhusu hisia za wahusika kupitia uandishi wa kina na usimulizi. Kwa kusoma na kuchanganua kazi za fasihi, wanafunzi wanapata uwezo wa kutambua na kuhisi hali za kihisia za wahusika, hivyo kuboresha utambuzi wao wa hisia. (T.Y)

Kulingana na dondoo hili, matini za fasihi husaidia wanafunzi kuelewa na kujifunza kuhusu hisia za wahusika kupitia uandishi wa kina. Hii inawasaidia wanafunzi kuboresha utambuzi wao wa hisia kwa kutambua na kuhisi hali za kihisia za wahusika. Aidha, Johnson (2018) anabainisha nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa stadi ya utambuzi wa hisia kwenye dondoo lifuatalo:

> Literature develops empathy among students. Literature conveys emotions and emotional states through various writing techniques, helping students identify and comprehend the feelings of characters. This enables students to develop their emotional awareness and engage more deeply in emotional communication.
> **Chanzo**: Johnson (2018, uk.22)
>
> Fasihi inakua huruma miongoni mwa wanafunzi. Fasihi inawasilisha hisia na hali za kihisia kupitia mbinu mbalimbali za uandishi, ikisaidia wanafunzi kutambua na kuelewa hisia za wahusika. Hii inawasaidia wanafunzi kukuza utambuzi wao wa kihisia na kushiriki kwa kina katika mawasiliano ya kihisia. (T.Y)

Kulingana na dondoo hili, fasihi inasaidia wanafunzi kukuza huruma kwa kuelewa hisia za wahusika kupitia mbinu mbalimbali za uandishi. Hii inawawezesha wanafunzi kuboresha utambuzi wao wa kihisia na kushiriki zaidi katika mawasiliano ya kihisia. Hii inaonesha kwamba fasihi andishi inakuza uwezo wa utambuzi wa hisia miongoni mwa wanafunzi. Licha ya haya, katika muktadha wa shule teule wilayani Nyanza, fasihi andishi haijatumiwa kwa ufasha kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Hii ni kwa sababu, taarifa tulizozipata kutoka kwa walimu kuhusu stadi za mawasiliano hakuna hata mmoja aliyegusia stadi ya utambuzi wa hisia. Hii inatoka na uelewa mdogo wa walimu kuhusu stadi za mawasilano.

Katika ushuhudiaji, tuliona kwamba mwalimu mmoja alihusisha stadi ya utambuzi wa hisia katika ufundishaji wake bila kujua. Mwalimu huyu alitumia mbinu za majadiliano na usimulizi katika darasa lake, ambapo wanafunzi walikuwa wanashiriki mawazo na hisia zao kuhusu wahusika wa hadithi walizokuwa wakisoma. Ingawaje mwalimu hakueleza moja kwa moja umuhimu wa utambuzi wa hisia, matumizi haya ya mbinu za kuzungumza na kubadilishana mawazo yalihusiana kwa karibu na kukuza uwezo wa wanafunzi kuelewa na kuhisi hisia za wahusika.

Aidha, mwalimu huyu alitumia mifano ya hali za kihisia kutoka kwa wahusika wa fasihi andishi ili kuamsha hisia za wanafunzi na kuwafanya waelewe hali za kihisia kwa kina. Katika hatua hii, ingawa mwalimu alilenga zaidi maelezo ya kimaudhui, matumizi haya ya mifano yalisaidia

wanafunzi kubaini na kuelewa hisia za wahusika, hivyo kukuza utambuzi wao wa kihisia bila mwalimu kujua.

Kwa hiyo, walimu wanafaa kufanya juhudi za makusudi ili kuendeleza ufahamu wao kuhusu stadi zote za mawasiliano, ikiwemo utambuzi wa hisia. Hii ni kwa sababu, kuelewa na kufundisha stadi hizi kwa kina kutasaidia wanafunzi kuboresha mawasiliano yao na kukuza hisia zao kwa usahihi.

## 4.3 Miongozo ya Utumiaji wa Ufundishaji wa Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano

Lengo mahususi la pili lautafiti lilikuwa kuunda miongozo ya kutumia fasihi andishi kukuza stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Ili kufikia lengo hili, mtafiti alichanganua matini mbalimbali kuhusu mwongozo wa kukuza stadi za mawasiliano kupitia ufundishaji wa fasihi. Zaidi ya hayo, mtafiti alifuata mhimili wa tatu wa nadharia ya mawasiliano, ambao unasisitiza kwamba mawasiliano hujengwa upya kila wakati watu wanapotafsiri ujumbe na kufikia maoni yao binafsi. Isitoshe, katika sehemu hii, utafiti uliofanyika umetoa miongozo ya utumiaji wa kazi ya fasihi andishi (Tamthilia: *Nguzo Mama* ya Penina Mahando) katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

### 4.3.1 Utumiaji wa Mbinu za Ufundishaji wa Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano

Sehemu hii inalenga kutoa miongozo ya kutumia fasihi andishi kukuza stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Hapa utafiti uliofanyika, unaonesha miongozo ya utumiaji wa mbinu tatu ambazo ni pamoja na: utumiaji wa mbinu ya mawasiliano ya mtu moja kwa mwingine, utumiaji wa mbinu ya uumbaji wa mazingira salama ya kujifunzia na uhusiano wenye msaada na utumiaji wa mbinu ya kusikiliza kwa makini.

#### 4.3.1.1 Utumiaji wa Mbinu ya Mawasiliano ya Mtu Moja kwa Mwingine

Katika utafiti uliofanyika, tuliamua kutoa mwongozo wa utumiaji wa mbinu ya mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine kama njia ya utumiaji wa fasihi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Kwa mujibu wa Rosalyn (2020),

mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine ni mbinu bora ya ukuzaji wa stadi za mawasiliano ambapo mtu hufundishwa kuwasiliana akiwa pamoja na mtu mwingine mmoja. Mbinu hii imebainika kuwa muhimu sana katika kujenga mahusiano na uelewa kati ya watu. Hii ni kwa sababu, mazungumzo ya karibu yanaruhusu uelewa wa kina zaidi kwa kutazama lugha ya mwili, njia fasaha za mawasiliano na ishara za kuonekana. Hii ina maana kwamba mbinu hii ni bora katika kujifunza na kufundisha jinsi ya kufanya mawasiliano kwa ufanisi katika lugha ya Kiswahili.

Mbinu ya mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine inaweza kushiriki katika utumiaji wa fasihi andishi kwa njia nyingi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Kwanza, mbinu hii inaweza kutumika wakati wa kujadili kazi za fasihi kama vile riwaya, hadithi fupi na mashairi ambapo mwanafunzi mmoja anamwelezea mwingine maudhui, wahusika na muktadha wa kazi hiyo. Mazungumzo haya ya ana kwa ana yatasaidia wanafunzi kuelewa kwa undani zaidi na kushirikiana mawazo yao kwa uhuru. Pili, mbinu hii inaweza kutumika katika mazoezi ya kuigiza dondoo za fasihi andishi ambapo wanafunzi wawili wanachukua majukumu ya wahusika na kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Hii itawasaidia wanafunzi kuboresha ustadi wao wa mawasiliano kupitia maingiliano halisi yanayotokana na maandiko ya fasihi.

Tatu, walimu wanaweza kutumia mbinu hii kwa kuanzisha mijadala ya kina kuhusu masuala yanayojitokeza katika fasihi, na hivyo kuwahamasisha wanafunzi kuelezea maoni yao na kujenga hoja kwa ufasaha. Kwa njia hizi, mbinu ya mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine inaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa Kiswahili kupitia utumiaji wa fasihi andishi.

Katika utekelezaji wa utumiaji wa mbinu ya mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine, walimu wa fasihi andishi kwa Kiswahili wanalazimika kufuata hatua nne. Kwanza, walimu wanapaswa kuanzisha mazungumzo ya awali na wanafunzi wao ili kujenga uhusiano wa kuaminiana.

Hii inaweza kufanyika kwa kupanga vipindi vya mazungumzo ambapo walimu wanaweza kuwasikiliza wanafunzi wao na kujua changamoto wanazokabiliana nazo katika kujifunza fasihi andishi. Katika hatua hii, walimu wanapaswa kuonesha utayari wa kusikiliza na kutokuhukumu wanafunzi kwa kufafanya wajisikie huru na salama kushiriki mawazo na hisia zao.

Pili, baada ya kuanzisha mazungumzo ya awali, walimu wanapaswa kuweka malengo mahususi ya mawasiliano ambayo wanafunzi wanatarajiwa kufikia. Malengo haya yanaweza kujumuisha na kuboresha ufasaha katika lugha ya Kiswahili, kusikiliza kwa makini, kuongeza ujasiri wa kujieleza mbele ya wengine, kukuza stadi za mawasiliano yasiyo ya maneno na kukuza uwezo wa wanafunzi wa kuchambua na kueleza maudhui ya kazi za fasihi andishi. Malengo haya yanapaswa kuwa wazi na kutumia vitenzi tendaji vinavyoweza kupimika.

Tatu, walimu wanapaswa kutumia mazoezi ya kivitendo ili kuwasaidia wanafunzi kukuza stadi zao za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Hii inaweza kujumuisha kuigiza tamthilia, kusimulia hadithi fupi, kukariri mashairi na kufanya mazungumzo ya kina kuhusu maudhui ya fasihi andishi wanayojifunza. Kwa mfano, mwalimu anaweza kumuomba mwanafunzi aelezee hadithi fulani au kuigiza kipande cha tamthilia mbele ya darasa au katika mazingira ya faragha. Hii itawasaidia wanafunzi kujifunza jinsi ya kutumia lugha kwa ufasaha na kujenga ujasiri wa kuwasilisha mawazo yao kwa wengine.

Katika hatua ya mwisho, walimu wanapaswa kutoa mrejesho jengaji kwa wanafunzi. Mrejesho huu unapaswa kuwa wa kweli na unaoelezea wazi maeneo ambayo mwanafunzi amefanya vizuri na yale yanayohitaji kuboreshwa. Walimu wanapaswa kuonesha maeneo ya uboreshaji kwa njia inayowatia moyo wanafunzi na kuwasaidia kuelewa jinsi ya kuboresha stadi zao za mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mwalimu anaweza kumwambia mwanafunzi kuwa ameonesha ufasaha mzuri katika kusimulia hadithi, lakini anahitaji kufanya kazi zaidi katika kutumia lugha ya mwili ili kuelezea hisia zake kwa ufanisi zaidi.

Hivyo basi, kwa kufuata hatua hizi nne, walimu wa fasihi andishi ya Kiswahili wataweza kutumia mbinu ya mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine kwa ufanisi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wao.

Mbinu hii itawasaidia wanafunzi kujifunza jinsi ya kuwasilisha mawazo yao kwa ujasiri na ufasaha, huku wakizingatia muktadha wa kijamii na kitamaduni wa lugha ya Kiswahili. Utumiaji wa mbinu hii unaendana na wazo la nadharia ya mawasiliano kwamba mawasiliano ni mchakato wa kusambaza habari kutoka kwa mtumaji kwenda kwa mpokeaji ambaye kisha huifafanua na kuchukua hatua kulingana na ujumbe alioupokea. Wakati mpokeaji anashindwa kufafanua ujumbe kutokana na sababu mbalimbali, mchakato wa mawasiliano hauwezi kuwa na mafanikio.

Hivyo basi, kwa kutumia mbinu ya mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine, walimu wa fasihi andishi ya Kiswahili watahakikisha kuwa ujumbe unafafanuliwa kwa usahihi na wanafunzi. Pia, wataboresha ufanisi wa mawasiliano kwa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wao kupitia ufundishaji wa fasihi andishi.

#### 4.3.1.2 Utumiaji wa Mbinu ya Kujenga Mazingira Salama na Uhusiano Msaada katika Kujifunza

Mazingira ya kujifunzia ni kitu muhimu katika ufundishaji wa somo lolote lile. Kutokana na wazo hilo, utafiti uliofanyika, umetoa mwongozo wa utumiaji wa mbinu ya uumbaji wa mazingira salama ya kujifunza pamoja na uhusiano wenye msaada kati ya walimu na wanafunzi. Ukosefu wa uhusiano wenye msaada kati ya wanafunzi na walimu huzuia kufikia malengo ya kufundisha na kujifunza.

Hivyo basi, ili kuboresha stadi za mawasiliano kati ya wanafunzi, walimu wanapaswa kuunda mazingira salama ya kujifunza ambayo yanazingatia uhusiano wenye msaada. Mazingira haya yanajengwa kwa kuweka mikakati ambayo inawafanya wanafunzi wajisikie huru na kuheshimiwa, huku walimu wakionesha utayari wa kusikiliza na kutokuhukumu (O'Connor & McCartney, 2007, uk.51). Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wanapata ujasiri wa kuwasilisha mawazo yao kwa uhuru na ufasaha, na hivyo kuimarisha mawasiliano na kujifunza kwa ufanisi zaidi.

Aidha, mbinu ya uumbaji wa mazingira salama ya kujifunzia na uhusiano wenye msaada inaweza kuchangia sana katika utumiaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Kwa kuunda mazingira yanayoheshimu na kusaidia uhusiano bora kati ya walimu na wanafunzi, wanafunzi wanajenga ujasiri wa kujieleza kwa uhuru na ufasaha.

Jambo hili ni muhimu sana katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano. Wanafunzi wakiwa katika mazingira salama, wanaweza kujifunza jinsi ya kueleza mawazo yao kwa uwazi zaidi, kuchambua maudhui ya fasihi andishi kwa kina na kushiriki kikamilifu katika majadiliano yanayohusu kazi za fasihi andishi. Hii husaidia kuimarisha uwezo wao wa kuelewa, kufikiri kwa kina na kujieleza kwa ufasaha ambao ni muhimu katika stadi za mawasiliano katika Kiswahili.

Hivyo, mbinu hii inachangia sana katika kuleta maendeleo ya mawasiliano kwa Kiwashili kupitia ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi andishi.

Katika utekelezaji wa mbinu husika, walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari wanaweza kuuata hatua zifuatazo. Mosi, walimu wanaweza kuanza kwa kuunda mazingira ambayo wanafunzi wanajisikia salama na kuheshimiwa. Hii inaweza kufanyika kwa kuanzisha sheria za darasa zinazopendeleza ushirikiano na heshima kati ya wanafunzi na kati ya wanafunzi na walimu. Hapa, walimu wanalazimika kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata nafasi ya kujieleza bila hofu ya kudharauliwa. Kuweka mazingira ya urafiki na kujali ni hatua muhimu katika kujenga uhusiano wenye msaada.

Pili, walimu wanaweza kutumia mbinu za kufundisha ambazo zinaweka msisitizo kwenye mazoezi ya kivitendo. Hii inaweza kujumuisha vipindi vya kuigiza, usomaji wa hadithi fupi kwa sauti na majadiliano ya vikundi vidogo.

Kwa mfano, walimu wanaweza kugawa wanafunzi katika makundi madogo na kuwaomba kusimulia hadithi fupi andishi wanazopenda au kujadili maudhui ya tamthilia waliyoisoma. Mbinu hizi za kivitendo zitawasaidia wanafunzi kukuza ujasiri na ufasaha katika matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Hatua ya tatu inalenga kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anashiriki kikamilifu katika kazi zilizotolewa. Hii inajumuisha kutoa msaada unaohitajika kwa wanafunzi ili kuondoa vizuizi vinavyoweza kujitokeza. Kwa mfano, walimu wanaweza kutoa miongozo zaidi au mazoezi ya ziada kwa wanafunzi wanaohitaji msaada zaidi. Kupitia msaada huu, lengo ni kuhakikisha kuwa kila mmoja ananufaika na mchakato wa kujifunza kulingana na uwezo na mahitaji yake binafsi

Hatua ya nne inahusisha kutathmini kwa kina ubora wa mbinu zilizotumiwa. Hii inajumuisha kuangalia matokeo ya wanafunzi, ushiriki wao katika mchakato wa kujifunza, na maoni yao. Kwa kuzingatia tathmini hii, walimu wanaweza kuamua ni mbinu zinazofaa kutumiwa na zile zinazopaswa kurekebisha au kuboreshwa.

Hatua hii ya tathmini inalenga kuhakikisha kuwa mbinu zinazotumiwa zinafaa kwa kuleta mazingira salama yenye uhusiano wenye msaada, na kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata fursa za kujifunza na kuendeleza stadi zao za mawasiliano kwa Kiswahili.

Kwa hiyo, mbinu ya uumbaji wa mazingira salama ya kujifunza na uhusiano wenye msaada ni muhimu sana katika utumiaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari. Kwa kufuata mwongozo uliowekwa na kuzingatia ushiriki wa wanafunzi na tathmini ya matokeo, walimu wanaweza kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata fursa ya kujifunza kwa ufanisi. Pia, wanaweza kuendeleza uwezo wa kuelewa na kueleza mawazo kwa ufasaha. Hii inaimarisha mawasiliano na inachochea maendeleo ya kujifunza na ufahamu wa fasihi andishi, ikichangia katika kuimarisha elimu na ujuzi wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi.

Mbinu hii inaendana na mhimili wa pili wa Nadharia ya Mawasiliano kwamba mawasiliano ni msingi wa mafanikio katika kujifunza, na hivyo mazingira salama na uhusiano wenye msaada ni mambo muhimu katika kufanikisha malengo ya ufundishaji na ujifunzaji.

#### 4.3.1.3 Utumiaji wa Mbinu ya Kusikiliza kwa Makini

Mhimili wa tatu wa Nadharia ya Mawasiliano unasisitiza kuwa mawasiliano yanachukuliwa kama ujumbe tofauti na unaoundwa na kuundwa upya wakati watu tofauti wanapotafsiri ujumbe na kufikia hitimisho lao wenyewe. Hii ina maana kwamba, ili mtu aweze kupokea na kutafsiri ujumbe, ni lazima awe na uwezo wa kusikiliza kwa makini.

Kwa hiyo, utafiti uliofanyika, ulitoa mwongozo wa utumiaji wa mbinu ya kusikiliza kwa makini kama mojawapo ya mbinu za utumiaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

Umuhimu wa kusikiliza kwa makini ni msingi wa mawasiliano yenye ufanisi na uelewa wa kweli. Curuso, Colombi & Tebbit (2017, uk.70) wanasema kwamba zaidi ya asilimia 60 ya matatizo ya kutoelewana hutokana na usikilizaji duni. Kwa hiyo, kuzingatia na kukuza uwezo wa kusikiliza kwa makini miongoni mwa wanafunzi ni muhimu sana katika kuendeleza stadi zao za mawasiliano na kujenga uelewa imara.

Mbinu ya kusikiliza kwa makini inachangia pakubwa katika utumiaji wa fasihi andishi kwa kukuza stadi za mawasiliano kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Kwa kusikiliza kwa makini wakati wa kujadili kazi za fasihi, wanafunzi wanapata fursa ya kuelewa kwa kina mawazo na hisia zilizopokatika kazi hizo. Hii inawasaidia kuelewa vizuri yaliyomo, na

kuboresha uwezo wao wa kujieleza kwa ufasaha. Kusikiliza kwa makini kunawawezesha wanafunzi kujifunza namna ya kutafsiri na kuchambua maandiko ya fasihi, hivyo kujenga uwezo wa kufikiri kwa kina na kuwasiliana kwa weledi. Hivyo, mbinu hii ni nyenzo muhimu katika kukuza stadi za mawasiliano katika Kiswahili miongoni mwa wanafunzi.

Katika utekelezaji wa utumiaji wa mbinu hii, walimu wa fasihi katika Kiswahili wanaweza kufuata taratibu zifuatazo. Kwanza, walimu wa fasihi andishi wanaweza kuanza kwa kuunda mazingira ya darasa ambayo yanazingatia umuhimu wa usikilizaji kwa makini. Hii inaweza kufanywa kwa kutoa maagizo ya wazi kwa wanafunzi kuhusu sheria na matarajio ya usikilizaji darasani.

Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwaelezea wanafunzi kwamba wakati wa mjadala au usomaji wa pamoja, wanapaswa kusikiliza kwa makini na kutofanya shughuli nyingine kama vile kuandika au kuzungumza na wenzao. Hii inaweza kusaidia wanafunzi kuelewa umuhimu wa kusikiliza kwa umakini.

Pili, walimu wanaweza kutoa mazoezi maalum ya usikilizaji kwa makini ambayo yanawahusisha wanafunzi katika kusikiliza kwa umakini. Kwa mfano, walimu wanaweza kuandaa vipindi vya kusoma hadithi ambapo wanafunzi wanahitajika kusikiliza kwa makini na kisha kueleza kwa ufupi hadithi hiyo kwa kutumia maneno yao wenyewe. Pia, walimu wanaweza kupanga mijadala ya vikundi ambapo wanafunzi wanahitajika kusikiliza hoja za wenzao na kisha kutoa maoni yao kwa kuzingatia yale waliyosikia. Mazoezi haya yanasaidia wanafunzi kukuza stadi zao za usikilizaji na kuelewa kwa kina.

Tatu, walimu wanafaa kuwafundisha wanafunzi jinsi ya kurudia na kuthibitisha maelezo waliyosikia ili kuhakikisha wameelewa vizuri. Hapa, walimu wanaweza kuwataka wanafunzi wao kurudia kile walichosikia kutoka kwa mwalimu au wenzao kwa maneno yao wenyewe. Kwa mfano, baada ya mwalimu kusoma sehemu ya hadithi, anaweza kuwauliza wanafunzi kurudia kwa ufupi kile walichosikia. Hii inawasaidia wanafunzi sio tu kuelewa vizuri balipia kujenga uwezo wa kueleza kwa usahihi maudhui waliyojifunza.

Mwisho, walimu wa fasihi andishi wanafaa kutumia mifano halisi ya maisha katika mazoezi ya usikilizaji kwa makini. Kwa mfano, walimu wanaweza kuleta hadithi za maisha ya watu maarufu

au matukio halisi yaliyotokea katika jamii na kuwaomba wanafunzi kusikiliza kwa makini na kisha kutoa maoni yao au kueleza jinsi wanavyoweza kutumia mafunzo hayo katika maisha yao ya kila siku. Hii inawasaidia wanafunzi kuona umuhimu wa kusikiliza kwa makini katika muktadha wa maisha yao na jinsi inavyoweza kuboresha stadi zao za mawasiliano na uelewa wa kijamii.

Kwa kufuata hatua hizi nne, walimu wa fasihi andishi wataweza kutumia mbinu ya usikilizaji kwa makini kwa ufanisi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wao. Hii itasaidia wanafunzi kujifunza jinsi ya kusikiliza kwa umakini, kuelewa na kuelezea maudhui kwa ufasaha, huku wakizingatia muktadha wa kijamii na kitamaduni wa lugha ya Kiswahili.

Mazingira ya kujifunza yanayozingatia usikilizaji kwa makini yatawajengea wanafunzi msingi imara wa stadi za mawasiliano na kuwaandaa vizuri kwa changamoto za mawasiliano katika maisha yao ya baadaye.

### 4.3.2 Mfano wa Kufundisha Fasihi Andishi kwa Mwongozo Unaokuza Stadi za Mawasliano

Sehemu hii inajikita katika mfano wa jinsi ya kutumia fasihi andishi katika kukuza stadi za mawasiliano kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule katika Wilaya ya Nyanza. Tulichagua tamthilia ya *Nguzo Mama* iliyoandikwa na Penina Muhando mwaka wa 2010, kama kielelezo cha ufundishaji. Kuna kazi za fasihi andishi nyingi ambazo zinaweza kutumiwa katika shule za sekondari nchini Rwanda. Licha ya hayo, katika utafiti tuliofanya, tulijikita hasa katika uchambuzi wa tamthilia *Nguzo Mama*, tukilenga kuonesha jinsi inavyoweza kufundishwa kwa lengo la kukuza stadi za mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili.

Pia, tamthilia inahusisha majadiliano ya kina na mijadala inayoweza kuchochea uelewa wa muktadha wa kijamii na kitamaduni, ikilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi andishi.

Tamthilia ya *Nguzo Mama* ilichaguliwa miongoni mwa nyingine kwa sababu inatoa mchango mkubwa katika kukuza stadi za mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa sekondari. Kwanza, tamthilia hii ina lugha rahisi na inayoweza kueleweka kwa urahisi na wanafunzi, hivyo kuwawezesha wanafunzi kuijadili kwa kina na kwa ufasaha. Pili, *Nguzo Mama* inagusia masuala ya kijamii yanayohusiana na mazingira ya wanafunzi ya kila siku, jambo

ambalo linawapa fursa ya kujadili mada zinazowagusa moja kwa moja na hivyo kuboresha uwezo wao wa kujieleza.

Aidha, kupitia wahusika wake na matukio yaliyo katika tamthilia, wanafunzi wanapata nafasi ya kujifunza mbinu za mawasiliano kama vile jinsi ya kutoa hoja, kujibu hoja na kushiriki katika mijadala. Hali kadhalika, tamthilia hii ina mazungumzo yenye msisimko na ambayo yanahusisha mijadala ya pande mbili au zaidi, jambo linalowawezesha wanafunzi kuboresha stadi zao za kusikiliza kwa makini na kujibu kwa usahihi. Vilevile, matumizi ya msamiati mbalimbali na miundo ya sentensi katika tamthilia hii yanaweza kuwasaidia wanafunzi kupanua wigo wao wa lugha na kuboresha uwezo wao wa kuandika.

#### 4.3.2.1 Mfano wa Kufundisha Fasihi Andishi kwa Njia Inayokuza Stadi za Mawasiliano ya Maneno

Sehemu hii inaonesha hatua kwa hatu namna ya kutumia Tamthilia ya *Nguzo Mama* ili kukuza stadi za mawasiliano ya maneno kwa wanafunzi wa madarasa ya Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Tamthilia ya *Nguzo Mama* ya Penina ilionekana kama hazina ya mafunzo kwa walimu wa Kiswahili wanaotaka kufundisha stadi za mawasiliano ya maneno kwa wanafunzi wao wa katika shule za sekondari. Tamthilia hii inatoa mifano halisi ya jinsi watu wanavyotumia lugha katika hali mbalimbali, na inaweza kutumika kuwafundisha wanafunzi kuhusu vipengele vyote vya mawasiliano ya maneno.

Kwanza, tamthilia ya *Nguzo Mama* ni kazi ya fasihi andishi ambayo inaweza kutumiwa na walimu wa Kiswahili ili kukuza stadi za kusoma na kuandika ambazo ni stadi muhimu za mawasiliano. Katika onesho la pili, Bi Nane aliitwa na Mwenyekiti na akapewa barua ambayo ilikuwa inaeleza shtaka aliloshitakiwa. Bi Nane alikuwa anashitakiwa na Bi Nne kwa kuanzisha kikundi cha kupinga juhudi za kusimamisha *Nguzo Mama*. Wazo hili linathibitishwa na dondoo lifuatalo:

> Lahaula!
> Bi Nane kashangaa tena kashangaa!
> Yamekuwaje mambo haya!
> Hakujua maskini kitu gani kaitiwa.
> Barua aliyopata kifupi ilisema
> Ofisini kwa Mwenyekiti saa tatu ufike.
> Kumbe ni yule wa zamani Bi Nne! (*Nguzo Mama*, uk.26)

Dondoo hili linaonesha kwamba Bi Nane aliandikiwa barua ya kumuelezea shtaka aliloshitakiwa. Kwa kuwa katika tamthilia hakuna barua hiyo, mwalimu anaweza kuwapatia wanafunzi zoezi la kuandika barua katika makundi ya watano watano kwa fikra zao. Zoezi hili linafaa kuchochea wanafunzi kushirikiana na kubadilishana mawazo juu ya jinsi ya kuandika barua rasmi ya kushitaki, jambo ambalo litawasaidia kujifunza mbinu mbalimbali za kuandika kwa usahihi na kwa mtindo rasmi.

Baadaye, mwalimu anaweza kuomba makundi kubadilishana barua walizoziandika. Kisha, kila kundi linafaa kusoma kwa makini barua iliyoandikwa na kundi jingine na kujibu barua hiyo.

Mwalimu anapokuwa na muda wa kutosha, baadhi ya makundi yanaweza kupewa nafasi ya kuwasilisha barua hizo mbele ya darasa. Shughuli kama hizi zikifanyika darasani, zinaweza kuwasaidia wanafunzi kukuza stadi za mawasiliano kwa upande wa kusoma na kuandika, kwa kuwa zitawapa fursa ya kujifunza kwa vitendo, kujadili na kutoa mrejesho kuhusu kazi za wenzao.

Aidha, tamthilia husika inaweza kutumiwa kufundishia kusoma na kuandika. Hili linaweza kufanyika kupitia hatua zifuatazo. Kwanza, mwalimu anaweza kuwashirikisha wanafunzi kusoma tamthilia nzima. Kisha, wanaweza kuandika muhtasari wa kila sura au sehemu muhimu.

Baada ya hapo, mwalimu anaweza kugawanywa wanafunzi katika makundi madogo na kushirikishana kazi zao na kuboresha maandishi yao kwa maoni ya wenzao. Zoezi hili linasaidia wanafunzi kufasiri na kuunda ujumbe mpya. Hili nijambo muhimu katika mawasiliano na linaendana na mhimili wa tatu wa Nadharia ya Mawasiliano, unaosisitiza kuwa mawasiliano ni ujumbe mpya unaotafsiriwa upya na watu mbalimbali. Pia, wanaweza kubuni na kujibu maswali kuhusu tamthilia kwa maandishi, hivyo kuboresha uelewa wao na stadi za usomaji na uandishi bora.

Pili, tamthilia ya *Nguzo Mama* inaweza kutumiwa na walimu wa Kiswahili ili kukuza stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi. Katika onesho la pili, Bi Tano alienda kuuza vitambaa. Kwa bahati mbaya, hakuna mtu yeyote aliyenunua kitambaa hata kimoja ingawaje hapo awali wateja walikuwa wakiviogombania. Alipoelezea wenzake tatizo alilokutana nalo, wao walimuelezea kwamba ndiye aliyesababisha wateja kutonunua vitambaa vyake. Bi Moja

alimwambia kwamba angewabembeleza wateja wake, wangenunua vitambaa vyake. Wazo hili la Bi Moja lilitetewa na Bi Tano kama inavyoonekana kwenye dondoo lifuatalo:

> BI NANE: Lakini kwa mni wakatae kununua hivi, mbona vile vya mwanzo walinunua?
> BI MOJA: Tena walikuwa wanavigombania.
> BITANO: (Amekasirika zaidi) Kila nilipokwenda wananiambia wameshanunua vya kutosha. Sasa mimi ningewalazimisha?
> BI MOJA: Biashara inataka kubembeleza eti.
> BI NNE: Eee. Unasema maneno matamu matamu. Basi hivihivi tu watu watanunua?
> BI TANO: Sasa chukueni muende mkauze wenyewe. (*Nguzo Mama*, uk. 23)

Walimu wa Kiswahili wanaweza kutumia tamthilia ya *Nguzo Mama* kufundisha umuhimu wa kuzungumza kwa kuigiza sehemu ambapo Bi Tano alishindwa kuuza vitambaa vyake kwa kutowabembeleza wateja. Kwa kutekeleza hili, hatua ya kwanza inaweza kuwa kuwagawanya wanafunzi katika makundi madogo ambapo mwanafunzi mmoja atachukua nafasi ya Bi Tano na wengine watakuwa wateja. Wanafunzi watapewa maelezo kwamba Bi Tano alishindwa kuuza vitambaa kwa sababu hakuzungumza kwa unyenyekevu na hakuwabembeleza wateja wake. Katika hatua hii, wanafunzi wataigiza hali hii kwa vitendo, ambapo Bi Tano atajaribu kuuza vitambaa bila kutumia maneno ya kuwashawishi wateja.

Baada ya igizo hilo, wanafunzi watajadili kwa nini Bi Tano alishindwa kuuza vitambaa vyake, na watapata kuelewa kuwa kutokuzungumza kwa unyenyekevu na ushawishi kulisababisha wateja kutojihusisha naye.

Hatua ya pili ni kuwapa wanafunzi zoezi jingine ambapo wanafunzi watagawanywa katika makundi mawili, moja likiwa na Bi Moja na lingine likiwa na Bi Nne, ambao watajaribu kuuza vitambaa kwa kuwabembeleza wateja. Wanafunzi watapata kuelewa jinsi Bi Moja na Bi Nne walivyofanikiwa kuuza vitambaa kwa kutumia maneno matamu na ya ushawishi.

Katika hatua hii, wanafunzi watatakiwa kuonesha jinsi ya kutumia lugha ya heshima, unyenyekevu na ushawishi katika mazungumzo yao na wateja. Mwishoni mwa igizo hili, mwalimu ataongoza mjadala darasani ambapo wanafunzi watajadili tofauti kati ya Bi Tano, ambaye hakuuza vitambaa na Bi Moja na Bi Nne, ambao walifanikiwa. Mjadala huu utasaidia wanafunzi kuelewa kwamba mawasiliano ni mchakato wa kusambaza habari kutoka kwa

mtumaji kwenda kwa mpokeaji, na kwamba mpokeaji anapaswa kufafanua na kuchukua hatua kulingana na ujumbe alioupokea. Kwa kutumia hatua hizi, wanafunzi watapata fursa ya kuboresha stadi zao za kuzungumza na kuelewa umuhimu wa mawasiliano mazuri katika kufanikisha malengo yao.

Aidha, mhimili wa pili wa Nadharia ya Mawasiliano unaonesha kuwa mawasiliano ni mchakato wa kusambaza habari kutoka kwa mtumaji kwenda kwa mpokeaji ambaye kisha huifafanua na kuchukua hatua kulingana na ujumbe alioupokea. Wakati mpokeaji anashindwa kufafanua ujumbe kutokana na sababu mbalimbali, mchakato wa mawasiliano hauwezi kuwa na mafanikio. Hii ina maana kwamba, ili mpokeaji aweze kufafanua ujumbe ni lazima ategе masikio ili aweze kusikia kwa maneno.

Wazo hili linathibitisha umuhimu wa kusikiliza kwa makini katika mawasiliano. Kwa hiyo, walimu wa Kiswahili wanaweza kukuza stadi ya kusikiliza kwa makini miongoni mwa wanafunzi wao kupitia ufundishaji wa tamthilia ya *Nguzo Mama*.

Katika onesho la pili, tunamwona Bi Nane akiitwa na Mwenyekiti akimweleza shtaka lake. Bi Nane alikaa kimya na kumsikiliza Mwenyekiti kwa makini. Baada ya kusikiliza shtaka kwa umakini, alifafanua ujumbe wa Mwenyekiti na kuuelewa vizuri. Aligundua kwamba alishitakiwa na Bi Nne ambaye alitaka kumharibia jina tu. Ingawa alikuwa kwenye matatizo, alipomaliza kusikiliza kwa makini na kutafakari kuhusu jambo aliloshitakiwa, alitabasamu. Alitaka kutukana lakini akajizuia kama inavyoonekana kwenye dondoo lifuatalo:

> MWENYEKITI: Bi Nane, umeitwa hapa kwa sababu habari zimefikishwa kwenye Kamati ya Mashauri na tunataka utupe maelezo kuhusu mambo fulani fulani.
> (Kimya).
> Kwa kifupi ni kwamba tumepata habari kwamba wewe umeanzisha kikundi cha kupinga juhudi za wenzetu hapa Patata za kusimamisha NGUZO MAMA. Tena kikundi hicho cha walimu watupu kinababagau wasio walimu. Tena kikundi hicho kimekuwa kikifanya mikutano kupanga njama za kuchafua juhudi za wenzenu.
> BI MSIMULIZI: Lahaula! Bi Nane kashangaa tena kashangaa! Yamekuwaje mambo haya! Hakujua maskini kitu gani kaitiwa. Barua aliyopata kifupi ilisema Ofisini kwa Mwenyekiti saa tatu ufike. Kumbe ni yule wa zamani Bi Nne!
> Ingawa yalikuwa mazito hayo yao mashtaka Kicheko kilimjia tabasamu hakuzuilia Haraka akafikiri Kitu gani niwajibu? Wajinga niwaambie uongo

> kunizulia. Nimtukane Bi Nne akome kunifuata? Upesi akajirudi moyoni akasema Jihadhari mwanakwetu makubwa sijizulie (*Nguzo Mama*,.uk25-26).

Dondoo hili linaonesha kwamba Bi Nane alifanikiwa kuelewa shtaka lililokuwa linamkabili kwa kumsikiliza Mwenyekiti kwa makini na kutafakari kabla ya kutoa majibu.

Alitumia muda wake kumsikiliza mtoa shtaka kwa makini, jambo ambalo lilimsaidia kufafanua ujumbe vizuri na kuchukua hatua stahiki. Hii inasisitiza umuhimu wa kusikiliza kwa makini katika mawasiliano, kwani kutoelewa vizuri ujumbe kunaweza kuleta mkanganyiko na hatua zisizofaa.

Kwa hiyo, walimu wa fasihi wanaweza kutumia tamthilia hii ili kukuza stadi za kusikiliza kwa makini kwa kufuata hatua zifuatazo: Kwanza walimu wanaweza kugawa wanafunzi katika vikundi vidogo na kuwapa nafasi ya kuigiza sehemu ya tamthilia hiyo. Kila mwanafunzi atapata nafasi ya kusikiliza na kuelewa majibu ya wenzake, jambo ambalo litawasaidia kuelewa umuhimu wa kusikiliza kwa makini.

Pili, walimu wanaweza kuendesha mijadala ya kina baada ya kuigiza ambapo wanafunzi watajadili jinsi kusikiliza kwa makini kulivyosaidia Bi Nane kufafanua shtaka lake vizuri. Katika mjadala huo, wanafunzi watajifunza na kuelewa zaidi umuhimu wa kusikiliza katika mawasiliano, hivyo kukuza stadi zao za kusikiliza kwa makini.

Hivyo basi, utafiti wetu unabainisha kuwa tamthilia *Nguzo Mama* ni zana muhimu kwa walimu wa Kiswahili katika kukuza stadi za mawasiliano ya maneno kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Kupitia tamthilia hii, wanafunzi wanapata mifano halisi ya matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali, jambo linalowajengea uwezo wa kuelewa na kutumia lugha kwa ufanisi. Njia za ufundishaji kama kuigiza, majadiliano na kazi za makundi zilionesha kama mbinu fasaha kwa walimu katika kuchochea maendeleo chanya ya stadi za mawasiliano kwa wanafunzi.

#### 4.3.2.2 Mfano wa Kufundisha Fasihi Andishi kwa Njia Inayokuza Stadi za Mawasiliano Yasiyo ya Maneno

Tamthilia ya *Nguzo Mama* ni tamthilia ambayo inaweza kutumiwa na walimu wa Kiswahili ili kukuza stadi za mawasiliano yasiyo ya maneno miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Kwanza kabisa, kupitia tamthilia hii, walimu wanaweza kukuza stadi za

lugha ya vitu katika mawasiliano. Kulingana na Pearson, Nelson, Paul, Titsworth & Hosek (2017:84), lugha ya vitu inahusisha elimu ya matumizi ya mavazi na vitu vingine kama kanuni za mawasiliano yasiyo ya maneno. Stadi hii inaendana na stadi nyingine za mawasiliano yasiyo ya maneno. Stadi ya kwanza ni mienendo ya mwili na lugha uso. Hii inajumuisha mkao, ishara na mienendo mingine ya mwili na lugha uso, inayojulikana kama kinesiki. Stadi ya pili ni mwonekano wa mwili. Stadi hii inajumuisha jinsi mtu alivyo na mvuto wa kimwili.

Kama inavyoelezwa na Pearson na wenzake (whj:84), stadi hizi tatu ni muhimu katika mawasiliano yasiyo ya maneno. Kwa hiyo, matokeo ya utafiti uliofanyika yanaonesha namna ambavyo tamthilia ya *Nguzo Mama* inavyoweza kutumiwa kwa kukuza stadi za mienendo ya mwili na lugha uso, mwonekano wa mwili, na lugha ya vitu.

Katikaonesho la kwanza, wanatuonesha wahusika ambao walifika jukwani kwa kujaribu kuinua NGUZO MAMA. Kila mhusika aliyefika jukwani, alikuwa anavaa mavazi ya kipekee ambayo yalikuwa yanatoa ujumbe kuhusu sifa za mhusika huyo na mahali anapotoka.

Aidha, kila mhusika alikuwa na mwondoko ambao unaashiria kuonesha tabia au sifa nyingine za mhusika huyo. Haya yanathibitishwa na dondoolifuatalo:

> Wakati wimbo unaendelea anaingia BIMOJA kwa miondoko ya ngoma ya Lelemama kufuatisha mapigo ya wimbo ambao huku anauimba. Amevaa kimwambao na ananata hasa. Anacheza kuelekea NGUZO MAMA. Anaingilia kati kuimbisha wimbo akielekea NGUZO MAMA (*Nguzo Mama*,.uk.1).

Kutokana na dondoo hili, tunaona kwamba mavazi, mwonekano, na mwondoko wa mhusika vina maana maalum katika tamthilia ya *Nguzo Mama.* Anaingia BIMOJA kwa miondoko ya ngoma ya Lelemama, akifuata mapigo ya wimbo huku akiimba, akionyesha utambulisho na hadhi yake kupitia mavazi ya kimwambao.

Mwondoko wake wa kucheza kuelekea NGUZO MAMA na kuimbisha wimbo unaashiria nia na malengo yake, huku ukionyesha uhusiano wake na NGUZO MAMA. Hii inaonesha jinsi mwili na mavazi vinavyotumika kuwasilisha ujumbe na tabia za mhusika bila maneno. Aidha, tunaoneshwa mhusika mwingine kwenye dondoo lifuatalo:

> Wakati wimbo unaendelea anaingia BI PILI kwa miondoko ya ngoma ya Kiduo huku akiimba wimbo. Amevaa kama mkulima wa bara. Anacheza Kiduo kuelekea NGUZO MAMA (*Nguzo Mama*., uk.2).

Dondoo hili linaonesha kwamba BI PILI anaingia kwa miondoko ya ngoma ya Kiduo huku akiimba, akiwa amevaa kama mkulima wa bara, na kucheza kuelekea NGUZO MAMA. Hii inaashiria kwamba mavazi yake yanaonyesha utambulisho wake kama mkulima. Miondoko yake ya Kiduo inaeleza hadhi na asili yake.

Pia, mwondoko wake kuelekea NGUZO MAMA unaonyesha nia na umuhimu wa NGUZO MAMA katika muktadha wa tamthilia, huku matumizi ya ngoma na wimbo vikiongeza uzito wa mawasiliano yasiyo ya maneno. Isitoshe, tunamuona mhusika mwingine akifika jukwaani kwenye dondoo lifuatalo:

> Wimbo unaendelea. BI PILI anajaribu kuinua NGUZO MAMA anashindwa. Wakati wimbo unaendelea, huku anaimba, anaingia BI TATU kwa miondoko ya Rumba. Amevaa vitenge vya Kizaire. Anacheza rumba kuelekea NGUZO MAMA (*Nguzo Mama*,.uk.3).

Hiki kipande kinaonesha BI PILI akijaribu kuinua NGUZO MAMA lakini anashindwa. Wakati wimbo unaendelea na huku akiimba, BI TATU anaingia kwa miondoko ya Rumba, akiwa amevaa vitenge vya Kizaire, na anacheza Rumba kuelekea NGUZO MAMA.

Hii inaashiria mawasiliano ya kitamaduni na hisia kupitia ngoma na mavazi, ikionesha utambulisho wa wahusika na uhusiano wao na NGUZO MAMA, yote yakiwa yamewasilishwa kupitia mawasiliano yasiyo ya maneno.

Kwa hivyo, walimu wa Kiswahili wanaweza kutumia tamthilia ya *Nguzo Mama* katika ufundishaji wa stadi za mawasiliano yasiyo ya maneno kwa njia mbalimbali. Kwanza, kupitia mienendo ya mwili na lugha uso (kinesiki), wanafunzi wanaweza kujifunza jinsi ya kutumia mkao, ishara na mienendo mingine ya mwili kuwasilisha ujumbe na hisia zao.

Pili, mwonekano wa mwili unaweza kufundishwa kwa kuzingatia jinsi mavazi na mwonekano wa nje yanavyoweza kuwasilisha utambulisho na sifa za mtu. Mwisho, lugha ya vitu inaweza kufundishwa kwa kuonyesha jinsi vitu kama mavazi, vifaa na mapambo vinavyotumika kama kanuni za mawasiliano yasiyo ya maneno. Kwa kutumia dondoo mbalimbali kutoka tamthilia hii,

walimu wanaweza kuwawezesha wanafunzi kuelewa na kutumia stadi hizi muhimu katika maisha yao ya kila siku na mawasiliano yao ya kijamii.

Isitoshe, utambuzi wa hisia ni stadi muhimu katika mawasiliano. Hii ni kwa sababu uwezo wa kuelewa na kutambua hisia za wengine huwezesha mawasiliano kuwa yenye ufanisi na yenye kueleweka zaidi. Wakati tunapoweza kutambua hisia za watu tunaozungumza nao, tunaweza kujua jinsi ya kujibu kwa njia ambayo ni sahihi na ya huruma, hivyo kujenga mahusiano mazuri na kuzuia migogoro. Kwa hiyo, katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano, ni lazima stadi hii ipewe nafasi inayostahili. Walimu wanaweza kutumia tamthilia ya *Nguzo Mama* kukuza stadi hii miongoni mwa wanafunzi wao. Kupitia maonesho ya wahusika mbalimbali na jinsi wanavyoshughulikia hisia zao na za wengine, wanafunzi watajifunza jinsi ya kutambua hisia na jinsi hisia hizo zinavyoathiri mawasiliano.

Kwa mfano, katika tamthilia hii, wahusika kama Bi Nane na Mwenyekiti huonesha hisia mbalimbali kama vile mshangao, hasira na furaha, na jinsi wanavyojibu hisia hizo katika mawasiliano yao. Kwa hivyo, wanafunzi wakijifunza kupitia wahusika hawa, watapata ujuzi muhimu wa kutambua na kushughulikia hisia katika mawasiliano yao ya kila siku.

Aidha, katika tamthilia husika, tunaona kwamba Bi Nane alipandwa na hasira, lakini aliweza kuzuia hisia zake na kutawala hasira yake. Hali hii inaonesha uwezo wa Bi Nane wa kufahamu hisia zake na za wengine na jinsi ya kuzidhibiti.

Alijua kwamba akiongea kwa hasira, angeweza kuzidisha matatizo yake. Badala yake, alikaa kimya na kutafakari kwa makini hali hiyo, akiwaza jinsi watu hao walivyopanga njama dhidi yake kama inavyoonekana kwenye dondoo lifuatalo:

> BI MSIMULIZI: Hasira zikampanda Bi Nane. Lakini vyema akazitawala. Mdomo akauma neno lisije mtoka. Akawatazama akawaza Hawa lao moja Huko wameshapanga mengi wameambizana Mpango umekamilika mie kuniangamiza Kamwe siwapi nafasi mwisho wake nione. Kimya kajikalia macho kawakodolea. Wakatazamana, wakatazamana Mwenyekiti anatafuta la kusema Bi Nne kiti hakimshiki (*Nguzo Mama*,.uk.25-26).

Hapa tunaona umuhimu wa utambuzi wa hisia katika mawasiliano. Bi Nane aliweza kutambua hisia zake za hasira na akachukua hatua za kuzidhibiti.

Kwa hiyo, walimu wa fasihi wanaweza kutumia tamthilia hii kukuza stadi za utambuzi wa hisia miongoni mwa wanafunzi wao kwa hatua zifuatazo. Kwanza, walimu wa fasihi wanaweza kukuza stadi za utambuzi na udhibiti wa hisia miongoni mwa wanafunzi wao kupitia maandishi ya maigizo. Kwa kuchambua vipande kama hicho kinachohusisha Bi Nane kudhibiti hasira zake, wanafunzi wanaweza kujifunza umuhimu wa kudhibiti hisia katika mawasiliano. Zoezi la kuigiza ambapo wanafunzi wanaigiza nafasi za Bi Nane na Mwenyekiti linawawezesha kueleza njia za vitendo za kushughulikia mwingiliano wenye hisia kali. Aidha, kuwaongoza wanafunzi kutafakari hisia zao wenyewe katika mazingira mbalimbali, kama alivyofanya Bi Nane, huweza kuwasaidia kuendeleza ufahamu wao binafsi kuhusu udhibiti wa hisia.

Hatua hii sio tu inaweza kuboresha uwezo wa wanafunzi wa kutambua na kudhibiti hisia, bali pia inakuza stadi za mawasiliano zenye busara na hekima, muhimu kwa ukuaji wao binafsi na mwingiliano mzuri na wengine.

Mwisho, tamthilia ya *Nguzo Mama* inaweza kutumiwa na walimu kukuza stadi ya ujasiri miongoni mwa wanafunzi. Ujasiri ni stadi inayohitajika katika mawasiliano fasaha. Stadi hii inaweza kukuzwa miongoni mwa wanafunzi kupitia uigizaji, mazoezi ya kuwasilisha darasani na mijadala. Kwa mfano, katika onesho la mwisho, tunamuona Bi Nne akitoa hotuba kwa hadhira kama inavyoonekana kwenye dondoo la hapo chini.

> BI NNE: (Kwa hadhira anahotubia. Anasema mfululizo) Haya yote tumeyafikiri. Maazimio tumeyapitisha mengi tena tunashukuru yote yamekubaliwa. Malezi ya watoto, hasa mwaka huu wa watoto, vituo vya watoto wadogo tutafungua kote nchini Patata. Miradi tutatilia mikazo, miradi ya kina aina, vilabu (*Nguzo Mama*, Uk.64-65).

Dondoo hili kutoka tamthilia ya *Nguzo Mama* ambapo Bi Nne anatoa hotuba, linatoa fursa nzuri kwa walimu kuendeleza stadi ya ujasiri miongoni mwa wanafunzi kupitia shughuli mbalimbali darasani. Kwanza kabisa, walimu wanaweza kuwaongoza wanafunzi kuchambua na kuelewa hotuba hiyo, wakilenga ustadi wa Bi Nne katika kufikisha ujumbe wake kwa hadhira. Kwa kujadili tabia yake ya kujiamini na lugha ya kuvutia, wanafunzi wanaweza kujifunza umuhimu wa kuzungumza kwa ujasiri na ufanisi katika mazingira ya umma. Zoezi hili linaweza kuboresha uelewa wao wa wahusika katika fasihi na kutoa mfano wa kuigwa kwa maendeleo ya uwezo wao wa kujieleza.

Pili, walimu wanaweza kuandaa mazoezi ya uigizaji ambapo wanafunzi wanaigiza sehemu ya hotuba ya Bi Nne au kuandaa hotuba zao wenyewe kuhusu mada muhimu kwao. Kuwahamasisha wanafunzi kujiandaa na kutoa hotuba mbele ya wenzao utawasaidia kuimarisha ujasiri wao katika kuzungumza hadharani. Kupitia maoni chanya na kutafakari kuhusu matokeo yao, wanafunzi wataweza kutambua maeneo ya kuboresha na kujenga uhakika wao katika uwezo wao wa kujieleza kwa ujasiri. Hatua hii si tu itaimarisha stadi zao za kuzungumza bali pia inawajengea uhakika katika kutoa mawazo na maoni yao kwa ufanisi.

Kwa hiyo, kwa kuingiza shughuli hizi zilizopendekezwa na tamthilia ya *Nguzo Mama* katika mtaala, walimu wanaweza kuunda mazingira ya darasani yanayosisitiza ujasiri na kuwawezesha wanafunzi kujieleza kwa uwazi na ujasiri. Hivyo basi, kupitia ufundishaji wa tamthilia hii, walimu wa Kiswahili wanaweza kufundisha stadi za mawasiliano yasiyo ya maneno kwa ufasaha.

### 4.3 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii inachambua kwa undani jinsi matokeo ya utafiti yanavyowasilishwa na kujadiliwa. Kwa hiyo inagawanywa katika sehemu kuu tano: utangulizi., lengo mahsusi la kwanza na la pili. Sehemu ya nne ni muhtasari wa sura ya nne.

# SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura ya tano inazingatia mambo muhimu matano. Mambo hayo ni utangulizi, muhtasari, ufaafu wa nadharia ya utafiti iliyotumika, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti uliofanyika ulikuwa na malengo mahususi mawili. Lengo mahususi la kwanza lilikuwa kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari sekondari teule wilayani Nyanza. Lengo mahususi la pili lilikuwa kuunda miongozo ya kutumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi ya mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Kwa hiyo, sehemu hii inatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti kwa kujiegemeza katika malengo mahususi mawili.

### 5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Lengo mahususi la kwanza la utafiti lilikuwa kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba fasihi andishi ina nafasi kubwa katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano. Kwanza, fasihi andishi ina nafasi muhimu katika kukuza uwezo wa mawasiliano, kama ilivyoonekana katika utafiti wetu. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba fasihi andishi inasaidia kuboresha uwezo wa mawasiliano kwa njia mbalimbali. Hata hivyo, walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyanza wanakumbana na changamoto, kama vile ukosefu wa mbinu bora za kufundishia na matumizi yasiyotosheleza ya fasihi andishi, ambayo yanaathiri ufanisi wa kufundisha stadi za mawasiliano.

Pili, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, fasihi andishi ina nafasi muhimu katika kukuza stadi za lugha kama kusoma, kuandika, kusikiliza na kuzungumza. Inaongeza uelewa wa lugha na maisha ya kibinadamu, na inajumuisha vipengele vyote vya lugha.

Hata hivyo, walimu wanakumbana na changamoto, kama mtazamo finyu kuhusu stadi za mawasiliano na tathmini zinazosisitiza zaidi stadi za kuandika na kusoma huku zikipuuzia stadi

za kuzungumza na kusikiliza. Mapendekezo ya kuboresha mbinu za ufundishaji kwa walimu na kujumuisha stadi zote za mawasiliano katika mafunzo na tathmini yametolewa.

Tatu, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, fasihi andishi ina uwezo mkubwa wa kukuza stadi stadi ya ujasiri. Aina mbalimbali za fasihi kama vile riwaya, mashairi na tamthilia, zinawasaidia wanafunzi kuboresha uwezo wao wa kujieleza kwa ujasiri. Kupitia uandishi wa kina na usomaji wa kazi za fasihi, wanafunzi wanajifunza jinsi ya kujieleza bila woga na kushiriki mazungumzo kwa ujasiri. Hata hivyo, hali halisi katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza inaonesha kwamba fasihi andishi haijatumiwa vyema katika kukuza ujasiri wa wanafunzi. Hii inatokana na changamoto kama vile muda finyuwa ufundishaji na kutozingatia stadi za mawasiliano wakati wa kuandaa somo

Mwisho, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, fasihi andishi inachangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza stadi ya utambuzi wa hisia kwa wanafunzi. Matini za fasihi hutoa nafasi kwa wanafunzi kuelewa na kujifunza kuhusu hisia za wahusika kupitia uandishi wa kina, hivyo kuboresha utambuzi wao wa kihisia. Kwa kusoma na kuchanganua kazi za fasihi, wanafunzi wanapata fursa ya kutambua na kuelewa hisia za wahusika, na hivyo kuwa na huruma na kushiriki kwa kina katika mawasiliano ya kihisia. Hata hivyo, katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza, fasihi andishi haijatumiwa ipasavyo katika kukuza utambuzi wa hisia kutokana na uelewa mdogo wa walimu kuhusu stadi hizi na changamoto nyingine zinazohusiana na ufundishaji.

### 5.2.2 Lengo Mahususi la Pili

Lengo mahususi la pili la utafiti lilikuwa kuunda miongozo ya kutumia fasihi andishi kukuza stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Ili kufikia lengo hili, mtafiti alitumia matini mbalimbali kuhusu miongozo ya kukuza stadi za mawasiliano kupitia ufundishaji wa fasihi. Zaidi ya hayo, mtafiti alifuata mhimili wa tatu wa nadharia ya mawasiliano, ambao unasisitiza kwamba mawasiliano yanachukuliwa kama ujumbe tofauti na mpya unaoundwa na kuundwa upya wakati watu tofauti wanapotafsiri tena ujumbe na kufikia hitimisho lao wenyewe.

Kwanza, utafiti uliofanyika ulitoa mwongozo wa utumiaji wa mbinu ya mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine. Mbinu hii inahusisha mwingiliano wa moja kwa moja kati ya wanafunzi

ambapo wanabadilishana maoni na mawazo yao kwa uhuru. Mbinu hii imebainika kuwa na ufanisi mkubwa katika kuboresha uwezo wa wanafunzi kujieleza na kuelewa mawazo ya wenzao kupitia fasihi andishi.

Pili, utafiti uliofanyika umetoa mwongozo wa utumiaji wa fasihi andishi kwa kutumia mbinu ya uumbaji wa mazingira salama ya kujifunzia na uhusiano wenye msaada. Ukosefu wa uhusiano wenye msaada kati ya wanafunzi na walimu huzuia kufikia malengo ya kufundisha na kujifunza. Kwa hivyo, walimu wanapaswa kuunda mazingira salama ya kujifunzia yanayozingatia uhusiano wenye msaada ili kuboresha stadi za mawasiliano kati ya wanafunzi. Mazingira haya yanajengwa kwa kuweka mikakati ambayo inawafanya wanafunzi wajisikie huru na kuheshimiwa, huku walimu wakionesha utayari wa kusikiliza na kutohukumu wanafunzi kwa makossa wanayoweza kufanay katika mawasiliano.

Tatu, utafiti uliofanyika umetoa mwongozo wa utumiaji wa mbinu ya kusikiliza kwa makini kama msingi wa mawasiliano yenye ufanisi na uelewa wa kweli. Kwa kusikiliza kwa makini wakati wa kujadili kazi za fasihi, wanafunzi wanapata fursa ya kuelewa kwa kina mawazo na hisia zilizopo katika kazi hizo. Hii inawasaidia kuboresha uwezo wao wa kujieleza kwa ufasaha na kujenga uwezo wa kufikiri kwa kina na kuwasiliana kwa weledi. Kwa hivyo, mbinu hii ni nyenzo muhimu katika kukuza stadi za mawasiliano katika Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari.

Mwisho, utafiti tulioufanya umebainisha jinsi tamthilia ya *Nguzo Mama* inavyoweza kutumika kama zana muhimu kwa walimu wa Kiswahili katika kukuza stadi za mawasiliano ya maneno na yasiyo ya maneno kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Tamthilia hii ilionekana kuwa chanzo kizuri cha mafunzo kwa walimu wanaotaka kufundisha stadi za kusoma, kuandika, kuzungumza, na kusikiliza. Kupitia maonesho ya wahusika na matukio mbalimbali, wanafunzi wanapata mifano halisi ya jinsi ya kutumia lugha katika muktadha tofauti. Jambo hili linawajengea uwezo wa kuelewa na kutumia mawasiliano ya lugha kwa ufanisi.

Zaidi ya hayo, njia zilizopendekezwa za ufundishaji, kama vile kuigiza, majadiliano na kazi za kikundi, zinaonesha jinsi walimu wanavyoweza kuleta mabadiliko chanya katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano.

Hivyo basi, tamthilia ya *Nguzo Mama* ilithibitishwa kuwa rasilimali muhimu katika kukuza stadi za mawasiliano ya maneno na yasiyo ya maneno baina ya wanafunzi wa Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyanza.

**5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti Iliyotumika**

Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Mawasiliano, ambayo iliasisiwa na S. F. Scudder mwaka 1980. Nadharia husika inaamini kwamba mawasiliano ni msingi wa maisha ya binadamu. Nadharia hii inaeleza kuwa binadamu wanawasiliana kwa kubadilishana mawazo, kufikisha ujumbe na kueleza hisia zao kwa kutumia sauti, ishara na vitendo mbalimbali.

Nadharia hii inachukuliwa kuwa muhimu katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya pili au ya kigeni, kwani inasisitiza umuhimu wa mawasiliano katika kuelewa na kujifunza lugha mpya. Hii ina maana kwamba walimu wanaweza kutumia nadharia hii kuboresha uelewa wa wanafunzi na uwezo wa kujieleza katika lugha ya Kiswahili, hivyo kuimarisha stadi zao za mawasiliano.

Kwa hiyo, ili kutimiza malengo ya utafiti, mtafiti alijiegemeza katika mihimili ya Nadharia ya Mawasiliano. Kwanza, kwa kutimiza lengo mahususi la kwanza mtafiti alijiegemeza katika mawazo ya Scudder (1980) na Robbins & Judge (2007); watafiti hawa wanasema kwamba mawasiliano ni mchakato wa kiufundi wa kuhamisha mawazo, ujumbe na hisia kutoka kwa mtu mmoja mmoja kwenda kwa mwingine.

Pia, wanabainisha kuwa mawasiliano ni mchakato ulio imara ambao una sheria zilizowekwa ambazo zinafaa kufuatwa. Mawazo haya yalishiriki katika kutathmini nafasi ya ufundishaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Hii ni kwa sababu, kupitia ufundishaji wa fasihi andishi, wanafunzi hujifunza mbinu na sheria mwafaka za kuwasilisha ujumbe na hisia zao kwa wengine.

Aidha, mhimili wa pili unasema kuwa mawasiliano ni mchakato wa kusambaza habari kutoka kwa mtumaji kwenda kwa mpokeaji ambaye kisha huifafanua na kuchukua hatua kulingana na ujumbe alioupokea. Wakati mpokeaji anashindwa kufafanua ujumbe kutokana na sababu mbalimbali, mchakato wa mawasiliano hauwezi kuwa na mafanikio.

Mhimili huu ilitufaa katika kuchunguza changamoto za utumiaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili. Pia, mhimili husika ulishiriki katika kubainisha mbinu za kuepukana na changamoto hizo.

Mwisho, mhimili wa tatu wa Nadharia ya Mawasiliano unaonesha kwamba mawasiliano yanachukuliwa kama ujumbe tofauti unaoundwa na kuundwa upya wakati watu tofauti wanapotafsiri tena ujumbe na kufikia hitimisho lao wenyewe. Mhimili huu ulikuwa faafu katika kuunda miongozo ya kutumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi ya mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Hii ni kwa sababu, ufundishaji wa fasihi andishi kwa Kiswahili unaruhusu wanafunzi kutafsiri na kuelewa maandiko ya fasihi kwa njia zao wenyewe. Jambo hili hujenga uelewa wa kina na wa kibinafsi wa maudhui na kuwezesha wanafunzi kuwasiliana kwa ufasaha kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

**5.4 Hitimisho**

Utafiti uliofanyika ulifanikiwa kutimiza malengo yake mawili mahususi. Kwanza, utafiti ulitimiza lengo la kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Matokeo ya utafiti husika, yameonesha kwamba fasihi andishi ina nafasi kubwa katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Imedhihirishwa kwamba fasihi andishi inawapa wanafunzi uwezo wa kuwasilisha mawazo yao na kufasili ujumbe kutoka kwa wengine kwa ufasaha. Pia, fasihi andishi huwezesha wanafunzi kuwasiliana na wengine kwa ujasiri, kuwasilisha na kutambua hisia za wengine kwa ajili ya kufanikisha mchakato wa mawasiliano.

Licha ya haya, matokeo ya utafiti yameonesha kwamba walimu wa Kiswahili hawafanikiwi kujumuisha kwa ufasaha ukuzaji wa stadi za mawasiliano wanapofundisha fasihi andishi kwa Kiswahili.

Hii ni kwa sababu ya changamoto tofauti ikiwa ni pamoja na muda wa kufundisha usiotosha na uelewa mdogo wa walimu kuhusu stadi za mawasiliano. Kwa kuepukana na changamoto hizi, matokeo ya utafiti yamependekeza mbinu tofauti. Mbinu hizi ni pamoja na matumizi ya TEHAMA, kufundishia kwa mijadala na midahalo, shughuli za darasani nje ya muda wa kawaida, michezo ya kuigiza na maigizo madogo.

Hatimaye, utafiti, ulifanikiwa kutimiza lengo mahususi lake la pili la kuunda miongozo ya kutumia fasihi andishi kukuza stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Matokeo ya utafiti yamebainisha miongozo ya utumiaji wa mbinu tatu. Kwanza, mawasiliano ya mtu mmoja kwa mwingine, ambayo inahusisha mwingiliano wa moja kwa moja kati ya wanafunzi. Pili, uumbaji wa mazingira salama ya kujifunzia na uhusiano wenye msaada kati ya wanafunzi na walimu. Tatu, kusikiliza kwa makini wakati wa kujadili kazi zafasihi, ili kuboresha uwezo wa kujieleza na kufikiri kwa kina. Mwisho, matokeo ya utafiti yamedhihirisha mfano wa namna ya kufundisha fasihi kwa kuegemea katika miongozo ya utumizi wa fasihi andishi katika kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi.

## 5.5 Mapendekezo

### 5.5.1 Mapendekezo kwa Wanafunzi wa Wanaojifunza Fasihi Andishi kwa Kiswahili

Wanafunzi wanapendekezwa kujitahidi kujifunza na kutumia Kiswahili kwa bidii kwa kuongea na kuandika mara kwa mara, kushiriki katika mijadala na mawasiliano ya kikundi, na kusoma kazi mbalimbali za fasihi andishi na simulizi. Aidha, wanapaswa kushiriki katika shughuli za ziada kama vile klabu za lugha na michezo ya kuigiza ili kuboresha ujasiri na stadi zao za mawasiliano. Hatimaye, ni muhimu kwa wanafunzi kutafuta msaada kutoka kwa walimu na wenzao ili kufanikisha lengo la kuwa na ujuzi bora wa lugha na mawasiliano kwa Kiswahili.

### 5.5.2 Mapendekezo Walimu Wanaofundisha Kiswahili

Walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza wanapaswa kutumia mbinu za ufundishaji zinazohusisha stadi za mawasiliano. Kwanza, walimu wanashauriwa kuingiza vipindi vya uwasilishaji na mijadala katika ratiba ya masomo ili kuwapa wanafunzi nafasi ya kujadili na kuchanganua kazi za fasihi andishi.

Pili, walimu wanapaswa kutumia mbinu za ufundishaji zinazochochea ushiriki wa wanafunzi, kama vile uigizaji wa tamthilia na usomaji wa riwaya kwa sauti, ili kuwasaidia wanafunzi kujenga ujasiri wa kujieleza na kuboresha stadi za kuzungumza, kusikiliza na stadi nyingine za mawasiliano yasoyo ya maneno.

Tatu, walimu wanashauriwa kufanya tathmini za mara kwa mara za stadi za mawasiliano kwa kutumia vipimo vya mdomo na maandishi ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanapata mazoezi

ya kutosha katika kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha. Hatimaye, walimu wanapaswa kushiriki katika mafunzo ya mara kwa mara kuhusu stadi za mawasiliano ili kuelewa vyema na kuweza kuzihusisha katika maandalizi ya masomo na ufundishaji wa fasihi andishi.

### 5.5.3 Mapendekezo kwa Watungaji wa Kazi za Fasihi Andishi katika Kiswahili

Watungaji wa kazi za fasihi andishi katika Kiswahili wanapaswa kuzingatia umuhimu wa kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wasomaji wao. Wanashauriwa kuandika kazi zinazochanganya matumizi ya lugha ya kisanaa na masimulizi yanayoakisi maisha halisi ya jamii ili kuwavutia na kuwaelimisha wasomaji. Vilevile, wanapaswa kujumuisha masuala yanayohusu stadi za mawasiliano ikiwemo utambuzi wa hisia, maadili, ujasiri na nyinginezo ili kusaidia wasomaji kujenga stadi za mawasiliano za kina. Aidha, wanashauriwa kushirikiana na walimu na wataalamu wa lugha ili kuhakikisha kazi zao zinatumika kwa ufanisi katika ufundishaji na ukuzaji wa stadi za lugha na mawasiliano katika shule za sekondari.

### 5.5.4 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu

Wizara ya Elimu ya Rwanda inashauriwa kuongeza muda wa kufundisha Kiswahili katika shule za sekondari ili kuruhusu ufundishaji wa kina wa fasihi andishi. Pia, inapaswa kuandaa masomo na warsha za mara kwa mara kwa walimu wa Kiswahili ili kuwawezesha kutumia mbinu bora za ufundishaji zinazokazia stadi za mawasiliano.

### 5.5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Kwanza, watafiti wa tafiti zijazo wanapendekezwa kufanya utafiti kuhusu sababu zinazowafanya wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda kukosa ujasiri wanapowasiliana na wengine hasa wanapotumia lugha ya Kiswahili. Utafiti huu utasaidia kubaini vikwazo vya kisaikolojia na kijamii vinavyoathiri ujasiri wa wanafunzi katika matumizi ya Kiswahili.

Pili, watafiti wengine wanafaa kufanya tafiti kuhusu umuhimu wa stadi za mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili kwa wahitimu wa shule za sekondari nchini Rwanda. Hii itatoa mwanga juu ya jinsi stadi hizi zinavyoathiri uwezo wa wahitimu kujieleza na kushindana kwenye soko la ajira.

Tatu, watafiti watakaofuata wanapendekezwa kufanya tafiti kuhusu nafasi ya fasihi simulizi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa madarasa ya Kiswahili

katika shule za sekondari nchini Rwanda. Fasihi simulizi inaweza kuwa nyenzo muhimu katika kukuza uwezo wa wanafunzi kuelewa na kujibu kwa ufanisi katika mawasiliano.

Mwisho, watafiti wengine wanapendekezwa kufanya tafiti kuhusu nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa madarasa ya Kiswahili katika shule za sekondari kwenye wilaya nyingine ambazo si Nyanza. Utafiti huu utasaidia kulinganisha na kuelewa tofauti za kimuktadha katika ufundishaji wa fasihi andishi na athari zake kwenye stadi za mawasiliano kwa wanafunzi katika maeneo mbalimbali.

Mwisho, watafiti wengine wanaombwa kufanya tafiti kuhusu namna ambavyo muda usiotosha kwa ajili ya kufundishia fasihi andishi huathiri ukuzaji wa stadi za mawasiliano kupitia ufundishaji wa fasihi andishi.

### 5.6 Muhtasari wa Sura ya Tano

Sura hii ya tano inatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti uliofanywa. Sura hii imegawanyika katika sehemu mbalimbali. Sehemu ya kwanza ni utangulizi. Sehemu ya pili ni muhtasari wa matokeo ya utafiti. Sehemu ya tatu inachambua kwa kina nadharia iliyotumika katika utafiti. Sehemu ya nne inatoa hitimisho. Sehemu ya tano inatoa mapendekezo na sehemu ya mwisho ni muhtasari.

## MAREJELEO


Ahmad, E.; Jailani M., & Yunus, F.M. A. (2011). The Implementation of Generic Skills at Technical Schools: Comparative Analysis in Different Platform, *Journal of Techno-Social*, 3(2), 23-41.

Al-Alawneh, M. K., Hawamleh, M. S., Al-Jamal, D. A., & Sasa, G. S. (2019). Communication Skills in Practice. *International Journal of Learning, Teaching and Educational Research*, 18(6), 1–19. https://doi.org/10.26803/ijlter.18.6.1.

Atkin, K. (2012). Communicate with Confidence: A Practical Guide. *Dental Nursing*, 8(9), 584-587. https://doi.org/10.12968/denn.2012.8.9.584.

Azimova, M. (2020). Self-confidence in Oral Performance. *Bulletin of Science and Practice*, 6(4), 444–452. https://doi.org/10.33619/2414-2948/53/52.

Barman, A., & Konwar, J. (2011). Competency Based Curriculum in Higher Education: A Necessity Grounded by Globalization, Revista Romaneasca Educatie, *Multidimessionala*, 3(6), 7-15.

Bennett, R. (2002). Employers' Demands for Personal Transferable Skills in Graduates: A content Analysis of 1000 Job Advertisements and an Associated Empirical Study. *Journal of Vocational Education & Training*, 54 (4), 457-476.

Bisamaza, M. (2022) Nafasi ya Hadithi katika Ukuzaji wa Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza: Mfano wa Shule Teule za Sekondari Wilayani Nyagatare Nchini Rwanda. *CHALUFAKITA*, 4 (4), 51-64.

Bizimana, J. (2022**).** *The role of cultural heritage in the preservation of Rwandan identity*. Tasnifu ya Umahiri katika Upangaji Elimu (Haijachapishwa).

Bowen, G. A. (2009). Document Analysis as a Qualitative Research Method. *Qualitative Research Journal*, 9(2), 27–40. https://doi.org/10.3316/qrj0902027.

Caruso, M., Colombi, G. A; Tebbit, S. (2017). Teaching how to Listen. Blended Learning for the Development and Assessment of Listening Skills in a Second Language, *Journal ofUniversity Teaching & Learning Practice*, 14(1), 207-221.

Charyulu, G. M. (2015). Enhancing Communication Skills through Language & Literature. *Journal of English Language and Literature*, *3*(1), 193-199.

Chepkemoi, N., & Wanyonyi, D. (2017). The Use of ICT in Teaching Kiswahili Play in Secondary Schools in Uasingishu County, Kenya. *European Scientific Journal*, ESJ, 13(25), 150. https://doi.org/10.19044/esj.2017.v13n25p150.

Ciesielska, M., Boström, K. W., & Öhlander, M. (2018). Observation Methods. In *Qualitative Methodologies in Organization Studies*, 4(2), 33–52). https://doi.org/10.1007/978-3-319-65442-3_2.

Collie, A. & Slater S. (2012). Literature Classroom: A Resource Book of Ideas and Communication Skills. *Contemporary Discourse*, 3, (1), 89 -94.

Cresswell, J. W. (2012). *Educational research*: Planning, Conducting, and Evaluating Quantitative and Qualitative Research (Toleo la 4 .). Los Angeles: SAGE Publications.

Creswell, J. W.  & Creswell, J. D. (2018). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Cuc, M. C. (2014). Development of a Communication System for Capitalizing Cultural Diversity. *Procedia Social and Behavioral Sciences*, 1 (4), 63-67.

Dennis, R. Laker & Powell, J.L. (2011). The Differences between Hard and Soft Skills and their Relative Impact on Training Transfer, *Human Resource Development Quarterly*, 22(1), 111–122.

Derakhshan, A., Tahery, F., & Mirarab, N. (2015). Helping Adult and Young Learners to Communicate in Speaking Classes with Confidence. *Mediterranean Journal of Social Sciences*, 6(2), 520-525.

Durga, S., & Mehrotra, V. (2022). Communication and its Vital Role in Human Life. *International Journal of Health Sciences*, 5940–5948. https://doi.org/10.53730/ijhs.v6nS5.10005.

Erdem, C., Bağcı, H., Koçyiğit, M., Altıner, C., Saykili, A., Polat, M., & Eğmir, E. (2019). *21st Century Skills and Education*. Kocatepe. Cambridge Scholars Publishing.

Evertson, W. (2011). *Handbook of Clasroom Management*. Routledge:New York.

Figueroa-Macias, E.M., & Andrade-Zambrano, C.D. (2022). Reading Comprehension in the Development of Communication Skills in High School Students. *International Journal of Linguistics, Literature and Culture*, 4(3), 122-131.

Frankel, R.J. & Warren, N.E. (2006). *How to Design and evaluate Research in Education?* (Toleo la 6). New York: McGraw Hill.

Frechtling, J. (2002).  An Overview of Quantitative and Qualitative Data Collection Methods. *The 2002 User-Friendly Handbook. Project Evaluation*, 7(2), 43-62.

Friston, K. J., Sajid, N., Quiroga-Martinez, D. R., Parr, T., Price, C. J., & Holmes, E. (2021). Active Listening. *Hearing Research*, *3(9),* 910-928. https://doi.org/10.1016/j.heares.2020.107998.

Garside, S.G. &Kleiner, B.H. (1991), Effective One-To-One Communication Skills. *Industrial and Commercial Training*, 23(7), 110-123. https://doi.org/10.1108/EUM0000000001586

Gamble, T. K., & Gamble, M. (2014). *Interpersonal Communication: Building Connections* (Toleo la 3.). London. Sage Publications.

Gomatam, C. (2015). Enhancing Communication Skills through Language & Literature. *Journal of English Language and Literature,* 3(1) 193-199.

Hartley, G. & Karinch, M. (2007). *I Can Read You Like a Book*: How to Spot the Messages and Emotions People Are Really Sending with Their Body Language. Franklin Lakes, NJ: Career Press.

Hassan, M. (2023). *Ethical Considerations- Types*, *Examples and Writing Guide*. https://shorturl.at/yQRY6.

Henderson, K., & Mathew-Byrne, J. (2016). *Developing Communication and Interviewing Skills*. In Skills for Social Work Practice (pp. 1–22). Macmillan Education UK. https://doi.org/10.1007/978-1-137-39027-1_1.

Hox, J. J., & Boeije, H. R. (2005). *Data Collection, Primary vs.* Secondary. In Encyclopedia of Social Measurement (pp. 593–599). Elsevier. https://doi.org/10.1016/B0-12-369398-5/00041-4.

Ilankumaran, M., & Deepa, P. (2018). Teaching Literature Enhances Communication Skills-a Study with Special Emphasis on Poetry. In *International Journal of Engineering & Technology*, *7(3). 312-345* www.sciencepubco.com/index.php/IJET

Jamshed, S. (2014). Qualitative Research Method-Interviewing and Observation. *Journal of Consulting Psychology*, 5(4), 87.

Johnson, M. (2018). *Literary Analysis and Emotional Intelligence*. University of Chicago Press, Chicago.

Kawulich, B. (2004). *Qualitative Data Analysis Techniques*. University of Alabama. https://www.researchgate.net/publication/258110388. Ilisomwa tarehe 4.5.2024

Khakasa, L.S. (2018). *Mikakati ya Kufundisha Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi katika Shule za Msingi za Kaunti ya Kakamega Nchini Kenya*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kombo, D.K. & Tromp, D.L.A. (2006). *Proposal and Thesis Writing*: An Introduction. Nairobi: Pauline's Publications.

Kothari, C.R. (2012). *Research Methodology- Methods and Techniques.* New Delhi. Willey Eastern Limited.

Lang'at, P. (2020). *East Africa: Kiswahili Goes to School in South Africa*. https://allafrica.com/stories/202001110056.html.

Lugano, A. (2021). *Ufundishaji wa Fasihi: Mbinu za Kujenga Uelewa na Kujiamini kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Lukenchuk, A. (2023). *Methodology Choosing among Paradigms and Research Designs*. https://about.jstor.org/terms.

Martín, R. D. (2014). The Importance of Communication Competency for Employability. *Procedia-Social and Behavioral Sciences*, 139, 387–394.

Martins, F. S., Cunha, J. A. C., & Serra, F. A. R. (2018). Secondary Data in Research – Uses and Opportunities. *Revista Ibero-Americana de Estratégia*, 17(04), 01–04.

Maxwell, J. A. (2005). *Qualitative Research Design: An Interactive Approach* (Toleo la 2.). Thousand Oaks, CA: Sage.

Mehrabian, A., Wiener, M. (1967). Decoding of Inconsistent Communications. *Journal of Personality and Social Psychology*. 6 (1), 109–114.

Melly, J. K., & Mohochi, E. S. (2023). Matumizi ya Kiswahili katika Mawasiliano na Uongozi wa Kidini katika Shule za Upili Nchini Kenya: Mfano wa Shule ya Wasichana ya Itigo. *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), 339–349. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422.

Miles, M. B., Huberman, A. M., & Saldana, J. (2014). *Qualitative Data Analysis*: A Methods Sourcebook. Sage Publications.

Morris, S. (2021). How Reading Enhances Self-Assurance. *Lara Law*. https://www.laralaw.com/reading-builds-confidence

Muhando, P. (2010). *Nguzo Mama*. Tanzania Publisher House. Dar-es-Salaam.

Muste, D. (2016) *The Role of Communication Skills in Teaching Process*. Journal of Consulting Psychology. 31 (3), 430–434, doi: 10.15405/epsbs.2016.12.52.

Mwakagele, C. (2016). *Lugha ya Kiswahili Ipewe Nafasi Inayostahili*. Muungwana Lazima Nilonge. Kutoka https://www.ippmedia.com/sw/safu/lugha-ya.

Ngọc, T. T. (2021). Communication Skills and Their Importance in Effective Interpersonal Interactions. *International Journal of Communication Research*, 11(2), 77-85.

Nguyen, H., Warren, W., & Fehring, H. (2014). Factors Affecting English Language Teaching and Learning in Higher Education. *English Language Teaching*, *7*(8). https://doi.org/10.5539/elt.v7n8p94.

Niyirora, E. & Mlaga, W. K. (2022). Ukuzaji wa Stadi ya Tafakuri Bunifu kupitia Ufundishaji wa Fasihi: Mfano wa Shule Teule Nchini Rwanda. *MULIKA*, 42 (2), 126-144.

Novik N. N. (2015). A Model of Developing Communication Skills among Adolescents with Behavioral Problems. *International Journal of Environmental & Science Education*, 10(4), 579-587.

O'Connor, P., & McCartney, R. (2007). The Impact of Supportive Relationships on Students' Communication Skills Development. *Journal of Education Research*, 30(2), 45-58.

Ordho, A.J. & Kombo, D.K. (2003). *Research Methods*, Nairobi: Kenyatta University, Institute of Open Learning.

Otieno E.A., Inyani, K.S. & Shikuku (2020). *Matumizi ya Lugha-Ishara katika Ufundishaji wa Sarufi ya Kiswahili kwenye Shule za Msingi Nchini Kenya*. University of Science and Technology of Murilo Press.

Pastory, W. S. (2016). *Lahaja za Kiswahili kwa Ujumla*. Berkeley: University of California Press.

Patki, L. (2013). *Development of Speaking Skills through Literature*. Cambridge University Press.

Paul, G. & Reem, A.-M. (2004). *Strategies for Communication Skills Development*. In Raymond Lister & Alison Young (wahariri.), Conferences in Research and Practice in Information Technology. Australian Computer Society.

Pearson, J. C., Nelson, P. E. Paul E., Titsworth, S., & Hosek, A. M. (2017). *Human Communication* (Toleo la 6.). New York, MA: McGraw-Hill Education.

Peck, J. (2005). Struggling with the Creative class. *International Journal of Urban and Regional Research*, 29,740–770.

Priyadharshini, J., & Hameed, M. A. M. S. (2018). Developing Communication Skills in English through Literature. *International Journal of Social Science and Humanities Research, 6*(1), 30-32. Retrieved From Http://Www.Researchpublish.Com

Pradesh, A., Toppo, T., & Philomina, D. (2021). A Study on the Problems in Communication Skills Faced by the Teachers in the Secondary Schools of Namsai District in. *IT in Industry*, *9*(3), 2021.

Radhika, S. (2020). Communication skills: The Foundation of Successful Teaching. *Journal of Educational Development*, 15(2), 45-56. https://doi.org/10.1016/j.jed.2020.03.007.

Rachella, M. (2021). Bridging the Gap: Practical Approaches to Developing Communication Skills in Language Teaching. *International Journal of Language Education*, 15(2), 30-45.

Rao, D.V. & Charyulu M. (2015). Enhancing Communication Skills through Language & Literature. *Journal of English Language and Literature*, 3(1):193-199.

REB. (2015). *Competence Based Curriculum*: Curriculum Framework Pre-Primary to Upper Secondary. Kigali.

Rogers, L. E., & Farace, R. V. (2017). Analysis of Relational Communication in Dyads: New Measurement Procedures. *Human Communication Research*, 1(3), 222–239.

Robbins, S. P., & Judge, T. A. (2007). *Organizational behavior* (12th ed.). Upper Saddle River, Pearson Education.

Rosalyn, S. (2020). *Effective Communication in the Classroom: Skills for Teachers*. Cambridge University Press.

Rustham, A. T. P., Rusadi, M. I., Sakinah, S., Kristanti, A., & Cholisha, F. A. (2022). *Empathic Communication Skill Optimization for Minimizing Children's Excessive Use of Gadgets*. https://doi.org/10.2991/assehr.k.220203.008.

Sarpparaje, A. (2019). Importance of Communication Skills for Secondary School Graduates: A Comprehensive Perspective. *Journal of Education and Development*, 25(1), 50-65.

Scudder, S. F. (1980). *Communication Theory and Practice*. Academic Press. New York.

Seiler, W. J., & Beall, M. L. (2011). *Communication: Making Connections* (Toleo la t.). Pearson Education.

Sen, S., Mahendra, A., & Patnaik, P. (2015). *Communication and Language Skills*. Cambridge University Press.

Sirbu, A. (2015). The Significance of Language as a tool of Communication. *Scientific Bulletin of Naval Academy*. 18(2), 405-406.

Sharma, M., Devi, M., Dangoria, R., & Jain, V. (2022). Literature Enhances Communication Skills: A comprehensive review. *World Journal of English Language*, *12*(3), 157-163 https://doi.org/10.5430/wjel.v12n3p157.

Smith, J., & Johnson, L. (2010). Understanding the Interpretivist Paradigm: A Study of How People Interpret and Define Their World. *Journal of Social Science Research*, 20(3), 45-60.

Sridhar, A. (2012). *Developing Communication Skills*. https://www.academia.edu/1464158

Standard Digital (2019). *Skill-Based Training Necessary to Curb Shortage of Employable Youth in Kenya.* International Labor organization. Bangkok. Thailand.

Sylvester, M. K. (2022). The Literature in English Syllabus through the 21st Century Skills Lens: A Hermeneutic Analysis. International Journal of Research Publication and Reviews, 04(01), 1681–1689. https://doi.org/10.55248/gengpi.2023.4147.

Terrell, R. S. (2022). *Writing a Proposal for Your Dissertation Guidelines and Examples*. Nova Southeastern University. Guilford Press.

Tibategeza, E.R., & Plessis, T. (2018). The Prospects of Kiswahili as a Medium of Instruction in the Tanzanian Education and Training Policy. *Journal of Language and Education*, 4(3), 88-98.

Trilling, B.; Fadel, C. (2009). 21st Century Skills: Learning for Life in Our Time. *Journal of Consulting Psychology*.,31 (3), 248–252.

Tubbs, S.L., Moss, S., Mulyana, D. (2000). Human Communication: Training Transfer. *Human Resource Development Quarterly*, 22(1), 111–122.

Valente, F. (2016). Empathy and Communication: A Model of Empathy Development. *Journal of New Media and Mass Communication*, 3(1), 1–24. https://doi.org/10.18488/journal.91/2016.3.1/91.1.1.24.

Venkateswar, R. D., & Mohana, C. G. (2015). Enhancing Communication Skills through Language & Literature. *Research Journal of English Language and Literature (RJELAL)*, *3*(1), 193-198. Ilisomwa tarehe, 08.03. 2024 kutoka Http://Www.Rjelal.Com

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers.

Williams, J., & Lee, J. (2019). Creating Safe Learning Environments and Supportive Relationships to Enhance Literature Instruction and Communication Skills Development. *Educational Research Review*, 14(2), 45-67.

Yang, P. (2011). Nonverbal Aspects of Turn Taking in Mandarin. Language and Discourse, 2, 99–130.

## VIAMBATISHO

**Kiambatisho I. Mwongozo wa Usaili kwa Walimu wa Kiswahili**

1. Je, stadi za mawasiliano ni zipi? (What are communication skills?)
2. Je, kama mwalimu wa Kiswahili, unatumiaje fasihi andishi katika kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi? (As a Kiswahili teacher, how do you use written literature to enhance communication skills among students?)
3. Je, ni changamoto zipi unazikabiliana na zo unapotumia fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi? (What challenges do you face when using written literature to develop communication skills in Kiswahili among students?)
4. Je, ni mbinu gani unazozitumia ili kuepukana na changamoto za utumiaji wa fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi? (What strategies do you use to overcome challenges in using written literature to develop communication skills among students?)
5. Je, fasihi andishi ina nafasi gani katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule ya sekondari hii? (What role does written literature play in developing communication skills in Kiswahili among secondary school students?

**Kiambatisho II. Mwongozo wa Ushuhudiaji kwa Somo la Fasihi Andishi katika Kiswahili Likifundishwa Darasani**

<table>
<tr><td colspan="3">1. Utumiaji wa Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano</td></tr>
<tr><td rowspan="3">a) Mwalimu alipoandaa andalio la somo la fasihi andishi, alihusisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika malengo ya ufundishaji na ujifunzaji au katika sehemu ya Uwezo wa Jumla na Maswala Mtambuka?</td><td>Ndiyo</td><td>Hapana</td></tr>
<tr><td colspan="2">Ikiwa jibu ni ndio, vipi?<br>………………………………………..</td></tr>
<tr><td colspan="2">Ikiwa jibu ni hapana, athari ni zipi?<br>………………………………………..</td></tr>
<tr><td rowspan="3">b) Je, mwalimu anahusisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano anapofundisha, somo la fasihi andishi?</td><td>Ndiyo</td><td>Hapana</td></tr>
<tr><td colspan="2">Ikiwa jibu ni ndio, vipi?<br>………………………………………..</td></tr>
<tr><td colspan="2">Ikiwa jibu ni hapana, athari ni zipi?<br>………………………………………..</td></tr>
<tr><td rowspan="3">c) Je, mwalimu wa fasihi andishi anatumia mbinu za ufundishaji zianazoweza kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi?</td><td>Ndiyo</td><td>Hapana</td></tr>
<tr><td colspan="2">Ikiwa jibu ni ndio, ni mbinu gani?<br>………………………………………..</td></tr>
<tr><td colspan="2">Ikiwa jibu ni hapana, ni mbinu gani na athari ni zipi?<br>………………………………………..</td></tr>
<tr><td rowspan="3">d) Mwalimu anahusisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano anapoandaa tathmini kuhusu somo la fasihi andishi?</td><td>Ndiyo</td><td>Hapana</td></tr>
<tr><td colspan="2">Ikiwa jibu ni ndio, ni mbinu gani?<br>………………………………………..</td></tr>
<tr><td colspan="2">Ikiwa jibu ni hapana, ni mbinu gani na athari ni zipi?<br>………………………………………..</td></tr>
</table>

| **2. Changamoto za Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano Kupitia Ufundishaji wa Fasihi** | |
|---|---|
| **Changamoto** | **Mikakati ya Kuepukana na Changamoto** |
| 1. ……………………………….. | 1. ……………………………….. |
| 2. ……………………………….. | 2. ……………………………….. |
| 3. ……………………………….. | 3. ……………………………….. |
| 4. ……………………………….. | 4. ……………………………….. |

**Kiambatisho III. Mwongozo wa Uchanganuzi Matini**

| Jina la Matini | Mwandishi & Mwaka | Data Kutoka kwenye Matini |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

**Kiambatisho IV. Kibali cha Kukusanya Data kutoka Chuoni**

UNIVERSITY of RWANDA

**COLLEGE OF EDUCATION**

**RESEARCH AND INNOVATION UNIT**

Rukara, 19th June 2024
Ref: DRI-CE/023(b)/EN/gi/2024

**The Mayor**
**Nyanza district**
**Southern province**
**Rwanda**

**Re: A Research recommendation letter for Mr Magnifique Idahemuka (Reg No: 220018613)**

I am pleased to introduce **Mr Magnifique Idahemuka:** our student enrolled in the Master of Education in Kiswahili Education at the School of Education of UR-CE. He is conducting research entitled: **"The Role of Written Literature in Developing Communication Skills in Kiswahili: A Case Study of Select Secondary Schools in Nyanza District."** His research will involve students of the combination of languages and teachers of Kiswahili in selected secondary schools of Nyanza district.

Thus, we kindly request his permission to collect data from the identified secondary schools of Nyanza district.

Your support to him in conducting this study is highly appreciated.

COLLEGE OF EDUCATION — UNIVERSITY of RWANDA — RESEARCH AND INNOVATION UNIT

**Assoc. Prof. Eugene NDABAGA**
Director of Research and Innovation
University of Rwanda-College of Education
E-mail: ndabagav@yahoo.ie
Mobile: +250788308862

**Cc:**

- Principal, UR-CE
- Dean, School of Education
- Dr Wallace K. Mlaga (Supervisor)

EMAIL: dri.ce@ur.ac.rw P.O. Box: 55 Rwamagana WEBSITE: www.ur.ac.rw

**Kiambatisho V. Idhini ya Itikeli ya Utafiti**

UNIVERSITY of RWANDA

COLLEGE OF EDUCATION

**RESEARCH AND INNOVATION OFFICE**

Rukara, 19th June, 2024
Ref: DRI-CE/023(a)/ EN/gi/2024

**Mr Magnifique Idahemuka**
**Reg No: 220018613**
Master Student
Masters of Education in Kiswahili Education
School of Education
UR-CE

Dear Mr Idahemuka,

**RE: RESEARCH ETHICAL CLEARANCE FOR YOUR STUDY**

Following your application for research clearance for your study entitled: **"The Role of Written Literature in Developing Communication Skills in Kiswahili: A Case Study of Select Secondary Schools in Nyanza District;"**

Having reviewed your application and being satisfied with your protocol (your research topic, interview schedule, and informed consent): your study is ethically acceptable. This ethical clearance shall last for 18 months and is renewable upon your request and presentation of the progress report to the UR-CE Research Screening and Ethics Clearance Committee (RSEC-C) through the Research and Innovation Unit. Please note that you will have to apply for ethical clearance before making changes in the protocol during the implementation phase. The Research and Innovation Unit shall receive a final copy of your study report at the end of your study.

We wish you success in your study.

COLLEGE OF EDUCATION — RESEARCH AND INNOVATION UNIT

**Assoc. Prof. Eugene NDABAGA**
Chairperson, UR-CE RSEC-C
Director of Research and Innovation Unit
Tel.: 250788308862
Email: ndabagav@yahoo.ie
UR-College of Education
**Cc:**

- The Principal, CE
- Dean, School of Education
- Dr Wallace K Mlaga, Supervisor

EMAIL: dri.ce@ur.ac.rw P.O. Box: 55 Rwamagana WEBSITE: www.ur.ac.rw

## Kiambatanisho VI. Kibali cha Kukusanya Data kutoka kwa Wilaya ya Nyanza

Repubulika y'u Rwanda
Intara y'Amajyepfo
**Akarere ka Nyanza**

**B.P. 62 NYANZA**
**Tél: 6262**
**E- mail:info@nyanza.gov.rw**
**Website : www.nyanza.gov.rw**
**TIN :101895086**

---

Nyanza,ku wa 06../.05.../2024
Réf :...1.2.4.7..../07/02/01/24

**IDAHEMUKA Magnifique**

**Tel: 0788703595**

**Email : magnifiqueidahemuka@gmail.com**

**Re: Your request for Academic Research**

Basing on your letter requesting for Academic Research in College du Christ-Roi, ES Nyanza and GS Kigoma in Nyanza District, I have the pleasure to inform you that you are given an opportunity to carry out your Academic Research.

However, you are requested to use the information given to you for academic purposes only and you will work closely with the above mentioned Schools in collaboration of Education Unit.

Best regards,

**NTAZINDA Erasme**
**Mayor of Nyanza District**

Cc:

- ✓ Acting District Executive Secretary ;
- ✓ Director of Education Unit ;
- ✓ Head Teacher of College du Christ-Roi ;
- ✓ Head Teacher of ES Nyanza
- ✓ Head Teacher of GS Kigoma;

***ABADAHIGWA BA NYANZA : DUFATANYE, DUHINDURE, DUTERE IMBERE***

**Kiambatisho VII. Mpango Kazi**

| | Kazi | Wakati | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2023 | | | 2024 | | | | | | | |
| | | Okt | Nov | Des | Jan | Feb | Mac | Apr | Mei | Jun | Jul | Ago |
| 1 | Kukamilisha ikisiri ya utafiti | | | | | | | | | | | |
| 2 | Kuandaa sura ya kwanza ya pendekezo la utafiti | | | | | | | | | | | |
| 3 | Kupitia maandiko nakutengeneza sehemu ya mapitio ya maandiko | | | | | | | | | | | |
| 3 | Kuandaa methodolojia ya utafiti | | | | | | | | | | | |
| 5 | ➢ Kukamilisha pendekezo la utafiti<br>➢ Kuomba vibali vya kukusanya data | | | | | | | | | | | |
| 6 | Kukusanya data | | | | | | | | | | | |
| 7 | Kuaandaa sura ya nne ya tasnifu<br>➢ Kuchanganua data<br>➢ Kufasili data<br>➢ Kuwasilisha data | | | | | | | | | | | |
| 8 | Kuandaa sura ya tano ya tasnifu | | | | | | | | | | | |
| 9 | ➢ Kukusanya ripoti ya utafiti<br>➢ Kutetea tasnifu | | | | | | | | | | | |
| 10 | Kuchapisha makala ya mradi wa utafiti | | | | | | | | | | | |

**Chanzo: (Mtafiti, 2024)**

**Imeandaliwa na**: Magnifique IDAHEMUKA
**Saini:**

**Imeidhiniswa na Msimamizi**: Dkt. Wallace. Kapele. Mlaga

**Saini:**